**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Ishirini na Nane – Tarehe 6 Juni, 2014**

*(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, atakayeuliza swali la kwanza ni Mheshimiwa Felix Mkosamali.

Na. 197

**Huduma za Zahanati – Muhambwe**

**MHE. FELIX FRANCIS MKOSAMALI** aliuliza:-

Vijiji vya Magarama, Kigina na Nyarulanga katika Jimbo la Muhambwe havina Zahanati:-

Je, Serikali imefikia wapi katika kuvipatia vijiji hivyo huduma ya zahanati?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mbunge wa Jimbo la Muhambwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Vijiji vya Kigina, Magarama na Nyarulanga, vilivyopo katika Jimbo la Muhambwe, havina Zahanati. Ujenzi wa Zahanati nchini unafanyika kupitia Mpango wa Fursa na Vikwazo Katika Maendeleo, ambapo Wananchi wenyewe huibua Miradi ambayo inazingatia changamoto zilizopo. Halmashauri huchangia gharama kidogo za utekelezaji wa Miradi hiyo kwa kuwezesha upatikanaji wa vifaa pamoja na usimamizi.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Zahanati katika Kijiji cha Kigina umekamilika kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 na ujenzi wa nyumba ya Mganga uko katika hatua ya mwisho, ambapo Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, ilitenga jumla ya shilingi milioni 20. Aidha, ujenzi wa jengo la wagonjwa *(OPD)* wa nje katika Kijiji cha Magarama upo hatua ya mwisho kukamilika. Serikali imetenga shilingi milioni 23 katika bajeti yake ya mwaka 2014/2015 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Nyarulanga ni kipya ambacho awali kilikuwa Kitongoji katika Kijiji cha Nyankwi. Serikali inaielekeza Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo kupitia mapato yake ya ndani, kuweka kipaumbele cha ujenzi wa Zahanati katika Kijiji cha Nyarulanga.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Wananchi wa vijiji hivyo wanapata huduma za afya katika Zahanati za Busunzu, Kichanga, Kagezi na Kiganga, ambazo ziko umbali wa wastani wa kilometa saba mpaka nane. Aidha, Wananchi wanapata huduma ya afya ya mkoba, ambapo wahudumu wa afya wanakwenda kwenye vijiji hivyo kutoa huduma za afya ya uzazi wa mama na motto, ikiwemo chanjo na utoaji wa *Vitamin* A kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa kwenye Kijiji cha Kigina, tayari Zahanati imekamilika toka mwaka 2012/2013; kwa nini Serikali isipeleke sasa mtumishi ili aweze kuanza kuhudumia hao Wananchi ambao wanatembea zaidi ya kilometa nane kutafuta huduma hii?

(ii) Ujenzi wa Zahanati katika Kijiji cha Magarama una zaidi ya miaka sita. Serikali inawathibitishia Wananchi nini kwamba, fedha hizi zinazotengwa mwaka huu zitakwenda ili waache kusumbuka kutembea mwendo mrefu? Huko ni mbali sana, mimi huwa nikipita gari linajaa maji mpaka kwenye *carrier*. Serikali inawathibitishia vipi kwamba fedha mwaka huu zitakwenda ili Zahanati hii iweze kukamilika?

**SPIKA:** Hiyo inakuwa kama *submarine* hivi! Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mkosamali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, niweke katika *record,* mimi nilipokuwa nazungumza na watu wa Kibondo na huko kwake, nilitaka kupata pia *record* ya Mbunge, kama yeye mwenyewe anawahamasisha Wananchi ili wajitume katika shughuli za maendeleo. *It is on record* kwamba, Mheshimiwa Mkosamali anafanya hivyo; kwa hiyo, napenda kumpongeza sana kwa kazi anayofanya. (*Makofi*)

Pili, kuhusu hiki, ndiyo kwa sababu tunalo tatizo pia wakati mwingine Mbunge anaweza akawa anatumika kuzuia maendeleo katika eneo lake. Nchi hii isingeweza kufika hapa ilipofika kama watu wake wasingekuwa wanajituma wenyewe kwa ajili ya kuleta maendeleo. Tukingoja Serikali yenyewe ifanye hivyo itakuwa ngumu.

Mheshimiwa Spika, sasa kuhusu hii Zahati ambayo imekamilika na ambayo anaihitaji, kwa heshima tuliyonayo kwa jambo hili, tutahakikisha tunapata. Tutazungumza na wenzetu, Mama Celina Kombani alisema kuhusu Watumishi, tupate walau mtu mmoja ambaye atakwenda pale. Nitaagiza leo kuhakikisha kwamba, mtumishi anakwenda katika Zahati hii ambayo imekamilika. Kwa sababu Wananchi wamefanya kazi yao kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hizi fedha ambazo zimetamkwa hapa shilingi milioni 20, ni kweli tumecheki katika MMAM, hela zao za MMAM ni shilingi milioni 147 na tumecheki tumekuta hakuna hela ambazo zimekwenda pale.

Mheshimiwa Spika, naomba nikiri mbele yako, hata hizo milioni 20 ambazo tumeahidi hapa, tutasukuma ili kuhakikisha hela hizi zinakwenda katika mwaka wa fedha huu tulionao kabla hatujaingia katika mwaka unaokuja.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, ningependa kumwuliza Mheshimiwa Waziri, pamoja na ziara ambayo alifanya Wilayani Kilwa, Wananchi wamehamasika sana kwenye kujitolea kujenga Zahanati. Nini mkakati wa Serikali hasa Serikali za Mitaa kuhakikisha watumishi wa kutosha wanapelekwa kuweza kukidhi mahitaji badala ya kutumia nguvu za Wananchi na majengo kuchakaa kabla hayajatumika?

**SPIKA:** Ni nchi nzima siyo huko kwako, yeye hakujui huko. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana umeweka vizuri; hii *problem* ni *problem* ya nchi nzima na kama tulivyomsikia Mheshimiwa Mama Celina Kombani, alipokuwa anaeleza hapa kwamba, tumepata idadi kubwa. Utaratibu ambao tumejiwekea sasa hivi ni kwamba, Wizara ya Afya wakishamaliza tu na wako hapa wanasikia, wanapeleka moja kwa moja kule. Kilwa aliposema nimekwenda ni kweli nimekwenda na tatizo hili lipo na pia lipo nchi nzima, lakini nitajaribu ku-*trace* kuona *allocation* hizi zilizofanyika tuone Kilwa katika hili eneo wanawezaje wakasaidiwa.

**SPIKA:** Nimesema siyo kumwingilia, maswali ya nyongeza lazima yawe ya jumla. Ukimwuliza mtu sehemu ya kwako unakotokea, hakujiandaa kwa hilo, ndiyo maana nikasema basi nchi nzima. Kwa hiyo, tumefanya vizuri, tuendelee na swali linalofuata; Mheshimiwa Lolesia Bukwimba!

Na. 198

**Kupandishwa Hadhi Barabara ya Katoro – Karumwa**

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA** aliuliza:-

Je, ni lini Barabara ya Katoro – Busanda – Kamena - Mwingiro hadi Karumwa itapandishwa hadhi kuwa ya Mkoa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara kutoka Katoro – Karumwa awali ilikuwa ikiitwa Barabara ya Mang'ombe, ambayo ni muunganiko wa barabara nne ambazo ni Katoro – Busanda, Nyalwanzaja – Kamena – Mwingiro na Mwingiro – Karumwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria na taratibu za kupandisha hadhi barabara kuwa Barabara ya Mkoa, vigezo vinavyozingatiwa ni kwamba, barabara husika lazima iwe

inaunganisha Barabara Kuu na Makao Makuu ya Wilaya au Makao Makuu ya Mkoa na iwe inaunganisha Makao Makuu ya Makoa na Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, katika hatua za awali, pendekezo hili limeshapitishwa na kujadiliwa katika Kamati za Ushauri ya Wilaya na Bodi ya Barabara ya Wilaya. Aidha, maombi hayo yatawasilishwa katika Vikao vya Kamati ya Ushauri ya Mkoa na Bodi ya Barabara ya Mkoa, ambavyo vimepangwa kufanyika mapema katika Mwaka wa Fedha wa 2014/2015. Vikao hivyo vikiridhia pendekezo hilo, maombi ya kupandisha hadhi barabara hii, yatawasilishwa kwa Waziri wa Ujenzi, ambaye ndiye mwenye dhamana kwa ajili ya kupandisha hadhi barabara hiyo kuwa ya Mkoa na iweze kuhudumiwa na *TANROADS*.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ya kutoka Katoro, Karumwa inaunganisha kati ya barabara kuu ya kutoka Geita kwenda Kagera, lakini pia inaunganisha Makao Makuu ya Wilaya Mpya ya Nyang'hwale ambayo ni Karumwa. Kwa hiyo, ni barabara muhimu sana kiuchumi katika Jimbo la Busanda na Wilaya ya Geita na Mkoa Mpya wa Geita kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe ni Makamu Mwenyekiti kwenye Bodi ya Barabara ya Mkoa na tulikaa kikao chetu tukapitisha Barabara hii katika Bodi ya Barabara ya Mkoa. Sasa ningependa kujua ni lini barabara hii itapandishwa hadhi kuwa Barabara ya Mkoa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, huo ndiyo utaratibu ambao Mheshimiwa Naibu Waziri ameusema. Lazima zipite katika vikao ambavyo vimeainishwa kwenye Sheria ya Barabara Namba 13 ya Mwaka 2007 na Kanuni zake. Barabara hizi ni lazima zikidhi vigezo vinavyotakiwa. Sasa kama anasema yeye ni Makamu Mwenyekiti na walishakaa, basi tutafuatilia tuweze kuona kama maombi hayo yameshaletwa Wizara ya Ujenzi na kule tumeweka Kamati Maalum, ambayo itapitia tena waende wakatembelee zile barabara na kuona kama kweli zinakidhi vigezo na baada ya hapo, Wizara itaweza kuipandisha hadhi barabara hiyo.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa najua sasa hivi Dar es Salaam kuna msongamano mkubwa sana wa magari; na kwa kuwa barabara ya kutoka Chanika mpaka kwenda Homboza, bado iko katika Halmashauri ya Wilaya ya Ilala pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe, ambayo changamoto yake katika urekebishaji inakuwa ni kubwa sana; na kwa kuwa katika vikao vyetu vya Mkoa tulipendekeza barabara hii ipandishwe kuwa barabara ya Mkoa:-

Naomba kupata kauli ya Serikali, je, tumefikia vipi katika kuhakikisha barabara hiyo inapandishwa kuwa Barabara ya Mkoa ilimradi watu wanaoishi Homboza na kufanya kazi Dar es Salaam wapate nafuu zaidi ya kufika katikati ya mji?

**SPIKA:** Maswali ya nyongeza unakwenda kwenye *specification* za kwenu, sasa mkipata majibu mazuri haya, yakiwa hivyo hivyo yawe hivyo hivyo. Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jafo, Mbunge wa Kisarawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jibu hapa halitaweza kutofautiana na jibu hili ambalo anatoa Naibu Waziri wa Ujenzi. Nitakachofanya hapa nitakwenda ku-*check,* kwanza, kujua hawa wako katika *inventory,* wamefuata utaratibu, *DCC,* wamekwenda kwenye *RCC,* wamekwenda kwenye Bodi ya Barabara na *the bottom line is,* hapa hatuwezi kutofautiana na wenzetu wa Ujenzi. Tukiona haya yote yamekamilika, mwenye dhamana ya kusema sasa nakubali barabara hii iwe barabara ambayo itahudumiwa na *TANROADS* ni Waziri wa Ujenzi. Kwa hiyo, yale majibu aliyotoa kwa ajili ya Busanda na Nyang'hwale, ndiyo majibu hayo hayo. Hapa hatutengui Torati, tunaimarisha Torati! *(Kicheko)*

**SPIKA:** Tunaendelea na swali linafuata, Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha!

Na. 199

**Fedha kwa Ajili ya Kuendesha Mabaraza ya Ardhi**

**MHE. IGNAS A. MALOCHA** aliuliza:-

Kutokana na Mabaraza ya Ardhi ya Kata na Wilaya kutokuwa na fedha za kutosha kuendesha shughuli zao, Mabaraza hayo hulazimika kuwatoza fedha Wananchi walioshitakiwa kutokana na migogoro ya ardhi ili waweze kufika eneo la mgogoro:-

Je, ni lini Serikali itayapatia Mabaraza hayo fedha za kutosha ili waachane na utaratibu wa kuwatoza fedha Wananchi hao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mabaraza ya Ardhi ya Kata yanaundwa chini ya Sheria inayounda Mahakama za Kutatua Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216, Toleo la Mwaka 2002 na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya, yanaundwa na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, chini ya Kifungu cha 22 cha Sheria Namba 2 ya Mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 27 cha Sheria inayounda Mabaraza hayo, kinaeleza kwamba, Wajumbe wa Baraza la Ardhi la Kata, wanatakiwa kulipwa posho kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa na Halmashauri husika kwa kushirikiana na Kamati ya Maendeleo ya Kata, yaani *Ward Development Committee*. Fedha ambazo hutumika kuendesha Mabaraza ya Ardhi ya Kata kwenye Halmashauri hutokana na mapato ya ndani ya Halmashauri pamoja na fedha za ruzuku ya vyanzo zilivyofutwa, yaani *GPG*. Hivyo, fedha za uendeshaji zinazotolewa na Halmashauri kwenye Kata, ndizo zinazotakiwa kutumika pia kulipa posho za Wajumbe wa Mabaraza hayo.

Mheshimiwa Spika, Mabaraza ya Ardhi ya Nyumba ya Wilaya ambayo yako chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, hutengewa fedha kila mwaka kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa Mabaraza, ukarabati wa majengo na ununuzi wa samani. Kwa mantinki hiyo, Mabaraza ya Ardhi hayaruhusiwi kisheria kuchangisha au kutoza fedha kutoka kwa Wananchi walioshtakiwa kutokana na migogoro ya ardhi kwa ajili ya uendeshaji wa Mabaraza ya Kata na yale ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuzikumbusha Halmashauri zote, kuhakikisha kwamba, zinatenga na kupeleka fedha za uendeshaji katika Kata ili zitumike kuyawezesha Mabaraza hayo kutekeleza wajibu wake kikamilifu.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, kwa mchanganuo ambao ameutoa na hasa msisitizo wa pale chini kama utaenda kwa utekelezaji. Pamoja na majibu hayo ninayo maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa Mabaraza ya Ardhi na Wilaya yako Makao Makuu ya Wilaya, kiasi kwamba yanagharimu Wananchi kutumia fedha nyingi katika kuyafikia. Je, kwa nini Serikali isitumie Mahakama za Mwanzo katika kutatua migogoro ya ardhi?

(ii) Serikali ina mpango gani wa kuwalipa mishahara Makarani wa Mabaraza ya Kata, wamekuwa wakijitolea kwa muda mrefu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ignas Malocha, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, juzi hapa utakumbuka Mheshimiwa Felix Mkosamali alikuja na hoja inayofanana kabisa na ya Mheshimiwa Malocha na *I think* ilitokana na Mheshimiwa Malocha huyo huyo. Akifikiri kwamba, labda kunaweza kukawa na uwezekano wa kuondoa haya Mabaraza. Mabaraza haya hayahusiki na ardhi tu, yanahusika pia na matatizo mengine, mirathi na vitu vingine. Yakaletwa mawazo kwamba, yapelekwe kule na siku ile mimi nika-*react* hapa kwa naiba ya Serikali kueleza kwamba ni kwa nini bado tunakuwa wazito kulikubali jambo hili kwamba waende kule. Wakati Mabaraza haya ya Kata yanaundwa, moja ya sababu zilizosababisha yaundwe ilikuwa ni msongamano ambao ulikuwa unatokea katika hizi *Primary Court* anazozizungumza hapa.

Hiyo ndiyo ilikuwa sababu ya kwanza, kwa sababu vikesi vyenyewe vile vingine vya kuku, mwingine sijui kamsukuma mwezake, mwingine kamng'ong'a mwenzake. Vikawa vikesi vile viko vingi vingi. Kazi yake pale kubwa ni kufanya maridhiano tu, kuleta amani na utulivu katika lile eneo na ndiyo maana watu wanaotakiwa pale siyo watu wenye madigrii, wala siyo Diwani, wala si Mbunge, watu wa kawaida tu wenye uelewa wa kawaida wanakaa pale wanachaguana wanakwenda pale wanaridhiana, wanafanya kitu kinachofanana kama wale watu wa Gachacha kule Uwanda, ambao mtu amemuua mama yako au nini, mnakaa mnazungumza mnaelewana mnakubaliana unasema nimekusamehe. Hakuna *fine*, hakuna chochote, kule kwetu Uchagani wanaweza wakakwambia basi lete hapa vikombe viwili vya mbege tunywe hapa mshike mwenzako mkumbatie ondoka.

Mheshimiwa Spika, *Institution* hiyo, kwa maoni yetu sisi, tunafikiri inatakiwa ifanyiwe kazi, *much as* Serikali ina-*appreciate* kwamba, uko upungufu huu anaouzungumza Mheshimiwa Malocha. Tumerudisha *general purpose grand,* mwaka jana ilikuwa bilioni 63, mwaka huu 67 bilioni. Tumeziambia Halmashauri na sasa hivi tutapeleka *circular* na mimi nataka nikuthibitishie tutasimamia jambo hili, nimewaita watu wangu kwa sababu nilijua hili jambo litazuka hapa.

Moja ya hela hizi zinazokwenda za *General Purpose Grand* tunataka zitengwe kwa ajili ya kuendesha haya Mabaraza. Tunataka liwe *ring-fenced*, siyo wanazi-*dump* humo, anamwambia hizo na akina mama humo humo na za madarasa humo humo; *no* tunataka zitengwe kabisa zifahamike.

Mheshimiwa Spika, naomba waniamini wenzetu hapa, hii sauti ni msisitizo tu mama yangu hapa, wala siyo kwamba ninafoka, lakini tutalichukua hili jambo kwa uzito mkubwa, ili tuhakikishe kwamba linakamilika. *(Kicheko)*

Pili, sasa kwa maana hiyo, hata hii mishahara anayozungumza ya Makarani, hata hizo posho zote, zitakuwa ni sehemu ya utaratibu huu. Tutakwenda kufanya hivyo na mtuombee kabisa tukasimamie jambo hili. Tukija hapa tusiwe tunaogopa ogopa hivi na nini na kama kutakuwa kuna mtu anayejua kwamba kuna Mtendaji wa Kata au Halmashauri haifanyi hiyvo, watuambie sisi. Hapa tuna watu wana *Ph.D* wanazunguka mtaani huko wanatafuta kazi, tutawaambia tutawafyekelea mbali, tunaweka watu ambao wanaweza wakafuata maelekezo haya yanayotolewa hapa.

**SPIKA:** Uamuzi wa siku ile ilikuwa Serikali mmesema mtakwenda kuliangalia, ndiyo maamuzi yaliyotolewa hapa. Kwa hiyo, sasa hiyo, mnaendelea na utaratibu lakini mlisema mtakwenda kuliangalia, ndiyo tulipita pale kwa msingi huo. Kwa hiyo, hiyo ahadi bado inaendelea. *(Makofi)*

Nataka tuendelee na swali lingine, kwa sababu huyu kasema kwa msisitizo mpaka akanimalizia na muda. Mheshimiwa Al-Shaymaa John Kwegyir! *(Kicheko)*

Na. 200

**Maafisa Elimu Maalum Nchini**

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR** aliuliza:-

(a) Je, Serikali inaweza kueleza mpaka sasa ina Maafisa Elimu Maalum wangapi kwa Halmashauri zote nchini?

(b) Je, wana viwango gani vya elimu kulingana na taaluma wanazozisimamia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, leo uko mwenyewe tu!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Al-Shaymaa J. Kwegyir, siku ile nilisikia anakwambia jinsi ya kutamka jina lake; kama nimekosea naomba anisamehe, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, elimu maalum inayotolewa katika mfumo wa elimu nchini inakusudia kufikia malengo ya Serikali kwa kutoa elimu bora kwa wote na kwa usawa. Hivi sasa kuna Maafisa wa Elimu 134 katika Halmashauri mbalimbali nchini wanaoshughulikia kusimamia na kuratibu shughuli za utoaji elimu maalum.

(b) Mheshimiwa Spika, viwango vya Maafisa Elimu Maalum waliopo, ni kuanzia cheti wako saba, stashahada wako 51, hadi shahada ya kwanza ya elimu maalum wako 76 kutoka vyuo vikuu na Chuo cha Elimu Maalum Patandi kinachotoa Elimu ya Cheti na Stashahada. Serikali itaendelea kuwapanga Maafisa Elimu Maalum katika Halmashauri mbalimbali kulingana na mahitaji, wanavyohitimu na sifa walizonazo.

**MHE. AL-SHYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa majibu, ambayo ni mafupi sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwanza kabisa, napenda kumwambia idadi hiyo ni ndogo ya hao Maafisa Elimu Maalum, ukizingatia Hamashauri, nafikiri yeye Mheshimiwa Naibu Waziri ataniambia Halmashauri ziko ngapi, ni wachache. Sasa basi, kumekuwa na malalamiko kwamba, Walimu wa Elimu Maalum pindi wanapotoka vyuoni, hawapelekwi kwenye zile shule husika za elimu maalum kama waliyosomea, wanapelekwa kwenye shule za kawaida.

Hilo lalamiko lipo na juzi tulikuwa Bwigiri na Mheshimiwa Waziri Mkuu, walimu wamelalamikia hilo. Tatizo kubwa la walimu, wanatoka kwenye vyuo, wanapelekwa kwenye shule ambazo sizo. Sasa Mheshimiwa Waziri aniambie, tatizo ni nini?

(ii) Hivi sasa kuna tangazo la udahili wa walimu katika vyuo na shule mbalimbali. Je, Serikali itazingatiaje udahili wa walimu wa elimu maalum kwenda kwenye shule za elimu maalum? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nimshukuru na kumpongeza Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Mwanri, kwa majibu mazuri kabisa katika swali la msingi la Mheshimiwa Al-Shaymaa.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imeshatoa tangazo la udahili wa walimu katika vyuo mbalimbali nchini. Ili kuzingatia suala zima la utoaji wa elimu na upatikanaji wa Maafisa Elimu Maalum nchini, Wizara ya Elimu na Mafuzo ya Ufundi, imekiteua na kuendelea kukitumia Chuo cha Ualimu Patandi kuhakikisha kinatoa Elimu Maalum kwa walimu wa ngazi ya cheti na kwa walimu wa ngazi ya stashahada, kukidhi mahitaji ya Walimu wa Elimu Maalum katika nchi yetu ya Tanzania.

Swali la Mheshimiwa Al-Shaymaa ni la msingi kabisa, sifa za waombaji zimeainishwa vizuri katika tangazo letu. Ninawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, ninawaomba Watanzania wote, wawasiliane na Ofisi zetu za Elimu Mkoa na katika Halmshauri zetu, zitatoa maelekezo mahususi na tunawaomba walimu watumie maelekezo hayo na waende wakasomee elimu hizo maalum ili kutusaidia sana kupunguza tatizo la Walimu wa Elimu Maalum na Maafisa Elimu Maalum katika nchi yetu ya Tanzania.

Serikali itaendelea kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge na walimu wetu wote ili kuhakikisha eneo hilo pia linazingatiwa ipasavyo katika kuhakikisha watoto wote wa Tanzania wanapatiwa elimu wakiwemo watoto hawa wenye mahitaji maalum. *(Makofi)*

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa walimu wengi hujiendeleza sana kielimu, lakini cha kushangaza, wanapokuwa wamemaliza masomo haya, mishahara yao huwa hairekeibishwi. Ninaomba Mheshimiwa Naibu Waziri atuambie, hivi Serikali inategemea kupata nini kutoka kwa walimu hawa ambao wamejiendeleza kielimu, lakini mishahara yao hairekebishwi?

**SPIKA:** Pamoja na Walimu wa Shule Maalum. Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, kuhusu hizi takwimu za Halmashauri kwamba ziko ngapi, Halmashauri ziko 168 na Wilaya ziko 133, kwa sababu tuliulizwa ziko ngapi.

Hawa walimu ambao anawazungumzia Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa kwamba, mtu amekwenda kujisomea; hii ni *obvious* kabisa, yaani mimi natoka hapa nakwenda kusoma *degree*, nilikuwa na *diploma*. Sasa nakuja marupurupu yangu yanabakia vilevile, *definitely, obviously*, kuna haja ya kuangalia upya kwamba, hivi unafanyaje ili uweze kuiona hiyo kwamba inakwenda kwendaje.

Najua kwamba kuna utaratibu wa kwetu ambao tunakwenda nao, najua mwalimu mmoja, walimu wawili, watatu, lakini nadhani *the Member of Parliament* anazungumza jambo ambalo la msingi sana. Haiwezekani mtu ana *masters* halafu amekwenda amepata *Ph.D*, hakuna kitu chochote. Kule nyuma nakumbuka tulikuwa tunakwenda, unaweza ukampa mishahara miwili ya nyongeza, unamwongezea mara mbili ya kile alichokuwa anapata. *No, I mean* unaweza ukaleta nyongeza moja, lakini yeye unampa mbili kwa sababu ya hicho alichokifanya.

Tutakwenda kuliangalia vizuri, tutashirikiana na wenzetu walioko Utumishi, tutazungumza na wenzetu walioko katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, wote kwa pamoja tuone jinsi ambavyo tunafanya na *practice* yake ikoje. *I promise* kwamba, tutawasiliana na Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa ili tuweze kupata jibu sahihi katika jambo hili.

**SPIKA:** Haya majibu mnayokwenda kuwasiliana na mtu aliyeuliza, mbona ametuulizia hapa wote. Ameuliza kwa wote, kwa hiyo, msiende kujadiliana na wenyewe, mlete *feedback* hapa. Mnakwenda kujadiliana peke yenu wakati sisi tumewasikiliza! *(Kicheko)*

Tunaenda Wizara ya Kazi na Ajira; Mheshimiwa Leticia Nyerere, nimefurahi umerudi salama.

Na. 201

**Mafao ya Wazee**

**MHE. LETICIA M. NYERERE** aliuliza:-

Tarehe 1 Oktoba, 2010 Mheshimiwa Waziri Mkuu katika kilele cha Siku ya Wazee Duniani aliahidi Wazee kupewa mafao yao:-

Je, ni kwa nini mpango huo haujatekelezwa mpaka sasa?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Serikali inatambua umuhimu wa kuhakikisha watu wake wote, ikiwa ni pamoja na wazee wanapata kinga ya hifadhi ya jamii. Katika kutekeleza azma hii, mnamo mwaka 2003, Serikali ilipitisha rasmi Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii. Sera hiyo pamoja na mambo mengine,

inaelekeza kuanzishwa kwa programu za misaada ya jamii inayojumuisha pensheni ya jamii kwa wazee.

Mheshimiwa Spika, tamko la Mheshimiwa Waziri Mkuu alilolitoa tarehe 1 Oktoba 2010, wakati wa kuadhimisha siku ya kilele cha Siku ya Wazee Duniani, ilitoa mwongozo wa kushughulikia suala la pensheni kwa wazee, kwa kuagiza mamlaka zinazohusika, kuchukua hatua stahiki. Baada ya hapo, Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii *(NSSRA),* ambayo ndiyo kwanza ilikuwa imeanzishwa, ilipewa jukumu la kushughulikia suala hili. Hata hivyo, mpango wa pensheni kwa wazee haujaanza kutekelezwa kutokana na kutokamilika kwa maandalizi. Hadi sasa kazi zifuatazo zimefanyika:-

Kwanza, Rasimu ya awali ya mpango wa pensheni kwa wazee imeandaliwa. Pili, ziara za mafunzo zimefanyika katika nchi za Kenya, Uganda, Mauritius, India, Thailand, Singapore, China na Indonesia. Lengo la ziara hizo zilizohusisha pia Waheshimiwa Wabunge, lilikuwa ni kujifunza na kupata uzoefu wa nchi zingine, katika kuendesha mipango ya pensheni kwa wazee.

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo maandalizi hayajakamilika ni pamoja na kubaini vyanzo endelevu vya mapato, vitakavyotumika kugharimia mpango huu, kuunda chombo kitakachosimamia pensheni, kupata maoni kuhusu mpango unaopendekezwa kutoka wa wadau na taasisi zinazohusika na kuwasilisha mpango huo katika vyombo vya maamuzi.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa mkweli kwamba, tamko la Mheshimiwa Waziri Mkuu limeshindwa kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, suala la kuwaangalia wazee wa taifa letu ni la msingi na siyo la ku-*negotiate*, ni la lazima, kama unapomtunza mtoto mdogo, huna uchaguzi au uamuzi ni lazima ufanye hivyo. Tuna wazee wetu ambao walikuwa wakulima, sasa hivi wameshindwa kulima kwa sabab:-

(i) Ili tusionekane katika macho ya Dunia kwamba sisi tunanyanyasa wazee wetu. Je, Serikali sasa iko tayari ku-*subsidies* matumizi ya wazee wetu ukianzia chakula, malazi, matibabu na kadhalika?

(ii) Tumezungumzia wastaafu ambao wamechangia mifuko yao ya kustaafu, lakini kuna wazee ambao hawakufanya kazi Serikalini; hivyo, hawajawahi kupewa pensheni, hawajawahi kutoa mchango kwenye pensheni zao; sasa hawa wazee tunawaweka wapi? Je, Serikali sasa iko tayari kuleta Wizara Maalum kwa ajili ya wazee wetu wote nchini ili matatizo yao yote yafuatiliwe, yashughulikiwe, yakiwemo matibababu na kadhalika?

**SPIKA:** Maswali mengi lakini jibu mawili tu.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba, agizo la Waziri Mkuu limepuuzwa. Ukweli ni kwamba, hata haya ninayoyaeleza ni utekelezaji wa maagizo ya Waziri Mkuu, aliyoyatoa kwamba, tuangalie sisi wahusika, ni namna gani pensheni hii ya wawee wote, yaani *universal pension*, inalipwa na akatoa ahadi hiyo. Sisi tumeanza hii kazi ya maandalizi na hayo niliyoyataja, kwa mujibu wa maagizo hayo.

Amekuwa akitufuatilia na sisi katika kumpa *brief,* amekuja kusisitiza kwamba, endeleeni, lakini angalieni *affordability* na *sustainability* ya mpango huu. Maana yake ni nini? Lazima taungalie kwamba je, Serikali ina uwezo na uwezo wenyewe uwe endelevu.

Mheshimiwa Spika, labda niseme tu kwamba, kama unavyojua mimi huwa najibu maswali kwa ufupi, lakini leo, tofauti na rafiki yangu Mheshimiwa Mwanri, lakini niruhusu kidogo nielezee hili. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kama sensa ya mwaka 2012, wazee hawa tunaowazungumzia, kati ya kuanzia miaka 60, walikuwa milioni mbili na nusu na ninyi mmeona. Ukisema uwape 20,000/= kila mwezi, kila mmoja, unahitaji bajeti ya bilioni 600 kwa mwaka. Sasa bilioni 600 ni bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, ambayo tumelilia kwamba ni ndogo na ukichukua Wizara ndogo ndogo kama Kazi na Ajira, yenye bilioni 20 kwa mwaka, unataka Wizara kama hizi 30 kama Wizara ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kazi tumeomba bilioni 36 kwa ajili ya mpango wa ajira kwa vijana, tumepata tatu na ninyi ni mashahidi hapa. Hata ukisema hiyo kuu 20,000/=, tupunguze tuwape 15,000/=, bado unahitaji bilioni 450 kwa mwaka na 10,000/= ambayo ndiyo kidogo kabisa, unataja bilioni 300.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni mambo ambayo lazima tukae, tuone wadau na hasa kwa mfano, Tume ya Mipango, ambao wanapanga mipango na Wizara ya Fedha wanaokusanya, tuna uwezo huo? Kwa sababu siyo jambo la kusema labda ni mkopo unakopa, halafu itakuwa *revolving* kwamba, watarudisha, kila mwaka lazima utenge kiasi hicho.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, yote haya tunayangalia, tunakuja kuangalia na *options*, kama hatuwezi, je, inawezekana kwa ajili tu ya kulipa hawa wazee, miaka ile tuongeze, badala ya miaka 60 tuanzie miaka 65 au 70, lakini itapungua kidogo tu. Tuangalie kwamba, je, hivi hawa wazee tunaowalipa, kwa nini tusiondoe wale ambao labda wana watu wanaowategemea, wanao uwezo. Kwa mfano, *universal pension* kwa wazee, hata baba yake Mahanga, ambaye ni Waziri, anatakiwa alipwe. Kwa nini hawa tusiwaondoe ambao tunaweza kuthibitisha kwamba wana watu wanaowategemea.

*Options* ziko nyingi, au taunze *pilot project,* tuanze na Wilaya fulani, kidogo tunakwenda, lakini unaangalia nayo itakuwa na matatizo; kwa nini uanze kule Karagwe kwa rafiki yangu Blandes na uache Tandahimba kwa Mheshimiwa Njwayo! Kwa hiyo, kuna haya yote ya kuangalia.

Mheshimiwa Spika, suala hili, niseme tu kwamba, hili la wazee, tunalozungumzia ni pensheni ya kila mwezi ambayo ni *cash* unaitoa tu kwao, lakini mambo mengine kama matibabu na kuwahudumia, yale yako kwenye sera na yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, hili la kuanzisha Wizara kwa wazee peke yake, mimi sioni kama ni lazima hata kidogo. Wale Wabunge tuliokwenda nao kwenye hizi ziara, watathibitisha kwamba, nchi zote nilizozitaja, ni Mauritius tu ambayo ambayo tumekuta wanatoa pensheni kama hii na wale wana watu 170,000 ambao ndiyo wazee wanaostahili, sisi milioni mbili na nusu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, tutatafuta semina kubwa kuliko haya maneno ya Waziri hapa. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Koka!

Na. 202

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi Kibaha**

**MHE. SILVESTRY F. KOKA** aliuliza:-

Kituo cha Polisi cha Kibaha Mjini kipo kwenye majengo ya Shirika la Elimu la Kibaha na ni dogo wala halikidhi mahitaji ya huduma hiyo kwa Wananchi wa Mji wa Kibaha:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kituo kingine chenye hadhi ya Mji wa Kibaha kwa ajili ya kutoa huduma bora ya usalama wa Wananchi wa maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Silvestry F. Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Halmashauri ya Mji wa Kibaha inatumia Jengo la Shirika la Elimu Kibaha kama Kituo cha Polisi cha Wilaya, ambalo halina hadhi ya kuwa Kituo cha Polisi. Kibaha ni miongoni mwa Wilaya 65 nchini ambazo hazijajengewa Vituo vya Polisi vya Wilaya na hii inatokana na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, ujenzi wa kituo hicho, pamoja na vituo vingine vya polisi maeneo mengine nchini, utaendelea kutekelezwa kwa awamu kadiri Serikali itakavyokuwa ikipata fedha.

Naomba Waheshimiwa Wabunge wote, pamoja na wadau wengine welevu, kushirikiana na Jeshi la Polisi chini ya mpango wake wa maboresho, kutimiza azma hii kwa kujenga Vituo vya Polisi kwenye maeneo yao.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mafupi ya Mheshimiwa Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Jengo hili liko ndani ya eneo la Shirika la Elimu, kwa hiyo, hata utaratibu wowote ule wa maboresho, siyo rahisi kwa sababu lile eneo siyo mali ya Serikali, kwa maana ya Wizara, bali ni mali ya Shirika na wenyewe hawako tayari kuona maboresho yoyote yanafanyika pale.

Jambo kubwa la kusikitisha ni kwamba, katika kituo hiki finyu, hata mahabusu ni moja na hata walivyotembelea Tume ya Haki za Binadamu, tarehe 9 Mei, ilikuwa ni jambo kubwa la kusikitisha kwamba, hakuna mahabusu kwa ajili ya jinsia zote mbili, bali iko moja.

Mheshimiwa Spika, hakuna hata ofisi ya wapelelezi, wao wanafanya kazi nje kabisa juani, pamoja na thamani na vitendea kazi vingine viko duni sana.

(i) Serikali ina mpango gani wa dharura, angalau wa kuhakikisha eneo jipya kwa ajili ya Kituo cha Polisi cha Wilaya linapatikana? Vilevile kuondoa haya matatizo makubwa angalau kwa dharura wakati mpango wa Serikali wa kuendelea kujenga kituo unaendelea?

(ii) Kumekuwa na kero kubwa sana kwa askari polisi na wamekuwa wakijiona kama wao wametengwa au kuna *double standard* katika kuwapa haki zao, hususan wanapopata matatizo mbalimbali ya kesi kama vile wizi na vitu vingine. Inapokuja katika suala la askari polisi, wanapohisiwa kupatikana na makosa, hufukuzwa jeshi na kesi inapopelekwa mahakamani, wanapoonekana hawana hatia, huwa hawarudishwi katika nafasi zao za kazi, wakati majeshi

mengine kama Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania huwa wanarudishwa kazini. Jambo hili linawafanya askari polisi kuona kama vile kuna *double standard* katika kutoa haki kwa askari hawa.

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba, askari polisi anapokutwa hana hatia kwa tuhuma yoyote aliyopewa anapata haki ya kurudishwa kazini kama raia mwema? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Koka, kama ifuatavyo:-

La kwanza, kuhusu ufinyu wa Kituo cha Polisi na kwamba, kiko kwenye maeneo ambayo hakiwezi kikarekebishika. Ninachoelewa mimi ni kwamba, Halmashauri ya Mji wa Kibaha, imeshatenga eneo kwa ajili ya Kituo cha Polisi cha Kibaha. Kwa hiyo, eneo siyo tatizo. Mimi namshauri Mheshimiwa Mbunge, tukae kitako tuone kwa pamoja vipi tunaweza tukakiendeleza kiwanja hicho tukiwa pamoja na Wananchi wa eneo lile.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Serikali inapata taabu sana kuona tunafanya kazi katika maeneo kama haya, lakini ujenzi nao kupitia Serikali moja kwa moja umepata matatizo, hasa wakati wa kufanya bajeti, ambayo kama mwaka wa jana na mwaka huu tunaambiwa tusianzishe majengo mapya tukamilishe yaliyokuwepo. Kwa hiyo, tukianza kukamilisha maana yake Kibaha inatoka moja kwa moja. Tuendelee kujadiliana tuone tufanye nini ili kuondoa tatizo hili.

Swali la pili kuhusu kesi za askari polisi; ni kweli kwamba, mara tu polisi anapotuhumiwa, kwa taratibu za kiaskari, ili apelekwe mahakamani, tunahisi kwamba ameshakiuka maadili ya kiaskari na pengine hahitajiki kuwepo kazini ili ashitakiwe, isipokuwa atolewe kwenye ajira ndipo aende kwenye mahakama. Ni kweli pengine haki haitendeki vizuri, lakini hili ni suala ambalo tunaweza tukatazama ili kama kuna uonevu wowote basi tuliweke sawa, wale ambao mahakama itawaachia huru waweze kurudishwa kazini. Wakati huo huo kuna ukakasi fulani wa askari kuhusika na mambo haya hata kama ataachiwa wakati ule.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Jeshi la Polisi limechukua jukumu la kuanzisha Dawati la Kijinsia, lakini ni kweli kwamba, miundombinu ya shughuli hiyo hairidhishi kwa nchi nzima. Je, Serikali ina mpango gani wa dharura na wa muda mrefu wa kuhakikisha Vituo vyote vya Polisi vinakuwa na miundombinu kwa ajili ya kazi hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba mjibu kwa kifupi, nilimruhusu mmoja tu kujibu kwa kirefu lakini wengine wote jibuni kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Waziri Kivuli Mstaafu wa Wizara hii, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uamuzi ni kwamba, kila mahala ambapo kuna Wananchi na kuna Kituo cha Polisi, kuwe na Dawati la Jinsia ili kuhudumia watoto na akina mama wakati wa matatizo. Tumeanza kujenga sehemu hizi taratibu na tunaendelea kupanua kwa kadiri fedha zinavyopatikana. Tuna mazungumzo na Shirika la Umoja wa Mataifa la *UNICEF* kutusaidia katika mambo haya na pia kuna Serikali nyingine za nchi za nje ambazo zinashirikiana nasi katika kuhakikisha kwamba, Madawati yanaenea. Tatizo tu hapa ni kwamba, kuna baadhi ya vituo kama hiki nilichozungumzia cha Kibaha, hata askari wanakaa nje, kwa hiyo, hivyo vitachelewa; kwanza, wakae askari halafu na Dawati litafuata.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Suala la Kibaha linafanana sana na suala la Jimbo la Konde na bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri ulifanya ziara, uliitikia wito wangu wa kuja Konde kuona hali halisi ya mazingira wanayoishi askari wale, ingawa mrejesho sijapata. Mheshimiwa Naibu Waziri, umekuwa ukitoa wito mara nyingi jamii ishirikiane na Serikali kuimarisha makazi ya polisi. Ninapenda ujue kwamba, mimi Naibu Waziri Kivuli, ninatoa shilingi milioni kumi hapa kusaidia wito wako, je, wewe Waziri halisi utatoa ngapi na Wizara yako?

**SPIKA:** Hii hapa inaitwa ahadi, hiyo ni ahadi, Mheshimiwa na wewe haya. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nimpongeze ndugu yangu, kwa kutoa shilingi milioni kumi na ninaomba *cheque* ije mapema. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, nimekwenda Konde na nimeona tatizo kubwa sana la makazi pamoja na hata Vituo vya Polisi pale, vimechakaa na vinahitaji huduma. Mimi ninachoahidi kwa Konde, ni kwamba, bajeti ijayo nitachangia kitakachowezekana. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Afadhali, tunaendelea jamani hata kama mnapenda kuendelea, lakini tuendelee na Wizara ya Nishati na Madini. Mheshimiwa Suleiman Nchambi, atauliza swali hilo, kwa niaba Mheshimiwa Ndassa.

Na. 203

**Kuhusu Kusambaza Umeme Vijiji vya Jimbo la Kishapu**

**MHE. RICHARD M. NDASSA (K.n.y. MHE. SULEIMAN N. SULEIMAN)** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kuhusu kusambaza umeme katika Vijiji 122 vya Jimbo la Kishapu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Nchambi Suleiman, kama ifuatavyo:-

Serikali itawezesha usambazaji wa umeme kwenye Vijiji vya Jimbo la Kishapu, kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha za utekelezaji. Katika vijiji hivyo 122, ni vijiji 19 tu vya Rubaga, Iboja, Mwakipoya Mwanuru, Mangu, Chagihiru, Toleleji, Toleleji Mission, Kimagi, Mwadoma, Mwamasala, Mwataga, Nyasamba, Buganika, Mwigumbi, Mipa, Bubiki, Seke na Mwamishon, vilivyobahatika kuwekwa kwenye Mpango Kabambe wa Umeme Awamu ya Pili. Mkandarasi atakayetekeleza Mradi huu ni *LTL Project PVT.*

Mheshimiwa Spika, vijiji vyote ambavyo Mheshimiwa Mbunge alihitaji viwekewe umeme vimeshapimwa na gharama zinatayarishwa ili zipelekwe kwa Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)*, kwa ajili ya kuomba vitengewe fedha kwa awamu ijayo ya Mpango Kabambe wa Umeme Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kupeleka umeme kwenye vijiji hivyo 19 itajumuisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa *kilovolt* 33, yenye urefu wa kilometa 98.9. Ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa *kilovolt* 0.4 yenye urefu wa kilometa 37, ufungaji wa transfoma 19 na kuwaunganishia umeme wateja wa awali wapatao 963. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2015 na utagharimu shilingi bilioni 4.23.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nimwulize Bwana Waziri. Bwana Waziri, kwa sababu Wizara ya Nishati na Madini inajinasibu kwamba, hii Wizara siyo Wizara ya maneno, lakini mara kwa mara mkijibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge, hasa kuhusu hizi *Project* za *REA;* mmekuwa mkitamka kwamba, kazi zitakamilika Juni, 2015. Mkandarasi huyu mpaka sasa hivi hayuko *site*. Vivyo hivyo *CHEKO* naye hayuko *site,* lakini mkisimama hapa mnasema watamaliza Juni, 2015 wakati hata kazi yenyewe haijaanza.

(i) Je, maswali hayo ni ya kweli?

(ii) Ni lini wakandarasi hawa sasa Serikali itawahimiza waende *site?*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Ndassa, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa utekelezaji utakamilika kama ilivyopangwa mwaka 2015 mwezi Juni; na kwamba, wakandarasi hawako *site*. Nipende tu kusema kwamba, wanachofanya wanakwenda *site* mara ya kwanza wanafanya *survey*, wanachora michoro na wakishamaliza kuchora michoro wanaangalia ni vifaa aina gani ambavyo vinatakiwa kuagizwa na kuwekwa pale. Kwa sasa hivi wakandarasi wengi wameshaenda *site* na kumaliza *survey*, sasa wanachofanya ni kuagiza vifaa. Sasa wakati vifaa havijafika, hawawezi kuwa pale kwa sababu itakuwa ni gharama. Vifaa vitakapofika wakandarasi watakuwa *site* na nimhakikishie Mheshimiwa Ndassa, wakandarasi wote watakuwa *site* hivi karibuni.

**SPIKA:** Naomba tuendelee tu, tumemaliza juzi Wizara hiyo wakaambia wote mtapata umeme vijijini. Mheshimiwa Christina Lissu, swali linalofuata.

Na. 204

**Mradi wa Umeme wa Upepo Singida**

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI** aliuliza:-

Katika jitihada za kutatua tatizo la umeme nchini Serikali ilianzisha Mradi wa Umeme wa Upepo Singida *(Singida Geo Wind)* kwa ushirikiano na *NDC* na *TANESCO:-*

(a) Je, utekelezaji wa Mradi huo umefikia wapi?

(b) Je, ni lini Mradi huo utakamilika?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA)** alijibu:-

Kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Nguvu ya Upepo Mkoani Singida, unatekelezwa na Kampuni ya *Geo Wind Power Tanzania Ltd.* ambayo ni ya Ubia kati ya

Shirika la Maendeleo Tanzania linalomiliki hisa za asilimia sitini, Shirika la Usambazaji Umeme Tanzania *(TANESCO)* linalomiliki hisa asilimia ishirini na Kampuni ya *Power Pool East Africa* inayomiliki hisa kwa asilimia ishirini.

Mheshimiwa Spika, Mradi uko takribani kilometa 12 Mashariki ya Manispaa ya Singida katika Vijiji vya Mugano, Ushankanya na Kisasida. Katika awamu ya kwanza, Mradi unatarajiwa kuanza kufua umeme wa *megawatt* 50 na baadaye Mradi huu utapanuliwa hadi kufikia *megawatt* 300. Umeme utakaofuliwa utaunganishwa katika Gridi ya Taifa kupitia Kituo Kikuu cha Umeme kilichoko Mjini Singida.

Mheshimiwa Spika, gharama za uwekaji wa Mradi huu awamu ya kwanza wa uzalishaji wa *megawatt* 50 na ujenzi wa miundombinu ya kukidhi *megawatt* 160, unakadiriwa kuwa Dola za Marekani milioni 186. *NDC* ikishirikiana na Wizara ya Fedha, inafanya utaratibu wa kupata mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Exim ya China.

Mheshimiwa Spika, Mradi huo umeshafanyiwa maandalizi ya kutosha, ikiwa ni pamoja na upembuzi yakinfu na uhakiki wa ufadhili pamoja na uwezo wa ujenzi wa mitambo. Serikali kupitia Shirika la *NDC*, imeshughulikia vibali vyote vinavyohitajika ili Mradi utekelezwe, ikiwa ni pamoja na hati miliki ya eneo la Mradi, Mkataba wa Ununuzi wa Umeme, Cheti cha Mazingira na Hati ya Vivutio vya Uwekezaji.

Mradi huu ni miongoni mwa Miradi yenye kipaumbele chini ya Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa *(Big Results Now)* na utatarajiwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Christina, swali la nyongeza.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, ambayo hayajaniridhisha, nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Tunayo taarifa kupitia Kamati kwamba, hadi sasa Serikali haijasaini mkataba na wawekezaji ili umeme huo wa upepo uweze kuzalishwa. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuuleta mkataba huo hapa Bungeni ili tujiridhishe ni nani anayechelewesha Mradi huo?

(ii) Kwa kuwa Serikali inatumia fedha nyingi sana kununua mafuta mazito kwa ajili ya kuzalisha umeme, takribani shilingi bilioni 1.1 kila siku; Serikali haioni kwa kuendelea kutumia fedha hizo nyingi sana na kuendelea kuchelewesha Mradi wa Umeme wa Upepo ambao ni wa rahisi sana kunawatwisha Watanzania mzigo, ambapo fedha hizo zingetumika kwa ajili ya huduma nyingine za jamii?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA):** Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Christina Lissu, maswali yake mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Kwanza, nimhakikishie tu kwamba, majibu yangu ya awali yanaridhisha. Nimhakikishie pia kwamba, mkataba uliopo, kuna taratibu ambazo Bunge linazo za kuweka mikataba kwa Katibu wa Bunge na kama itahitajika basi tutaiweka pale. Kuhusu mafuta mazito na kwamba inatumia pesa nyingi, labda nitoe ufafanuzi kwamba, Mradi huu wa Upepo ni kati ya Miradi ambayo umeme wake ni aghali sana. Kwa hiyo, asifikirie kwamba, Mradi wa Umeme ni rahisi. Kama nilivyoeleza hapo awali ni kwamba, umeme rahisi kabisa wa kwanza ni maji, unafuatia mkaa, unafuatia gesi, unafuatia mafuta, halafu unakuja *renewables,* ambazo ni pamoja na jua, ambayo *cost* yake ya mwanzo pamoja na upepo ni ghali sana. Kwa hiyo, inabidi … gharama za umeme kwa muda mrefu ili ziweze kuwa pungufu.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO (MHE. CHARLES M. KITWANGA):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Miradi hii ya Nishati ambayo iko *NDC,* ina urasimu mkubwa sana, kwa sababu *NDC* kiutendaji iko chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara inayoshughulika na nishati ni Nishati na Madini. Hivi Serikali haioni kwamba, sasa wakati umefika, kuiondoa hii Miradi ya Nishati iwe chini ya *STAMICO* ili kupunguza urasimu?

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kayombo, kama ifuatavyo:-

Wazo lake tutalichukua, lakini ikumbukwe kwamba, kila Shirika lina mipango yake, ikiwa ni pamoja na *NSSF;* pale ambapo inaona itawekeza na kuweza kupata faida, inafanya mipango na kuingia ubia na watu mbalimbali. Hata hivyo, wazo lake tumelichukua tuone ni kwa namna gani tunaweza tukalitekeleza.

**SPIKA:** Haya, twende Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Dkt. Gervas Mbassa, atauliza swali hilo.

**MHE. DKT. GERVAS A. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Awali ya yote, naomba nianze kwa kutoa pole kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo, kwa kuondokewa na mtumishi, Maria Kahesi na pia wanafamilia; naomba Mungu awape moyo wa ustahimilivu katika msiba huu mzito. Sasa naomba swali langu Namba 205 lipatiwe majibu.

Na. 205

**Upungufu wa Walimu Kwenye Vyuo vya *VETA***

**MHE. DKT. GERVAS A. MBASSA** aliuliza:-

Vyuo mbalimbali vya *VETA* vilivyoanzishwa ikiwemo na Chuo cha *VETA/FDC* Biharamulo vina upungufu wa walimu katika fani mbalimbali:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza walimu katika fani mbalimbali?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza mfumo wa Kikanda au wa Kimkoa wa kubadilishana walimu pale ambapo walimu hao hawapo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Gervas Anthony Mbasa, Mbunge wa Biharamulo, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeteua Vyuo 25 vya Maendeleo ya Wananchi *(FDC),* kutoa mafunzo ya ufundi stadi katika baadhi ya fani chini ya uratibu wa *VETA*. Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Rubondo kikiwa kimojawapo. Chuo hiki kimeteuliwa kutoa mafunzo ya ufundi stadi katika fani za ufundi magari na uashi, ambapo walimu wawili wamejengewa uwezo na *VETA* kufundisha fani hizo. Kwa mantiki hiyo, Chuo hiki kina walimu wanaokidhi mahitaji ya fani

tajwa zinazoendeshwa kwa makubaliano kati ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshiwa Spika, Mamlaka ya Elimu ya Mafunzo ya Ufundi Stadi ina jukumu la kuajiri Walimu wa vyuo vya *VETA,* kutegemeana na Mahitaji. Kutokana na utaratibu huo, vyuo vya *VETA* vina walimu wanaoidhi mahitaji ya fani ilizopo kwa kila chuo.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa hakuna mfumo wakubadilishana walimu kati ya *VETA* na *FDC* pale ambapo kuna upungufu wa walimu, kwa sababu walimu wa *VETA,* wana utaratibu tofauti wa ajira na walimu wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Aidha, mfumo huo unaweza kutumika tu, kwa walimu wanaoanaliwa kufudisha fani zinazoratibiwa na *VETA,* katika vyuo vya *FDC*.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Labda nianze na ombi maalum, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuandamana na mimi, kwenda jimboni kuangalia chuo hicho?

(a) Kwa kuwa leo saa 01.30 asubuhi, nimeongea na Mkuu wa Chuo hicho Bwana Josephat Kamugisha na akanieleza kuna upungufu mkubwa. Aidha au hana walimu wa fani ya uashi, ufundi magari, useremala, umeme na ni mafunzo ambayo ndiyo kimbilio kwa vijana ambao ndiyo tegemeo lao. Je, Wizara iko tayari kuniletea walimu hao?

(b) Kwa kuwa mfumo uliopendekezwa hapa ni wa walimu wale wa *VETA* ambao wana mafunzo maalum, walau kutengengeza programu ya kubadilishana kwenda kwenye vyuo vile ambavyo havina walimu hao, kwa ajili ya kufundisha.

Je, Wizara ina ridhia ombi hilo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Gervas Mbassa, yaliyotanguliwa na ombi maalum la kuandamana naye, kwennda katika Chuo hicho ili kuweza kuangalia hali halisi, ilivyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimkubalie Mheshimiwa Mbassa, niko tayari tutaandamana, aandae tu hiyo safari vizuri iwe na mafanikio, na tutakwenda kuangalia chuo hicho tukiwa pamoja sina tatizo na hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali (a) la Mheshimiwa Mbassa anataka kujua kama Wizara inaweza ikamsaidia kupata walimu katika fani nyingine. Wizara ya Elimu kwa mwaka huu, imejipanga kufanya udahili wa walimu katika fani za ufundi katika Chuo chetu cha Kleruu.

Mheshimiwa Spika, tumewaeleleza wale wote wanaohitaji kujiunga na ualimu wa fani hizo za ufundi, katika Chuo cha Kleruu, tuwapate wale ambao wana sifa za cheti *NTA level* ya *VI* na wakipatikana walimu hao, ninaamini kabisa kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, tunaweza kuajiri walimu ili kukidhi fani hiyo. Hilo linaendana sambamba na wale Walimu wa

Elimu Maalum, ambao wanasomea Elimu Maalum, lakini hawaendi kufundisha katika maeneo husika. Wizara na Serikali itaendelea kujitahidi kuhakikisha hali hiyo inasimamiwa na kuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, ombi lake la pili ni kwamba, pamoja na *VETA*, haina mahusiano na *FDC,* katika kubadilishana walimu, ameomba sana suala hilo liangaliwe upya katika Wizara yetu.

Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kama mpango huu wa kuendeleza fani katika vyuo vya *FDC* kupitia VETA, litaendelea kufanyiwa kazi na kuongeza fani nyingi zaidi katika vyuo hivyo, basi hata utaratibu wa upatikanaji wa walimu ili kukidhi maakwa ya ufudishaji litazingatiwa na tutaweza, kulizingatia kama vile Mheshimiwa Mbunge alivyosema.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa ni Sera ya Serikali ya kujenga vyuo vya *VETA,* kwa kila Mkoa, na Mkoa wa Kagera, peke yake katika Mikoa ya zamani ukiondoa Mikoa mipya, ndiyo Mkoa ambao hauna chuo cha *VETA* kwa hadhi ya Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitaka nijue je, Serikali ina mpango gani wa kujenga chuo cha *VETA* katika Mkoa wa Kagera?

**NAIBU WAZIRI ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza niwapongeze sana Wabunge wote wa Mkoa wa Kagera kwa juhudi zao na kuhakikisha kwamba Mkoa wa Kagera nao unapatiwa chuo cha *VETA* Mkoa ili kutoa elimu ya ufundi stadi katika Mfumo wa *VETA*.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu, tarehe 2 Juni, nilifanya ziara ya makusudi kabisa katika Mkoa wa Kagera, kwenda kukagua chuo cha *VETA* ambacho kiko katika Wilaya ya Bukoba, kuona kama kina sifa na kinastahili kupanda hadhi na kuwa Chuo cha Mkoa, ama kijengwe chuo kingine cha Mkoa.

Mjheshimiwa Spika, naomba kumuarifu Mheshimiwa Mbunge, nimetizama na kuchunguza hali halisi ya chuo kile katika Wilaya ya Bukoba, lakini vilevile tumekubalina na Mkuu wa Mkoa na viongozi wengine wa pale mkoani, kuona namna gani, ama tuanze kukipandisha chuo hicho ili watafute ardhi nyingine na kuendelea kutengeneza mipango ya kujenga chuo kipya.

Kwa hiyo maamuzi ambayo tutayafikia kupitia Serikali baada ya ziara yangu nitawaarifu Wabunge wote wa Mkoa wa Kagera na nitaomba ushirikiano sana ili tuweze kufanikisha azma yao ya kupatiwa elimu ya ufundi stadi kwa vijana wa Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hii saa inatakiwa tuiangalie wote, siyo mimi peke yangu. Kwa hiyo, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimwia Betty Machangu, atauliza swali linalofuata.

Na. 206

**Mbolea ya Ruzuku**

**MHE. BETTY E. MACHANGU** aliuliza:-

Mwongozo wa utaratibu wa utoaji pembejeo katika kilimo ni mlengwa kuwa na eka moja au zaidi; mkulima hupewa mfuko mmoja wa mbolea ya kupandia, mfuko mmoja wa mbolea ya kukuzia na mbegu ya eka moja na Serikali inachangia 50% hata kama mkulima ana zaidi ya eka moja.

Serikali imepania mpango huu kuongeza uzalishaji katika kilimo na mpango huu umedhihirisha kutokuwa na manufaa katika uzalishaji zaidi:-

Je, kwa nini Serikali isiweke ruzuku katika mbolea yote ili kuongeza uzalishaji na kuondoa rushwa katika uuzwaji wa mbolea?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Betty E. Machangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto za uzalishaji na tija katika kilimo, Serikali imekuwa ikitoa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa wakulima wa vocha kwa lengo la kujenga utamaduni wa matumizi endelevu wa pembejeo za kilimo miongoni mwa wakulima nchini ili kuwezesha uzalishaji wa chakula cha kutosha nchini

Mheshimiwa Spika, waraka wa utaratibu wa utoaji wa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa wakulima, umeweka vigezo mbalimbali vya wanufaika ikiwemo uwezo wa kuchangia gharama za pembejeo husika, kwa lengo la kuwajengea wakulima, uwezo na mazoea ya kujinunulia pembejeo wenyewe. Aidha, utaratibu huo umezingatia ukweli kuwa mpango wa kutoa ruzuku siyo endelevu na Serikali haina uwezo wa kibajeti wa kutoa ruzuku ya pembejeo kwa wakulima wote nchi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwapo na changamoto mbalimbali katika utoaji wa ruzuku ya pembejeo ikiwemo ufinyu wa bajeti na usimamizi hafifu wa utaratibu wa utoaji wa ruzuku katika ngazi ya Serikali za Mitaa, ambayo imechangia pembejeo za ruzuku kushindwa kuwafikia wakulima kwa wakati.

Kutokana na changamoto hizo Serikali imekuwa ikitekekeza mikakati mbalimbali ya kuongeza upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima ikiwemo mpango wa kutoa ruzuku kupitia vikundi vya wakulima kwa njia ya mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupita utaratibu wa utoaji wa ruzuku ya pembejeo kwa njia ya mikopo, vikundi vya wakulima nchini kupitia *SACOS* na *AMCOS* vitapata fursa ya kupata pembejeo wakati wote wa mwaka na hivyo kuongeza uzalishaji na tija ya mazao ya kilimo. Utaratibu huo ukitekelezwa na kusimamiwa vizuri, utapunguza ubadhilifu wa fedha za umma na kudhibiti vitendo vya rushwa. Aidha, utaratibu huu unategemewa kuwa suluhisho endelevu la mpango wa utoaji wa ruzuku ya pembejeo kwa wakulima nchini.

**MHE. BETTY E, MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa vikundi kukopa, yaani vikundi kulipa asilimia 20 na Serikali kulipa asilimia 80, umeleta matatizo makubwa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaweza kulieleza Bunge hili na wakulima tatizo lilikuwa ni nini na kuna mkakati gani kurekebisha mfumo huo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa imedhihirika kwamba mbolea ya Minjingu inafaa baadhi ya maeneo nchini Tanzania. Je, Serikali iko tayari sasa kutangaza yale maeneo ambayo yanafaa kutumia mbolea ya Minjingu kwa ajili ya kuondoa usumbufu kwa wakulima?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua matatizo yalikuwa ni nini kufuatia Serikali kutotekeleza ahadi yake ya kuvipatia vile vikundi udhamini wa asilimia 80 na vikundi kuchangia ile asilimia 20.

Mheshimiwa Spika, ni kweli ninaomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge ya kwamba Serikali ilivielekeza vikundi ambavyo viko tayari vichangie asilimia 20 na kwamba Serikali ingelitoa asilimia 80.

Lakini kuna matatizo ambayo kimsingi yalijitokeza ambayo yalisababisha jambo hilo lisiweze kufanikiwa. Moja, ni suala la benki kutaka walipwe kwanza pesa *in advance*, kwa maana ya kwamba, utangulize kwanza pesa halafu na sisi tutaweza kutoa mikopo. Kwa maana kama Serikali ingetoa asilimia 20, basi na benki zingetoa asilimia 20 kwa maana ya kufanya *leverage* ya pesa zenyewe.

Lakini tatizo ilikuwa ni kwamba Serikali haikuwa na uwezo kwa maana ya kuweza kuweka *deposit* kwenye benki, kwa hiyo vikundi hivyo havikuweza kupata mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini tukumbuke kwamba mwaka jana bado tulikuwa na utaratibu wa *voucher,* kwa hiyo maeneo mengi yaliweza kupata mbolea kwa utartibu wa *voucher.* Sasa mwaka huu hatuna utaratibu tena wa *voucher* zile ambazo tulilikuwa tumezoea, lakini tunakuja na utaratibu wa kupitia mbolea hii kwenye vikundi vya *SACCOS* na *AMCOS.*

Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imejipanga vizuri, kwamba tunazungumza na benki, nadhani tunaelekea kukubaliana, lakini pia tunazungumza na makampuni yenye ambayo yanatoa mbolea pamoja na mbegu ili yaweze kukopesha vikundi moja kwa moja.

Kwa hiyo Serikali inataka kulisimamia vizuri sana suala hili mwaka kuhakikisha kwamba yale yaliyojitokeza mwaka jana hayajitokezi tena.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mbolea ya Minjingu kwamba Wizara iwe tayari kuelekeza yale maeneo ambayo mbolea hii haifai, ili wananchi wajue.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, Wizara tutaelekeza maeneo hayo ambayo mbolea hiyo inafaa kutumika au ambayo haifai ili wananchi waweze kujua.

Lakini pia la msingi ni kwamba mwaka huu tunataka wananchi wenyewe wachague mbolea wanayotaka kuitumia. Kwa sababu tutakuwa tunatumia vikkundi, kwa hiyo hatutawaelekeza mkulima huyu atumie mbolea hii au ile, kwa hiyo ni mkulima mwenyewe atachagua mbolea ambayo anataka kuitumia.

**SPIKA:** Waheshimwia Wabunge, nilishasema tusome saa kwa pamoja, mnapenda tu kusimama. Muda umekwisha sana, nawaomba niwatambue baadhi ya wageni walioko katika ukumbi wetu. *(Kicheko)*

Kwanza kabisa, nina wageni 25 wa Mheshimiwa Naibu Spika, ambao ni *Miss Redds Higher Leaning Institution,* toka Vyuo Vikuu vyote Tanzania wakiongozwa na Ndugu Agnes Matthew – Muandaaji wa shindano hilo, pia ni Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Taifa na Mjumbe wa Baraza la UWT-Taifa kutoka Mara. Kwanza huyu Agnes mwenyewe yuko wapi? Ahaa huyo. Sasa naomba na wale wengine 25 wasimame walipo.

*Okay,* tulikuwa tunashanga watu waliopendeza wametoka wapi, kumbe ndiyo ninyi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna wageni wengine wa Mheshimiwa Naibu Spika, kutoka Dodoma, ambao ni Ndugu Teddy Chimagu na Ndugu Benjamin Chimagu. Hawa nao wasimame walipo. Ahaa, wako upande huu. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Stephen Wasira, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Mahusiano na Uratibu, ambao ni Wanafunzi 70 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotoka Wilaya ya Bunda.

Naomba wote msimame, wanafunzi 70 kutoka Bunda. Sasa mkimaliza ninyi wote, Bunda itakuwa mbele kabisa. Someni kwa bidii. *(Makofi)*

Halafu nina wageni wa Mheshimiwa Juma Nkamia, Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, ambao ni wanafunzi 35 na walimu watatu kutoka shule ya Sekondari Msakwalo, Kata ya Orada, Wilaya ya Chemba. Naomba hawa wote wasimamame na walimu wao kama wamepata nafasi ndani. Ahaa, wapo! Asanteni sana, someni kwa bidii. (*Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Josephine Chagulla, ambao ni wanafunzi 12 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Nadhani na wenyewe wanatoka kwake. Wasimame hao 12 wageni wa Mheshimiwa Chagulla. Ahsante. Lakini Wanafunzi wote wa *UDOM* tunawatakia masomo mema. *(Makofi)*

Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Albert Obama, ambao ni mtoto wake Alert Albert Obama na Waziri Magae, rafiki wa mtoto wake. Wako wapi watioto hawa? Nadhani wataingia baadaye.

Kuna wageni wa Mheshimwia Selemani Jafo kutoka Kisarawe nao ni Ndugu Abdallah Madeng'a, na Ndugu Msafiri Gunia. Wako wapi hawa? Aa, wako hapa. Karibuni sana.

Tuna wageni wa Bunge *Sports Club* ambao ni wanamicheo 18 na viongozi wao 4 kutoka Akiba *Commercial Bank,* wakiongozwa na Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Shughuli za Benki, Bi. Juliana Swai, na mwenyeji wao Meneja wa Akiba *Commercial Bank* Tawi la Dodoma, Ndugu Magigita. Wapo hapa bungeni kwa ziara ya mafunzo na kesho watakuwa na mchezo wa mpira wa miguu na Timu ya Bunge. Naomba ujumbe huu wote usimame. Karibuni sana. Karibuni sana. Nawatakia mchezo mwema hiyo kesho. *(Makofi)*

Halafu tuna wageni waliofika kwa ajili ya mafunzo. Tunao watumishi 23 kutoka Mamlaka mbalimbali za Serikali za Mitaa waliohudhuria mafunzo ya kujenga uwezo na kuboresha utendaji katika Chuo cha Serikali za Mitaa na Wahadhiri 10 kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Dodoma. Naomba hawa nao wasimame walipo. Na sisi Mbunge wetu mmoja amesomea huko huko. Karibuni sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

Tunao Umoja wa Wanafunzi 25 kutoka Mbeya wanaosoma Chuo Kikuu Cha *St. John's.* Hawa na wenyewe 25 wa St. John's wako wapi? Ahsante sana, someni kwa bidii.

Tunao pia wanafunzi wengine 65 kutoka Chuo cha Mipango – Dodoma, na wenyewe wasimame walipo. Ahsanteni sana. Tunashukuru sana, msome wote kwa bidii. *(Makofi)*

Matangazo ya kazi: Katibu Mkuu wa Chama cha Wabunge Kupambana na Rushwa (Katibu Mkuu wa *APNAC),* Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa. Anasema, naomba niwatangazie Wajumbe wa *APNAC* kuwa leo katika Ukumbi wa *African Deams,* kutakuwa na mkutano unaohusu masuala ya rushwa na utawala bora kuanzia saa saba mchana baada ya kuahirisha kikao cha Bunge cha asubuhi. Kwa hiyo kutakuwa na mkutano mkuu huko. Ratiba itaanza na chakula kwa Wajumbe wote. Wajumbe wote wa *APNAC* waanakarishwa. Kwa sababu watatoka tu hapa mara moja, basi muende huko *African Dreams* mkafanye mkutano huo.

Mwenyekiti wa Bunge *Sports Club,* Mheshimiwa Idd M. Azzan anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa kesho tarehe 7 saa 10.00 jioni kwenye Uwanja wa Jamhuri, kutakuwa na mchezo wa kirafiki wa mpira wa miguu kati ya Bunge *Sports Club* na Akiba *Commercial Bank,* hao wageni wetu nimeishawatambulisha. Aidha, tarehe 8 Juni, Bunge *Sports Club* watacheza na Waheshimiwa Madiwani wa Dodoma katika uwanja huo huo. Kwa hiyo mnaombwa wote kujitokeza kwa wingi. Kamati ya ufundi ikiongzwa na Profesa Maji Marefu, imeishajiandaa vya kutosha. *(Makofi/Kicheko)*

Tangazo la mwisho, leo saa saba mchana baada ya kuahirisha hapa, tunafungua rasmi *Gym* yetu hapa. *Gym* ile tuliyokuwa tunasema iko katika jengo lile jipya, tunaifungua saa saba mchana. Kwa hiyo wote mnakaribishwa.

## HOJA ZA SERIKALI

## AZIMIO

### Azimio la Kuridhia Itifaki ya *SADC* ya Fedha na Uwekezaji *(SADC Protocol on Finance and Investment)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Fedha na Uwekezaji wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika - *SADC (The SADC Protocol on Finance and Inestment)*.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni miongoni mwa nchi 14 Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika inayosimamiwa na Mkataba ujulikano kama *The Treaty on The Southern African Development Community* ambao ulisainiwa na Wakuu wa nnchi, wanachama wa *SADC* tarehe 17 Agosti, 19

**SPIKA:** Wale wanaotoka, watoke kwa staha na kimya. Tusilete vurugu humu ndani.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA):** Madhumuni Makuu ya Umoja huu, ni kuimarisha ushirikiano wa kikanda, na mtangamano ili kuleta maendeleo ya kichumi, kwa nchi wanachama na hivyo kuboresha maisha ya wananchi kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 21 cha Mkataba wa Jumuiya ya Nchi za *SADC,* kinazitaka nchi wanachama kushirikiana katika nyanja mbalimbali kwa nia ya kuleta maendeleo na mtangamano kwa misingi ya haki usawa na kwa faida ya wote.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 18 Agosti, 2006, Wakuu wa nchi wanachama wa *SADC* walisaini itifaki ya *SADC* ya Fedha na Uwekezaji mjini Maselu, Lesotho na Tanzania ni mojawapo ya nchi 14 wanachama zilizotia saini itifaki hii. Kifungu cha 29 cha itifaki kinabainisha kwamba itifaki hii itaanza kuwa na nguvu za kisheria siku 30 baada ya theluthi mbili ya nchi za *SADC* kuridhia. Hadi kufikia tarehe 16 Aprili, 2010, itifaki hii ilipata nguvu za kisheria ya utekelezaji baada ya nchi tisa kati ya nchi 14 za *SADC* zilizosaini itifaki hii kuwasilisha hati za kuridhia. Nchi hizo ni Angola, Botswana, Lesotho, Mauritius, Msumbiji, Malawi, Afrika Kusini, Namibia pamoja na Zambia. Mpaka kufikia Juni 2014, nchi 11 tayari zimeridhia itifaki hii, na nchi ambazo bado hazijaridhia ni pamoja na Tanzania, Zimbabwe pamoja na Shelisheli.

**SPIKA:** Naomba tupunguze kuzungumza!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 22 (9) na 22(10) ya Mkataba ulioanzisha *SADC*, nchi ambayo haijaridhia itifaki hairuhusiwi kushiriki katika kufanya maamuzi na haifungwi kisheria katika utekelezaji wa maamuzi mbalimbali ya itifaki husika. Pamoja na kwamba Tanzania haijaridhia itifaki husika, tayari kuna maeneo mengi ya itifaki hii ambayo inashiriki.

Maeneo hayo ni pamoja na kufuatilia viashiria vya uchumi wa jumla, ushirikiano katika masuala ya kodi, ushirikiano na uratibu wa sera za kudhibiti ubadilishaji wa fedha na mitaji, ushirikiano wa taasisi za fedha zisizo za kibenki, ushirikiano katika masoko ya hisa na mitaji na ushirikiano na taasisi za fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, lengo la itifaki hii ni kuweka mazingira bora ya sera za fedha na uwekezaji kwa nchi wananchama ili yaendane na malengo makuu ya *SADC* ikiwemo mzunguko huru wa mitaji, bidhaa, nguvukazi na huduma. Lengo hili litafikiwa iwapo kutakuwa na mtangamano katika uchumi wa nchi wanachama na ushirikiano katika taratibu za utendaji katika maeneo ya fedha na uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Itifaki ya *SADC* ya Fedha na Uwekezaji imegawanyika katika sura 11 zenye jumla ya vifungu 32. Sura ya kwanza yenye vifungu 1 na 2 inaeleza madhumuni ya tafsiri maeneo muhimu yaliyotumika katika itifaki hii. Sura ya 2 yenye kifungu cha tatu inahusu ushirikiano katika sera za kukuza na kuvutia uwekezaji katika Jumuiya ya *SADC* kwa lengo la kuongeza uwekezaji, ufanisi, kulinda na kuboresha mazingira ya uwekezaji katika nchi wanachama.

Sura ya 3 inahusu kifungu cha 4 inafafanua shabaha na utaratibu wa kurazinisha *(harmonise)* sera za kiuchumi za nchi wanachama katika kuwianisha viwango vya viashiria vya uchumi jumla *(marco economic convergence)* kwa kuzingatia sera za maendeleo ya uchumi endelevu. Kwa mujibu wa kifungu hiki nchi wanachama zinategemewa kujenga uchumi madhubuti wenye uwiano na unaosimamia vizuri sera za kiuchumi *(stability oriented macro economic policies)*.

Sura ya 4 yenye kifungu cha 5 inazungumzia ushirikiano kwenye masuala ya kodi kwa nchi wanachama. Sehemu hii inazitaka nchi wanachama kushirikiana katika masuala yanayohusu kodi na uratibu wa mifumo ya kodi ya kikanda.

Sura ya 5 yenye vifungu vya 6 hadi 10 inahusu ushirikiano katika maeneo yanayohusu kusimamiwa Benki Kuu za nchi wanachama ambayo malengo yake ni kuweka mfumo wa ushirikiano katika kuoanisha utaratibu wenye sera za ubadilishaji fedha na mitaji, kurazinisha mifumo ya kisheria, kiutendaji, kuweka miundombinu ya ushirikiano, uratibu wa mifumo ya malipo, kutumia TEHAMA katika uendeshaji na uboreshaji wa huduma za Benki Kuu na kuboresha udhibiti wa usimamizi wa mabenki katika kuzingatia viwango vya kimataifa.

Sura ya 6 yenye kifungu 11 inabainisha uanzishwaji wa mitandao ya taasisi za kifedha zinazohusisha utoaji wa mikopo ya maendeleo *(development finance institutions)* katika nchi wanachama ili kuongeza upatikanaji wa fedha za kuanzisha na kutekeleza miradi mikubwa ya kikanda.

Nchi wanachama zinatakiwa kuanzisha mtandao wa taasisi za fedha za maendeleo ya kuwezesha utendaji wa taasisi hizo ndani ya nchi wanachama na kikanda. Aidha, mtandao huo utajihusisha na kuzijengea uwezo taasisi zitakazoshiriki ikiwa ni pamoja na kuzipatia utaalamu na utambuzi na uchambuzi wa miradi na usimamizi wa mikopo ya muda mrefu.

Sura ya 7 yenye vifungu 12 hadi 14 inazungumzia ushirikiano wa nchi wanachama katika uendeshaji wa masoko ya fedha na mitaji *(cooperation in regional capital and financial markets and stock exchanges)* na usimamizi wa huduma za taasisi za fedha ambazo siyo za kibenki *(the non banking financial services)*.

Ili kutimiza lengo hili, nchi wanachama zinapaswa kuafikiana kuhusu uendeshaji na usimamizi wa taasisi za fedha zisizokuwa za kibenki na uimarishaji wa masoko ya fedha na mitaji *(capital and financial markets)*.

Mheshimiwa Spika, sura ya 8 yenye kifungu cha 15 inahusu ushirikiano wa nchi wanachama katika kudhibiti biashara ya fedha haramu *(anti-money laundering)*.

Ili kutekeleza jukumu hili, nchi wanachama zinatakiwa kushirikiana kujenga mfumo wa kikanda na kudhibiti biashara ya fedha haramu.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka jambo hili hata hapa lilishajitokeza sana baada ya Mheshimiwa Mpina kulipigia kelele sana suala la utoroshaji wa fedha. Kiambatanisho kitakachofafanua hatua za utekelezaji wa azma hii kimekwishaandaliwa na kusainiwa na Wakuu wa nchi na Serikali katika mkutano wao wa kilele uliofanyika mwezi Agosti, 2012, Mjini Maputo, Msumbiji na kitaongezewa katika itifaki hii.

Sura ya 9 yenye kifungu 16 inahusu Mfuko wa *SADC* wa Uandaaji na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo (*SADC Project Preparation and Development Fund)*. Nchi wanachama zinapaswa kuanzisha mfuko wa kuandaa na kuendeleza miradi ya maendeleo. Mfuko huo utagharamia wataalamu waelekezi, kuibua na kutambua miradi, kufanya upembuzi yakinifu na uendelezaji wa miradi itakayochaguliwa. Mfuko huu umeanzishwa na uko kwa muda katika Benki ya Maendeleo ya Afrika Kusini, inakusidiwa kwamba mfuko huu baadaye utaunganishwa na Mfuko wa Maendeleo wa *SADC* na hivyo kuandaa dirisha litakaloshughulikia maendeleo ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, sura ya 10 inahusu vifungu vya 17 na 22 ambavyo vinabainisha masuala ya kiutawala yanayohusu usimamizi wa utekelezaji wa itifaki. Sura hii inabainisha taasisi ambazo zinahusika kulingana na matakwa ya vifungu vya 9, 10 na 11 vya mkataba wa *SADC*. Taasisi hizo ni pamoja na:-

(a) Kamati ya Mawaziri wa Fedha na Uwekezaji wa nchi wanachamana wa *SADC*.

(b) Kamati ya Magavana wa Benki Kuu za nchi wanachama wa *SADC*.
(c) Jopo la Mapitio ya Masuala ya Uchumi, jopo hili linaundwa na Kamati ya Mawaziri wa Fedha na Uwekezaji pamoja na Magavana wa Benki Kuu za nchi wanachama

na jopo hili limepewa jukumu la kufanya mapitio ya masuala ya uchumi mpana na viashiria vyake.

Mheshimiwa Spika, sura ya 11 yenye vifungu 23 hadi 32 vya itifaki inabainisha kuwa kutakuwa na taratibu za usuluhisho wa migogoro, majukumu ya nchi wanachana katika kutekeleza matakwa ya itifaki, taratibu za kufanya marekebisho ya itifaki na taratibu za kuridhia na kujiondoa katika itifaki hii.

Mheshimiwa Spika, faida za itifaki hii: Mpango mkakati wa maendeleo wa *SADC* unatoa dira ya mtangamano wa nchi wanachana wa *SADC* ambayo ni Soko Huru la Biashara, hii ni ya mwaka 2008, Umoja wa Forodha ya mwaka 2010, Soko la Pamoja ya mwaka 2015, Umoja wa Sera za Fedha *(Monetary Union)* ya mwaka 2016 na hatimaye Sarafu Moja *(Single Currency)* mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa nchi wanachama wa Jumuiya ya nchi za *SADC* zinatekeleza hatua ya kwanza ya mtangamano wa soko huru la biashara ambalo lilizinduliwa mwaka 2008.

Eneo huru la biashara la *SADC* ambalo Tanzania inashiriki, linalenga kuondoa ushuru wa forodha na vikwazo vingine vya kibiashara miongoni mwa nchi wanachama na hivyo kukuza biashara baina ya nchi wanachana wa *SADC*, kuongeza uzalishaji na maingiliano ya kijamii, na katika eneo hili kumekuwa na ongezeko la biashara kati ya Tanzania na nchi wanachama wa *SADC*. Tanzania itanufaika iwapo itatumia kikamilifu fursa zitakazotokana na Itifaki ya *SADC* ya Fedha na Uwekezaji zikiwemo kuongezeka kwa uzalishaji, kupanuka kwa soko la mitaji, kuimarika kwa bima na mifuko ya pensheni na ukuaji wa uchumi ulio endelevu kutokana na utangamano wa kikanda.

Mheshimiwa Spika, kutekelezwa kwa itifaki hii kutaongeza fursa ya ajira kwa Watanzania. Ushirikiano katika masuala ya kodi yataiwezesha nchi kuwa na mifumo yenye ufanisi katika kuongeza tija na kusimamia masuala ya kodi. Kwa kufuatilia mwenendo wa viashiria vya uchumi mpana kutaongeza nidhamu katika uendeshaji wa uchumi na kunufaisha kwa malengo yaliyowekwa.

Mheshimiwa Spika, maeneo mahsusi ambayo Tanzania tayari inanufaika ni pamoja na kushiriki kwenye mtandao wa taasisi za kifedha za maendeleo za *SADC*, Kituo cha Kuendeleza Raslimali Fedha kimeanzishwa na Tanzania inanufaika kwa kujengewa uwezo *(DFRC)*.

Mheshimiwa Spika, taasisi za Tanzania ambazo ni wanachama na zinaendelea kunufaika kwa kujengewa uwezo ni pamoja na *TIB Development Bank, NDC* na *SIDO*. Aidha, mfuko wa fedha kwa ajili ya kuandaa na kuendeleza miradi ya maendeleo umeanzishwa na vilevile majadiliano yanaendelea kuhusu uendeshaji wa mfuko wa fedha wa kugharamia miradi ya maendeleo ya nchi wanachama wa *SADC*. Tanzania pia inashirikiana na mabenki mengine ya maendeleo kubainisha miradi ya kufanya upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Mamlaka ya Bima, Mitaji, Taasisi za Fedha zisizo za kibenki imeanzishwa na aidha Mamlaka ya Usimamizi wa Mifuko ya Kijamii, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana na Mamlaka ya Usimamizi wa Masuala ya Usimamizi wa Masuala ya Bima zimeanzishwa na zinafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni mshirika katika Kamati ya *SADC* ya Masoko ya Mitaji (*Committee of the Insurance Securities and Non Banking Financial Institutions)* na ile ya Masoko ya Hisa *(The Committee of SADC on Stock Exchanges)* ambazo zilianzishwa mwaka 1997.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano katika kujenga uwezo wa watendaji kwenye masuala ya kodi umeshaanza kutekelezwa.

Tanzania imeshaingia mkataba wa kutokutozwa kodi mara mbili *(double taxation agreement)* na nchi ya Afrika Kusini na Zambia na ipo katika hatua mbalimbali ya kukamilisha mkataba na nchi nyingine wanachama wa *SADC*.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyobainisha hapo awali, Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo haziridhia itifaki hii, kutokana na kutokuridhia itifaki hii, Tanzania haina haki ya kutoa maamuzi yoyote katika vikao vinavyohusu masuala ya fedha na uwekezaji kikanda.

Nairudia hii; Tanzania haina haki ya kutoa maamuzi yoyote katika vikao vinavyohusu masuala ya fedha na uwekezaji ya kikanda. Hivyo, ni muhimu kwa Tanzania kuridhia itifaki hii ili ipate fursa ya kushiriki katika kutoa maamuzi yanayohusu masuala ya fedha na uwekezaji katika kuleta maendeleo ya nchi na mtangamano wa *SADC* kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuridhia itifaki hii, Tanzania itahitajika kukabiliana na changamoto mbalimbali hususani kuongezeka kwa uwekezaji na uzalishaji, kuimarisha miundombinu muhimu ya uzalishaji na usafirishaji, matumizi ya teknolojia ya kisasa na kuongeza uwezo wa ushindani kwa upande wa biashara ya kimataifa. Aidha, Tanzania itahitaji kuweka utaratibu mzuri wa kukabiliana na vihatarishi vya soko la mitaji.

Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha Watanzania kunufaika na fursa zitakazotokana na itifaki hii, Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Viwanda na Biashara na wadau wengine, itaandaa programu na mkakati wa kitaifa wa utekelezaji wa fedha na uwekezaji pamoja na kutoa elimu kwa umma.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa kuwasilisha Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Fedha na Uwekezaji wa nchi za *SADC (The SADC Protocol on Finance and Investment)* kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)*, kwa mujibu wa mkataba ambao ulisainiwa na Wakuu wa Nchi wanachama wa *SADC* tarehe 17 Agosti, 1992;

Na kwa kuwa, mkataba unaoitwa Mkataba wa *SADC* wa mwaka 1992 *(The SADC Treaty)* unazitaka nchi wanachama wa *SADC* kushirikiana katika nyanja mbalimbali ili kuleta maendeleo kwa misingi ya haki, usawa na faida kwa wote;

Na kwa kuwa, mkataba unaelekeza kwamba kila itifaki itakayoandaliwa itaidhinishwa na mkutano wa Wakuu wa Nchi wanachama wa *SADC* na itakuwa wazi kwa ajili ya kusainiwa na hatimaye kuridhiwa na nchi wanachama kwa mujibu wa taraitibu zao; Na kwa kuwa, Itifaki ya *SADC* ya Fedha na Uwekezaji *(The SADC Protocol on Finance and Investment)* ilitiwa saini na wakuu wa nchi wanachama tarehe 18 Agosti, 2006 Mjini Maseru, Lesotho ambapo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mojawapo ya nchi wanachama wa *SADC* ambazo zilitia saini itifaki hii;

Na kwa kuwa, lengo la itifaki hii ni kuboresha sera za kifedha na uwekezaji ili kuboresha biashara na kuvutia vitega uchumi miongoni mwa nchi wanachama;

Na kwa kuwa kwa kujiunga na mkataba huu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itafaidika kwa kukuza biashara za ndani na za kimataifa, kukuza sekta ya uwekezaji na kuboresha vitega uchumi vya taifa, vilevile Tanzania itafaidika kwa kuweka mazingira bora ya sera za fedha na uwekezaji katika *SADC* ikiwemo mzunguko huru wa mitaji, bidhaa, nguvukazi na huduma, hali itakayopelekea kukuza ajira na kuboresha maisha ya Watanzania;

Hivyo basi, kwa kuzingatia manufaa yatakayotokana na itifaki hii kwa Tanzania na pia umuhimu wa kuridhia itifaki hii, Bunge hili katika Mkutano wa 15 na kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, linaazimia kuridhia itifaki hii iitwayo Itifaki ya *SADC* ya Fedha na Uwekezaji *(The SADC Protocol on Finance and Investment)*.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya naomba mridhie Itifaki ya *SADC* ya Fedha na Uwekezaji *(The SADC Protocol on Finance and Investment)* ili Tanzania iweze kunufaika na hivyo kujenga uchumi imara na endelevu na kupunguza umaskini hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja!

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante. Siku hizi sijui mnakuwa wapi! Ahsante, hoja imeungwa mkono. Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati iliyohusika na *protocol* au kwa niaba yake Mheshimiwa Zubeir!

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara juu ya Azimio la kuridhia Itifaki ya *SADC* ya Fedha na Uwekezaji *(SADC Protocol on Financial and Investment)*.

Mheshimiwa Spika, utangulizi: Kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara yanayohusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Fedha na Uwekezaji wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika *(The SADC Protocol on Finance and Investment)*.

Itifaki ya Fedha na Uwekezaji ilitiwa saini na Wakuu wa Nchi 14 wanachama tarehe 18 Agosti, 2006 Mjini Maseru, Lesotho.

Mheshimiwa Spika, kuanzia tarehe 20 Oktoba, 2013 hadi tarehe 5 Novemba, 2013 Kamati ilipata fursa ya kuwasikiliza wadau mbalimbali ambao walialikwa kufika mbele ya Kamati ili kutoa maoni yao.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya taasisi na Wizara ambazo zilishiriki ni pamoja na Wizara ya Fedha, Ofisi ya Waziri Mkuu - Uwekezaji, Wizara ya Viwanda na Biashara, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, taasisi nyingine zilileta michango kwa maandishi. Aidha, mnamo tarehe 5 Juni, 2014 Kamati ilifanya kikao kingine Dodoma kwa lengo la kuboresha zaidi taarifa hii. Kwa niaba ya kamati napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wote waliotoa maoni ambayo kwa kiasi kikubwa yameisaidia Kamati katika kuandaa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata ufafunuzi wa masuala yote ye msingi kama vile namna bora ya kuitekeleza Itifaki, na endapo katika kuitekeleza itakinzana na mikataba na makubaliano ya kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ama kuathiri majadiliano ya *ACP/EU* pamoja na mambo mengine ya msingi yenye maslahi kwa taifa letu. Kamati ilihakikishiwa kuwa hakuna athari yoyote kwa Tanzania kuridhia Azimio hili kwa kuwa Tanzania ilishiriki katika majadailiano ya itifaki mwaka 2006. Katika majadiliano hayo Tanzania ilihakikisha masuala ya ushirikiano katika itifaki hii hayakinzani na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, Kamati ilitaka kujua kwa nini Azimio hili limechelewa sana kuletwa Bungeni na kuletwa wakati huu ambapo Tanzania inakabiliwa na migogoro inayohusisha baadhi ya nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, Maudhui ya Azimio: Itifaki hii ya Fedha na Uwekezaji inajielekeza katika kuweka mazingira bora ya sera za fedha na uwekezaji kwa nchi washirika ili zishabihiane na malengo ya *SADC* ambayo ni uwepo wa mzunguko huru wa mitaji, nguvukazi na huduma.

Sambamba na hilo, Itifaki inalenga vilevile kuhakikisha kuwa mabadiliko yoyote ya kisera katika mojawapo ya nchi washirika hayaleti athari katika ushirikiano wa kibiashara na ukuaji wa sekta za uzalishaji miongoni mwa nchi washirika. Aidha, Itifaki inajikita katika kuhakikisha kuwa nchi washirika zinakuwa na maendeleo endelevu ya kiuchumi ili hatimaye ziweze kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, itifaki hii inahusu ushirikiano katika sera za kukuza na kuvutia uwekezaji katika Jumuiya ya *SADC* kwa lengo la kuongeza uwekezaji, ufanisi, kulinda na kuboresha mazingira ya uwekezaji katika nchi wanachama. Itifaki hii imeelezea ushirikiano kwenye masuala ya kodi kwa nchi wanachama, kuoanisha utaratibu kwenye sera za ubadilishaji fedha na mitaji, kurasimisha mifumo ya kisheria na kiutendaji na kuboresha udhibiti na usimamizi wa mabenki kwa kuzingatia viwango vya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, madhumuni na faida ya kuridhia Azimio: Katika dunia ya sasa umuhimu wa nchi kutumia fursa zinazopatikana kupitia ushirikiano wa kikanda, katika kuleta fursa ambazo nchi itazipata baada ya kusaini makubaliano ambayo mambo ya msingi yamezingatiwa kwa mapana na marefu ni suala lisiloepukika. Kutokana na ukweli huu, Azimio hili ni muhimu kuridhiwa na Bunge letu ili Tanzania iweze kunufaika na soko litokanalo na uwepo wa eneo huru la biashara *(free trade area)* ambalo lilizinduliwa mwaka 2008.

Eneo huru la biashara la *SADC* ambalo Tanzania inashiriki linalenga kuondoa ushuru wa forodha na vikwazo vingine vya kibiashara miongoni mwa nchi wanachama na hivyo kukuza biashara baina ya nchi wanachama wa *SADC*.

Mheshimiwa Spika, fursa pana za mitaji, kuimarika kwa mifumo ya kibenki, kuongezeka kwa uzalishaji, matumizi ya mifumo yenye ufanisi katika kuongeza tija na kusimamia masuala ya kodi, ongezeko la ajira na ukuaji wa uchumi endelevu ni miongoni mwa faida lukuki zinazoweza kupatikana kutokana na ushiriki na utayari wetu wa kuzitumia kikamilifu fursa hizi za Itifaki ya *SADC*.

Ni kwa msingi huu Kamati inaona kuna umuhimu mkubwa wa Bunge kuridhia itifaki hii ambayo kwa bahati mbaya sana tumechelewa kuiridhia.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati: Itifaki ya Fedha na Uwekezaji ya Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika imegawanyika katika Sura 11 zenye jumla ya vifungu 32. Kamati ilipitia vifungu vyote ili kubaini faida na hasara ambazo Tanzania itazipata kwa kuridhia itifaki hii. Kamati ilitoa maoni mbalimbali katika kila kifungu na kukubaliana na Serikali karibu maeneo yote yaliyohusiana na uwekezaji, utawala bora katika masuala ya

uchumi na uwekezaji, uoanishaji wa sheria na sera za fedha na uwekezaji na mahusiano mbalimbali ya kikanda katika biashara, uwekezaji na fedha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kukubaliana na mambo mengi, Kamati haikuridhika na maelezo ya sababu za Serikali kuchelewa kuleta bungeni Azimio hili kwa ajili ya kuridhia Itifaki ya *SADC*. Tangu Azimio hili lisainiwe na Wakuu wa nchi za *SADC* ni takriban miaka Saba (7) sasa imepita. Hili si jambo jema na linaashiria udhaifu katika kufanya maamuzi mazuri kwa haraka kwa faida ya nchi yetu.

Kamati inaishauri Serikali kuwa na mikakati ya dhati ya kuleta bungeni maazimio ili kuweza kuridhiwa mapema iwezekanavyo kuliko ilivyo hivi sasa ambapo maazimio mengi yanaletwa kwa kuchelewa sana. Aidha, Kamati inashauri Serikali kuwa pindi inapoingia mikataba mbalimbali, iwe ya Jumuiya za Afrika au nje ya Afrika; wananchi washirikishwe mapema iwezekanavyo kupitia mijadala ya kitaifa ili waweze kushiriki kikamilifu kutoa maoni yao kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, suala la kuwa na sarafu moja ya *SADC* kwa wanachama wake ifikapo mwaka 2024 linakinzana na makubaliano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kuwa na sarafu moja kwa nchi wanachama ifikapo 2018. Kamati inahoji tuna mipango gani ya kujinasua kutoka mtego huu wa sarafu mbili tofauti.

Pamoja na maelezo mazuri kwamba Tanzania inaweza kufaidika na mambo mengine mengi kabla ya kufikia hatua ya kuwa na sarafu moja, Kamati inashauri Serikali iangalie kwa kina suala hili lenye mkanganyiko ambalo linaweza kuleta madhara, kwani nchi ikisharidhia Azimio inaweza kuwa ni vigumu sana kujizuia kuutekeleza mkataba huo, hata kama suala hili limo katika majadiliano ya Utatu kati ya *EAC-SADC-COMESA (tripartite negotiations)*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuridhia Azimio hili, Wajumbe wa Kamati walionesha wasiwasi kuhusu uwezekano wa utoroshwaji wa mitaji kwenda nchi za nje *(capital flight)*. Hivyo Serikali inashauriwa kuweka mikakati na taratibu za kukabiliana na suala hilo na halikadhalika kuweka sera madhubuti za uchumi zitakazoleta utulivu wa uchumi ili kuwawezesha wawekezaji kuwekeza mitaji yao nchini badala ya kuitorosha na kuwekeza nchi za nje.

Kutokana na sharti la Itifaki la kuwa na vivutio vya kodi vinavyoshabihiana kwa nchi wanachama ili kuondoa ushindani usiokuwa wa haki, ni maoni ya Kamati kuwa Tanzania itapaswa kuwa na vivutio mbadala vitakavyowawezesha wawekezaji mahiri kuendelea kuwa na imani na mazingira ya uwekezaji bila ya kupewa vivutio vya kodi nje ya utaratibu wa sheria kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha matakwa ya Itifaki, Tanzania itahitaji kukabiliana na changamoto mbalimbali hususan kuongeza uwekezaji na uzalishaji, kuimarisha miundombinu muhimu ya uzalishaji na usafirishaji, matumizi ya teknolojia ya kisasa na kuongeza uwezo wa ushindani kwa upande wa biashara za kimataifa.

Mheshimiwa Spika, ushauri mwingine muhimu uliotolewa na Kamati ni pamoja na mikakati ya Serikali ya kuelimisha wananchi kuhusu itifaki hii pamoja na nyingine nyingi ambazo zinaridhiwa na Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, kutoa elimu kwa itifaki hii kutawawezesha jumuia za kibiashara vijana, wanawake…

**SPIKA:** Jamani Waheshimiwa, tuko ndani ya Bunge, wanaofikiri wanapenda kuongea watoke nje. Naomba uendelee. *(Makofi)*

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA):** Vijana na wanawake ambao ndiyo wadau muhimu katika itifaki hii kunufaika na malengo ya kujipatia maendeleo. Serikali itoe elimu kwa umma ili kuondoa hofu kwa wadau walio wengi ambao hawana uthubutu katika masuala muhimu ya kimataifa na kutoa elimu itakayowapa ujuzi wananchi wetu ili waweze kuwa kwenye nafasi nzuri kiushindani.

Mheshimiwa Spika, uhusiano mwema na nchi tunazofanya nazo biashara ni jambo muhimu sana kwa mustakabali wa uchumi wa nchi yetu. Hivi karibuni imezuka tabia ya makundi mbalimbali ambayo si wasemaji wa Serikali kuhusu mambo yetu ya nje ya nchi, kutoa taarifa ambazo zimekuwa chanzo cha matatizo na majirani zetu na kuleta athari kubwa kiuchumi, kisiasa na kidiplomasia.

Kamati inashauri Serikali iwe makini katika kuzuia jambo hili ili kukuza mahusiano mazuri na jirani zetu kwa manufaa ya taifa letu. Aidha, kuna baadhi wa wananchi wachache ambao wamekuwa wakitumia mitandao ya kijamiii katika kuchochea migogoro na nchi jirani. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua stahiki dhidi ya watu hao ili kuepusha migogoro.

Mheshimiwa Spika, hitimisho: Kwa niaba ya Kamati, naomba nitumie fursa hii kuishukuru sana Serikali kupitia Wizara ya Fedha kwa kuandaa Azimio hili. Shukrani za pekee ziwandee Waziri wa Fedha Mheshimiwa Saada Mkuya, Mbunge pamoja na Manaibu wake wawili Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, Mbunge na Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge.

Aidha, napenda kuwapongeza Watumishi wa Wizara chini ya Katibu Mkuu Dkt. Likwelile pamoja na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kujadili Azimio hili. Hivyo sasa napenda kuchukua nafasi hii ya kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara kwa mchango wao mkubwa katika kufanikisha kazi hii kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina – Mwenyekiti, Mheshimiwa Dunstun Luka Kitandula, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Freeman owe, Mheshimiwa Dkt. Terezya Pius Luoga Huvisa, Mheshimiwa Margaret Agness Mkanga.

Pia, Mheshimiwa Ester Lukago Minza Midimu, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mheshimiwa Joyce John Mukya, Mheshimiwa David Zakaria Kafulila, Mheshimiwa Vicky Pascal Kamata, Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, Mheshimiwa Shawana Bukhet Hassan, Mheshimiwa Naomi A. M. Kaihula, Mheshimiwa Khatibu Said Haji, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Mohamed Hamis Misanga na Mheshimiwa *Eng*. Habib Juma Mnyaa,

Mheshimiwa Spika, naomba nimalize kwa kuwashukuru watendaji wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah

Aidha, nawapongeza kwa dhati Makatibu wa Kamati Ndg. James Warburg, Ndg. Lawrence R. Makigi na Msaidizi wa Kamati Ndg. Paulina Mavunde kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii. Baada ya kusema hayo, naunga mkono Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya *SADC* ya Fedha na Uwekezaji.

**SPIKA:** Tunashukuru sana kwa majina hayo. Unawasilisha au unafanyaje?

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA):** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja na nawasilisha.

**SPIKA:** Haya, ahsante. Sasa nitamuita Msemaji kutoka Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio hili, Mheshimiwa Christina Lissu.

**MHE. CHRISTINA M. LISSU (K.n.y. MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Fedha, naomba kuwasilisha Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Kuridhia Azimio la Itifaki ya *SADC* Kuhusu Fedha na Uwekezaji *(SADC Protocol on Finance and Investment)* kwa mujibu wa *Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu Bunge, Toleo la 2013)*

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 18 Agosti, 2006, Wakuu wa Nchi 14 za *Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC)* walitia saini *Itifaki ya SADC Kuhusu Fedha na Uwekezaji*, yaani *(SADC Protocol on Finance and Investment)* katika Mji wa Maseru, Lesotho.

Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete alisaini Itifaki hiyo kwa niaba ya Tanzania. Wengine waliotia saini itifaki hiyo ni Wakuu wa Nchi za Angola, Botswana, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Falme ya Lesotho, Madagascar, Malawi, Mauritius, Msumbiji, Namibia, Afrika Kusini, Falme ya Swaziland, Zambia na Zimbabwe.

Mheshimiwa Spika, Itifaki ya SADC ina jumla ya Ibara 32 na Nyongeza 11 zinazohusu masuala ya ushirikiano kuhusu uwekezaji, mafungamano ya kifedha *(macro-economic convergence)*, ushirikiano katika kodi na masuala yahusuyo kodi, ushirikiano na uratibu wa sera za udhibiti wa fedha za kigeni na usajihishaji wa mifumo ya kisheria na kiutendaji.

Nyongeza nyingine zinahusu ushirikiano juu ya mifumo ya malipo, ushirikiano katika eneo la teknolojia za habari na mawasiliano miongoni mwa Benki Kuu, ushirikiano na uratibu katika eneo la udhibiti na usimamizi wa masuala ya kibenki, ushirikiano juu ya taasisi za fedha za maendeleo, ushirikiano juu ya taasisi na huduma za kifedha zisizo za kibenki na ushirikiano juu ya masoko ya hisa katika *SADC*.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la Itifaki ya *SADC* linatajwa katika Ibara ya 2(1) ya Itifaki kuwa ni kukuza usajihishaji wa sera za fedha na uwekezaji za nchi wanachama ili kuziweka sambamba na malengo ya *SADC* na kuhakikisha kwamba, mabadiliko katika sera za fedha na uwekezaji za nchi wanachama, moja hazilazimu marekebisho yasiyotakikana katika nchi mwanachama mwingine.

Kwa mujibu wa ibara ya 2(2), lengo kuu hilo litatekelezwa kwa kupitia ushirikiano wa kikanda, ushirikiano na uratibu katika sekta za fedha na uwekezaji kwa lengo la kupanua sekta za uzalishaji na kukuza biashara katika kanda ili kupata maendeleo na ukuaji endelevu wa kiuchumi na kufuta umaskini kwa kujenga ushirikiano katika maeneo yote yaliyotajwa katika Nyongeza za Itifaki.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 29 ya Itifaki ya *SADC* inalazimu kwamba, itifaki itaanza kutumika siku 30 baada ya kuridhiwa na angalau theluthi mbili ya nchi wanachama. Kwa kigezo kilichowekwa na Sekretarieti ya *SADC*, theluthi mbili ni sawa na nchi wanachama 10.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa, kwa kadri ya taarifa ilizonazo Kambi Rasmi ya Upinzani, ni nchi wanachama tisa tu ambazo ndizo zilizoridhia itifaki hiyo.

Hivyo basi, kwa sababu hiyo, Itifaki ya *SADC* haijaanza kutumika, miaka takriban nane baada ya kusainiwa na Wakuu wa nchi Wanachama.

Mheshimiwa Spika, Itifaki ya *SADC* ni Mkataba wa Kimataifa. Kwa sababu hiyo, ibara ya 28 ya itifaki imeweka masharti ya kuridhiwa na nchi wanachama kufuatana na kanuni zao za kikatiba.

Kwa nchi kama Tanzania, kama zilivyo nchi nyingine zinazofuata mila na desturi za kisheria na kikatiba na Jumuiya ya Madola, Mikataba yote ya Kimataifa inayosainiwa na nchi yetu inatakiwa kuridhiwa na Bunge lako Tukufu.

Ndiyo maana Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, imelipa Bunge lako Tukufu, mamlaka ya kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inaamini kwamba msimamo huu wa Katiba yetu ulikuwa unajulikana kabla na baada ya Rais Kikwete kusaini Itifaki ya *SADC* mwaka 2006.

Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu, inaamini kwamba Serikali hii ya CCM ilikwisha kufanya maandalizi yote yaliyokuwa yanahitajika kabla ya kutia saini itifaki hii. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kwamba Serikali hii ya CCM ilisaini itifaki hii kwa nia ya kuitekeleza na siyo kwa lengo la kujionyesha tu kuwa na sisi ni sehemu ya *SADC*.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hizi, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inataka kujua sababu zilizoifanya Serikali hii kuchukua miaka nane kuleta Mkataba huu wa Kimataifa mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kupata ridhaa ya Bunge ili uanze kutumika. Vilevile, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali hii ya CCM ilieleze Bunge lako Tukufu kama kuna athari zozote za kiuchumi au kijamii zilizotokana na nchi yetu kuchelewa kuridhia itifaki hii.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imetiliana saini Mikataba ya Uwekezaji *(Bilateral Investment Treaties*) na baadhi ya nchi Wanachama wa Itifaki ya *SADC*.

Mheshimiwa Spika, kwa kadri ya taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani inazo, Tanzania ina mikataba ya aina hiyo na Malawi ambao ulisainiwa tarehe 30 Juni, 2003, Zimbabwe ambao ulisainiwa tarehe 3 Julai, 2003 na Afrika Kusini ambao ulisainiwa tarehe 22 Septemba, 2005.

Aidha, Tanzania ina Mkataba wa Uwekezaji na Mauritius uliosainiwa tarehe 4 Mei, 2009. Kwa taarifa zilizotolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo *(United Nations Conference on Trade and Development)*, hadi kufikia tarehe 1 Juni, 2013, mikataba hiyo kati ya Tanzania na baadhi ya nchi Wanachama wa Itifaki ya *SADC* ilikuwa haijaanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, Kambi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inataka kujua sababu zilizoifanya Serikali hii ya CCM kutokuileta mikataba hiyo katika Bunge lako Tukufu ili ipate ridhaa na kupata nguvu za kisheria. *(Makofi)*

Serikali hii pia ilieleze Bunge lako Tukufu ni lini inatarajia kuileta mikataba hiyo Bungeni kwa ajili ya kupata ridhaa kwa mujibu wa Katiba yetu. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kauli rasmi ya Serikali kulikuwa na sababu gani za kusaini Itifaki ya *SADC* ilhali ilikwishasaini mikataba mingine ya uwekezaji na baadhi ya nchi wanachama wa itifaki hiyo.

Vilevile, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inaitaka Serikali hii ya CCM ieleze faida za kuendelea kuwa na utitiri huu wa mikataba ya kimataifa ya uwekezaji ambayo hata hivyo haitekelezwi kwa sababu haijapata ridhaa ya Bunge kama inavyotakiwa na Katiba yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 3 ya Itifaki ya *SADC* inawataka nchi Wanachama kuratibu taratibu zao za uwekezaji na kushirikiana kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji katika kanda kama ilivyofafanuliwa katika Nyongeza ya 1 ya Itifaki hiyo.

Hata hivyo, maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani na masharti ya itifaki yanapingana na matakwa ya ibara ya 2 ya nyongeza ya 1 ya itifaki yanayoitaka kila nchi mwanachama kuhamasisha uwekezaji katika eneo lake na kuruhusu vitega uchumi hivyo kufuatana na sheria na kanuni zake.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani, wakati ibara ya (3) ya Itifaki inaweka masharti ya ushirikiano baina ya Nchi Wanachama, ibara ya (2) Nyongeza ya (1) inaruhusu ushindani miongoni mwao. Mkanganyiko huu ni hatari kwa maslahi ya nchi yetu. Hii ni kwa sababu rasilimali nyingi zilizomo kwenye Nchi Wanachama wa Itifaki hii zinafanana kwa kiasi kikubwa. Ukiacha Afrika Kusini ambayo ina uchumi wa kiviwanda, Nchi nyingine Wanachama zinategemea kilimo au madini au rasilimali nyingine za asili kwa ajili ya uchumi wao.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira hayo, kuruhusu ushindani, kama inavyopendekezwa na ibara ya (2) ya Nyongeza ya (1), kuna hatari ya kuzifanya nchi hizo kulegeza masharti yao ya uwekezaji kwa kiwango ambacho kitakuwa na madhara makubwa kwa maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii ya nchi hizo. Hatari hii inaitwa *the race to the bottom*, yaani ushindani wa kujichimbia kaburi kati ya nchi na nchi zinazoshindana kuvutia uwekezaji mkubwa katika sekta za uchumi zinazofanana.

Mheshimiwa Spika, aidha, thamani ya ushirikiano chini ya ibara ya (3) ya Itifaki imefifishwa zaidi na masharti ya ibara ya (7) ya Nyongeza ya (1) ambayo inaweka wazi kwamba: "*Masharti hayo ya ushirikiano hayatahusu manufaa, nafuu au misamaha inayoweza kutokea kutokana na mkataba wa uwekezaji baina ya nchi na nchi ambayo Nchi Mwanachama inashiriki au inaweza kushiriki.*"

Mheshimiwa Spika, kwa lugha nyepesi, Tanzania haifungwi na masharti ya ushirikiano na Nchi nyingine Wanachama chini ya ibara ya (3) ya Itifaki ya *SADC* kwa manufaa, nafuu au misamaha ambayo tumewapa wawekezaji kutoka Afrika Kusini, Malawi, Mauritius na Zimbabwe kwa mujibu wa mikataba ya uwekezaji baina ya Tanzania na nchi hizo.

Mheshimiwa Spika, kama ni hivyo, nchi Wanachama wa Itifaki ambazo hazitanufaika manufaa, nafuu au misamaha hiyo zitakuwa na maslahi ya kuendelea kuheshimu matakwa ya Itifaki kuhusu ushirikiano kama Itifaki yenyewe inaruhusu ubaguzi dhidi yao kutoka kwa Nchi Wanachama wengine?

Mheshimiwa Spika, Ibara ya (2) ya Nyongeza ya (1) inaweza ikawa ndio kichocheo kikubwa cha Nchi Wanachama kuacha kushirikiana na hivyo kusambaratisha dhana nzima ya ushirikiano ambayo ndio msingi wa Itifaki hii.

Mheshimiwa Spika, mkanganyiko mwingine uliotengenezwa na ibara ya (6) ya Nyongeza ya (1) inayohusu wawekezaji wa nchi zisizokuwa wanachama wa Itifaki ya *SADC*. Kwa mujibu wa ibara ya 6(1) ya Nyongeza hiyo, vitega uchumi na wawekezaji watakuwa na

fursa na haki sawa katika eneo la Nchi Mwanachama. Aidha, kwa mujibu wa ibara ya 6(2), fursa na haki hizo hazitakuwa pungufu kuliko fursa na haki walizopewa wawekezaji wa nchi zisizokuwa wanachama wa Itifaki.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, usawa huo umefutwa na matakwa ya ibara ya 7(1) ya Nyongeza hiyo inayoruhusu Nchi Wanachama, kufuatana na sheria zao za ndani, kutoa upendeleo kwa vitega uchumi na wawekezaji ili kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa. Kwa kujua kwamba masharti haya yamefuta dhana ya fursa na haki sawa chini ya ibara ya (6), ibara ya 7(2) inazitaka Nchi Wanachama baadaye kusajili tena sera na sheria zao za ndani katika moyo wa kutokubaguana kama ulivyowekwa kwenye ibara ya (6). Hakuna muda wowote uliowekwa kwa Nchi Wanachama kufanya hivyo. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali hii ya CCM kutoa kauli rasmi mbele ya Bunge lako Tukufu kama tafsiri hii ya ibara ya (6) na ya (7) ni sahihi au la.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa utatuzi wa migogoro ni eneo lingine la Itifaki ya *SADC* ambalo linahitaji kutazamwa upya. Chini ya ibara ya 27 ya Nyongeza ya (1), Nchi Wanachama zitahakikisha kwamba wawekezaji wana haki ya kufungua mashtaka katika mahakama, Mabaraza ya Kimahakama au ya kiutendaji na mamlaka nyingine zinazohusika chini ya sheria za Nchi Mwenyeji ili kupata haki kwa malalamiko yao kuhusu jambo lolote linalohusu uwekezaji wowote. Kwa mujibu wa kifungu hiki, endapo mwekezaji atanyimwa haki ya kwenda katika Mahakama ya Nchi Mwanachama, hiyo itakuwa ni ukiukwaji wa Itifaki hii.

Hata hivyo, ibara ya 28 ndio yenye umuhimu mkubwa zaidi, ibara hiyo inawaruhusu wawekezaji kufungua mashtaka kwenye vyombo vya upatanishi wa uwekezaji vya Kimataifa pale ambapo mgogoro unaohusu wajibu wa Nchi Mwanachama kuhusu uwekezaji uliokubaliwa umeshindikana kusuluhishwa kwa maridhiano na baada ya kumaliza nafuu zote za ndani ya nchi na baada ya kupita miezi sita tangu malalamiko yalipowasilishwa rasmi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upatanishi wa nje ambako mwekezaji anaweza kupeleka malalamiko yake, ibara ya 28(2) inatamka kwamba mwekezaji na Nchi Mwanachama wanaweza kukubaliana kupeleka mgogoro wao katika Baraza la *SADC* au Kituo cha Kimataifa cha Utatuzi wa Migogoro ya Uwekezaji, yaani *International Centre for the Settlement of Investment Disputes (ICSID)*, moja ya taasisi nyingi za Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, migogoro inaweza pia kufunguliwa kwa mujibu wa kanuni za upatanishi za Tume ya Umoja wa Mataifa juu ya Sheria za Kimataifa za Biashara, yaani *United Nations Commission on International Trade Law (UNCITRAL) Rules*. Endapo hakuna makubaliano katika kipindi cha miezi mitatu, ibara ya 28(3) inaelekeza kwamba mgogoro husika utapelekwa kwenye upatanishi kwa mujibu wa Kanuni za *UNCITRAL*.

Mheshimiwa Spika, wakati utaratibu wa kutatua migogoro ya uwekezaji chini ya Taasisi hizo umetumiwa sana na wawekezaji kuishtaki Serikali, nchi yetu au taasisi na mashirika yake na kwa sababu hiyo, unafahamika na kupendelewa na wawekezaji, utaratibu wa kutumia *SADC Tribunal* hautekelezeki. Hii ni kwa sababu Baraza hilo limevunjwa kufuatia uamuzi wake katika kesi ya *Mike Campbell (Pty) Limited* & Wenzake dhidi Jamhuri ya Zimbabwe.

Mheshimiwa Spika, kesi hiyo ilifunguliwa chini ya Mkataba wa *SADC* na kikundi cha makampuni ya watu binafsi waliokuwa wanamiliki mashamba makubwa nchini Zimbabwe kupinga kunyang'anywa mashamba yao na Serikali ya Zimbabwe. Walalamikaji, wengi wao wakiwa wakulima wa kizungu, walituhumu kwamba unyang'anyi wa mashamba yao kwa

nguvu ulikuwa batili kwa sababu walizuiliwa kwenda mahakamani na kwamba walibaguliwa kwa misingi ya rangi yao.

Mheshimiwa Spika, katika hukumu yake ya tarehe 28 Novemba, 2008, Baraza la *SADC* lilikubali madai ya walalamikaji, Baraza liliridhika kwamba walalamikaji walinyang'anywa ardhi zao bila kupatiwa fursa ya kwenda mahakamani na kusikilizwa kwa haki, ambavyo ni vigezo muhimu vya utawala wa sheria, na kwa hiyo, Mlalamikiwa amekiuka ibara ya 4(c) ya Mkataba *(wa SADC)*.

Mheshimiwa Spika, Baraza liliamua kwamba, kwa vile Sheria ya Urekebu wa Milki za Ardhi ilikuwa inawaathiri wakulima wa kizungu peke yao na kwa hiyo ilikuwa ya kibaguzi, Serikali ya Zimbabwe ilikuwa imewabagua walalamikaji kwa msingi wa rangi na kwa hiyo imekiuka wajibu wake chini ya ibara ya 6(2) ya Mkataba. Aidha, Baraza hilo liliamua kwamba walalamikaji walikuwa na haki ya kulipwa fidia ya haki, ijapokuwa kiwango cha fidia hiyo hakikutamkwa kwenye hukumu hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Zimbabwe ilipinga uamuzi huo vikali na suala hili hatimaye liliingizwa kwenye duru za kidiplomasia. Hivyo basi, mnamo tarehe 20 Mei, 2011, katika kikao cha dharura cha Wakuu wa Nchi na Serikali wa *SADC*, Nchi Wanachama wa *SADC* ziliamua kutoteua wajumbe wapya wa Baraza la *SADC* na kuzuia Baraza hilo kusikiliza kesi mpya dhidi ya Nchi Wanachama.

Mheshimiwa Spika, kwa maneno mengine, Mahakama ya *SADC* inayotajwa katika ibara ya 28(2)(a) ya Nyongeza ya (1) haipo tena. Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inaitaka Serikali hii ya CCM kutoa kauli rasmi mbele ya Bunge lako Tukufu kama inakubaliana na maelezo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Itifaki hii ya fedha na uwekezaji kwa kuwa ilikwishasainiwa na Wakuu Wa Nchi Wanachama, lakini kuna upungufu ambao ni dhahiri, kwani hakuna kifungu kinachoeleza pindi Nchi Mwanachama itakayoshindwa kutekeleza yale yaliyokubaliwa ni adhabu au hatua au vikwazo gani vinatakiwa kuchukuliwa dhidi ya nchi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 12 inaitaka Nchi Mwanachama kutumia rasilimali zake kiuendelevu wakati huo wakitilia maanani utunzaji wa mazingira. Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge, kwa mikataba ambayo tayari imesainiwa kama ile *Rai Group* ya kufyeka misitu ya Mufindi bila kupanda miti na hivyo kutokuwepo kwa uendelevu wa misitu hiyo. Je, baada ya kuridhiwa kwa itifaki hii mikataba ya awali itatenguliwa kuwekwa kifungu cha matumizi endelevu?

Mheshimiwa Spika, ibara ya 19 katika kiambatanisho cha (1) inahusu ushirikiano kwenye uwekezaji, Itifaki inasema kuwa kila nchi mwanachama lazima ijisajihishe na malengo ya kuendeleza kanda na kuwa kanda ya uwekezaji ya *SADC* ambayo pamoja na mambo mengine inaendeleza mkakati wa mtangamano *(intergration)* wa kanda kwa kuhuhisha sera na sheria ili ziendane kwa nchi zote mwanachama. Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge ni kwa vipi Ibara hiyo inazifanya Nchi Wanachama kuwajibika, kwani Itifaki hii haionyeshe mpango mkakati wa utekelezaji na ni muda gani nchi mwanachama zinatakiwa ziwe zimetekeleza matakwa ya kifungu hiki *(Accountability for performance is weakened by the fact that the FIP does not contain any timelines. Consequently, there is no deadline for implementation)*.

Mheshimiwa Spika, aidha, haionesha popote kuwa makubaliano ya itifaki yanayotakiwa kutekelezwa na wanachama pale mwanachama akishindwa kuyatekeleza ni hatua gani

zitachukuliwa. Badala yake matakwa ya itifaki yameachwa kwa Mawaziri wa Fedha wa Nchi Mwanachama kutekeleza matwaka au makubaliano ya itifaki.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba utekelezaji wa itifaki umejikita zaidi kwa *secretariat* ya *SADC* badala ya Nchi Wanachama na hivyo kupelekea kutokuwepo kwa msukumo wa uwajibikaji kwa Nchi Mwanachama kutekeleza uhitaji wa kutoa taarifa kwa kipindi kilichokubaliwa juu ya utekelezwaji wa vifungu vya itifaki. Kasoro hizi zinatoa mwanya kwa nchi mwanachama kushindwa kutekeleza matakwa ya itifaki hii.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa tathmini iliyofanywa na Mwakilishi Mkaazi *wa* Taasisi ya Kijerumani *ya FES, ofisi ya Botswana Dr. Marc Meinardus* kwenye andiko lake la *Deepening Integration in SADC,* kuhusu lengo la pili kifungu kidogo cha c kwenye Itifaki hii. Ameuliza ni kwa vipi ushirikiano kwenye masuala ya kodi utaongeza utengamano wa *SADC* na kusaidia Nchi Mwanachama kufikia malengo ya kukua kwa uchumi na mwisho kuwepo kwa maendeleo endelevu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kodi inakwenda sambamba na matumizi ya nchi ambayo ni utoaji wa huduma za msingi kwa wananchi. Hivyo, ushirikiano wa kodi pia unatakiwa uende sambamba na utoaji wa huduma za msingi au matumizi ya nchi kwa ujumla. Kwa hiyo basi, ni kwa nini kusiwepo utaratibu wa ushirikiano kwenye matumizi kwa nchi mwanachama? Hii ni kutokana na ukweli kwamba tumekuwa na kilio cha muda mrefu kuhusu jinsi gani matumizi ya nchi yasivyoendana na mipango tunayoipanga na hivyo kupelekea kuwa hapa tulipo. Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi zaidi kwenye lengo hili.

Mheshimiwa Spika, lengo la pili la Itifaki kifungu kidogo cha (j) kinachohusu ushirikiano kwenye asasi za fedha zilizo rasmi, lakini zisizo za kibenki zimeachwa na ni ukweli kwamba Nchi Mwanachama zimekuwa zikiendeshwa kwa asasi za fedha ambazo ni rasmi na zisizo rasmi. Hivyo basi, kutokutambua kazi nzuri inayofanywa na taasisi zisizo rasmi ambazo kwa kiasi kikubwa ndio watoaji wa mikopo kwa wafanyabiashara wadogo wadogo na wale wenye kipato kidogo, inaleta upungufu katika hoja hii.

Mheshimiwa Spika, sekta ndogo ya fedha na sekta ya fedha isiyo rasmi ndio chanzo kikuu cha fedha za mitaji kwa wafanyabiashara wadogo wadogo na biashara ndogo ndogo na za kati kwa Nchi Mwanachama wa *SADC*.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, mkakati wowote ambao hauitambua sekta ya fedha isiyo rasmi, siyo mkakati makini kwa ajili ya kuleta maendeleo endelevu kwa wananchi wa Nchi Mwanachama. Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atupe maelezo ya ziada katika jambo hili, aidha, kutokuwepo kwa ushawishi wa Sera za kuzilazimisha benki zinazofanya kazi katika ukanda wa *SADC* kuweka sera za kuwakopesha sekta isiyo rasmi na kukopesha uanzishwaji wa viwanda vidogo na vya kati, ni dhahiri hakutakuwepo na maendeleo endelevu ya kupambana na umaskini na kukuza ajira kwa Nchi Wanachama.

Mheshimiwa Spika, inaweza kuonekana kwamba hoja hizi ni mambo ya ndani kwa Nchi Mwanachama, lakini kwa kuwa lengo la Itifaki hii ni kuleta maendeleo endelevu kwa Nchi Mwanachama, hivyo ili *SADC* ioneshe kuwa ni chombo makini na chenye dhamira ya kweli, ni muhimu kuzitaka Nchi Mwanachama zifanyie kazi mapendekezo hayo na kuyatolea taarifa katika vikao husika.

Mheshimiwa Spika, mambo ni mengi sana ya kuhoji ili kupatiwa ufafanuzi, lakini Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini suala kubwa kama hili lingepatiwa muda wa kutosha ili kuangaliwa na kupitiwa na Bunge zima kwa mtindo wa kifungu kwa kifungu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, tunasubiri maelezo na majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**Taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya SADC ya Fedha na Uwekezaji**
**Kama Ilivyowasilishwa Mezani**

**MAONI YA MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU KURIDHIA AZIMIO LA KURIDHIA ITIFAKI YA SADC KUHUSU FEDHA NA UWEKEZAJI (*SADC PROTOCOL ON FINANCE AND INVESTMENT*)**

*(Inatolewa chini ya Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Bunge, 2013)*

**Mheshimiwa Spika,** Mnamo tarehe 18 agosti, 2006, Wakuu wa Nchi kumi na nne wa *Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika*, yaani *Southern African Development Community* ('SADC') walitia saini *Itifaki ya SADC Kuhusu Fedha na Uwekezaji*, yaani *SADC Protocol on Finance and Investment*, katika Mji wa Maseru, Lesotho. Rais Jakaya Kikwete alitia saini Itifaki hiyo kwa niaba ya Tanzania. Wengine waliotia saini Itifaki hiyo ni Wakuu wa Nchi za Angola, Botswana, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Falme ya Lesotho, Madagascar, Malawi, Mauritius, Msumbiji, Namibia, Afrika Kusini, Falme ya Swaziland, Zambia na Zimbabwe.

**Mheshimiwa Spika,** Itifaki ya SADC ina jumla ya ibara 32 na Nyongeza kumi na moja zinazohusu masuala ya Ushirikiano kuhusu Uwekezaji; Mafungamano ya Kifedha (Macro-Economic Convergence); Ushirikiano katika Kodi na masuala yahusuyo kodi; Ushirikiano na Uratibu wa Sera za Udhibiti wa Fedha za Kigeni, na Usajihishaji wa mifumo ya kisheria na kiutendaji. Nyongeza nyingine zinahusu Ushirikiano juu ya Mifumo ya Malipo; Ushirikiano katika Eneo la Teknolojia za Habari na Mawasiliano miongoni mwa Benki Kuu; Ushirikiano na Uratibu katika Eneo la Udhibiti na Usimamizi wa Masuala ya Kibenki; Ushirikiano juu ya Taasisi za Fedha za Maendeleo; Ushirikiano juu ya Taasisi na Huduma za Kifedha Zisizo za Kibenki, na Ushirikiano juu ya Masoko ya Hisa katika SADC.

**Mheshimiwa Spika,** Lengo kuu la Itifaki ya SADC linatajwa katika ibara ya 2(1) ya Itifaki kuwa ni "*… kukuza usajihishaji wa sera za fedha na uwekezaji za Nchi Wanachama ili kuziweka sambamba na malengo ya SADC na kuhakikisha kwamba mabadiliko katika sera za fedha na uwekezaji za Nchi Mwanachama mmoja hazilazimu marekebisho yasiyotakikana katika Nchi Wanachama wengine*." Kwa mujibu wa ibara ya 2(2), lengo kuu hilo litatekelezwa kwa kupitia ushirikiano wa kikanda, ushirikiano na uratibu katika sekta za fedha na uwekezaji kwa lengo la kupanua sekta za uzalishaji na kukuza biashara katika Kanda ili kupata maendeleo na ukuaji endelevu wa kiuchumi na kufuta umaskini kwa kujenga ushirikiano katika maeneo yote yaliyotajwa katika Nyongeza za Itifaki.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 29 ya Itifaki ya SADC inalazimu kwamba Itifaki itaanza kutumika siku thelathini baada ya kuridhiwa na angalau theluthi mbili ya Nchi Wanachama. Kwa kigezo kilichowekwa na Sekretarieti ya SADC, theluthi mbili ni sawa na Nchi Wanachama kumi. Hadi sasa, kwa kadri ya taarifa ilizo nazo Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu, ni Nchi Wanachama tisa tu ndizo zilizoridhia Itifaki hiyo. Hivyo basi, kwa sababu hiyo, Itifaki ya SADC haijaanza kutumika, miaka takriban nane baada ya kusainiwa na Wakuu wa Nchi Wanachama.

**Mheshimiwa Spika,** Itifaki ya SADC ni mkataba wa kimataifa. Kwa sababu hiyo, ibara ya 28 ya Itifaki imeweka masharti ya kuridhiwa na Nchi Wanachama "… kufuatana na kanuni zao za kikatiba." Kwa Tanzania, kama zilivyo nchi nyingine zinazofuata mila na desturi za kisheria na kikatiba na Jumuiya ya Madola, mikataba yote ya kimataifa inayosainiwa na nchi yetu inatakiwa kuridhiwa na Bunge lako tukufu. Ndio maana ibara ya 63(3)(e) ya *Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977*, imelipa Bunge lako tukufu mamlaka ya "*kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa.*"

Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inaamini kwamba msimamo huu wa Katiba yetu ulikuwa unajulikana kabla na baada ya Rais Kikwete kusaini Itifaki ya SADC mwaka 2006. Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inaamini kwamba Serikali hii ya CCM ilikwisha kufanya maandalizi yote yaliyokuwa yanahitajika kabla ya kusaini Itifaki hii. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inaamini kwamba Serikali hii ya CCM ilisaini Itifaki hii kwa nia ya kuitekeleza na sio kwa lengo la kujionyesha tu kuwa na sisi ni sehemu ya SADC. Kwa sababu hizi, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inataka kujua sabab zilizoifanya Serikali hii ya CCM kuchukua miaka nane kuleta mkataba huu wa kimataifa mbele ya Bunge lako tukufu kwa ajili ya kupata ridhaa ya Bunge ili uanze kutumika. Vile vile, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inataka Serikali hii ya CCM ilieleze Bunge lako tukufu kama kuna athari zozote za kiuchumi au kijamii zilizotokana na nchi yetu kuchelewa kuridhia Itifaki hii.

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania imetiliana saini mikataba ya uwekezaji (*bilateral investment treaties – BITs*) na baadhi ya Nchi Wanachama wa Itifaki ya SADC. Kwa kadri ya taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inazo, Tanzania ina mikataba ya aina hiyo na Malawi ambao ulisainiwa tarehe 30 Juni, 2003; Zimbabwe ambao ulisainiwa tarehe 3 Julai, 2003, na Afrika Kusini ambao ulisainiwa tarehe22 Septemba, 2005. Aidha, Tanzania ina mkataba wa uwekezaji na Mauritius uliosainiwa tarehe 4 Mei, 2009.

Kwa taarifa zilizotolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo, yaani United Nations Conference on Trade and Development (UNCTAD), hadi kufikia tarehe 1 Juni, 2013, mikataba hiyo kati ya Tanzania na baadhi ya Nchi Wanachama wa Itifaki ya SADC ilikuwa haijaanza kutumika. Kwa sababu hiyo, Kambi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inataka kujua sababu zilizoifanya Serikali hii ya CCM kutokuileta mikataba hiyo katika Bunge lako tukufu ili ipate ridhaa na kupata nguvu za kisheria.

Pia, Serikali hii ya CCM ilieleze Bunge lako tukufu ni lini inatarajia kuileta mikataba hiyo Bungeni kwa ajili ya kupata ridhaa kwa mujibu wa Katiba yetu. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inataka kauli rasmi ya Serikali hii ya CCM kulikuwa na sababu gani za kusaini Itifaki ya SADC ilhali ilikwishasaini mikataba mingine ya uwezekaji na baadhi ya Nchi Wanachama wa Itifaki hiyo. Vile vile, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inaitaka Serikali hii ya CCM ieleze faida za kuendelea kuwa na utitiri huu wa mikataba ya kimataifa ya uwekezaji ambayo hata hivyo haitekelezwi kwa sababu haijapata ridhaa ya Bunge lako tukufu kama inavyotakiwa na Katiba yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 3 ya Itifaki ya SADC inawataka Nchi Wanachama kuratibu taratibu zao za uwekezaji na kushirikiana kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji katika Kanda kama ilivyofafanuliwa katika Nyongeza ya 1 ya Itifaki hiyo. Hata hivyo, kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu, masharti hayo ya Itifaki yanapingana na matakwa ya ibara ya 2 ya Nyongeza ya 1 ya Itifaki yanayoitaka kila Nchi Mwanachama "… *kuhamasisha uwekezaji katika eneo lake na kuruhusu vitega uchumi hivyo kufuatana na sheria na kanuni zake.*"

Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu, wakati ibara ya 3 ya Itifaki inaweka masharti ya ushirikiano baina ya Nchi Wanachama, ibara ya 2 Nyongeza ya 1 inaruhusu ushindani miongoni mwao. Mkanganyiko huu ni hatari kwa maslahi ya nchi yetu. Hii ni kwa sababu raslimali nyingi zilizomo kwenye Nchi Wanachama wa Itifaki hii zinafanana kwa kiasi kikubwa. Ukiacha Afrika Kusini ambayo ina uchumi wa kiviwanda, Nchi nyingine Wanachama zinategemea kilimo au madini au rasilimali nyingine za asili kwa ajili ya uchumi wao.

Katika mazingira hayo, kuruhusu ushindani, kama inavyopendekezwa na ibara ya 2 ya Nyongeza ya 1, kuna hatari ya kuzifanya nchi hizo kulegeza masharti yao ya uwekezaji kwa kiwango ambacho kitakuwa na madhara makubwa kwa maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii ya nchi hizo. Hatari hii inaitwa *'the race to the bottom'*, yaani ushindani wa kujichimbia kaburi kati ya nchi na nchi zinazoshindana kuvutia uwekezaji mkubwa katika sekta za uchumi zinazofanana.

**Aidha, Mheshimiwa Spika,** thamani ya ushirikiano chini ya ibara ya 3 ya Itifaki imefifishwa zaidi na masharti ya ibara ya 7 ya Nyongeza ya 1 ambayo inaweka wazi kwamba masharti hayo ya ushirikiano *"… hayatahusu manufaa, nafuu au misamaha inayoweza kutokea kutokana na mkataba wa uwekezaji baina ya nchi na nchi … ambayo Nchi Mwanachama inashiriki au inaweza kushiriki."* Kwa lugha nyepesi, Tanzania haifungwi na masharti ya ushirikiano na Nchi nyingine Wanachama chini ya ibara ya 3 ya Itifaki ya SADC kwa manufaa, nafuu au misamaha ambayo tumewapa wawekezaji kutoka Afrika Kusini, Malawi, Mauritius na Zimbabwe kwa mujibu wa mikataba ya uwekezaji baina ya Tanzania na nchi hizo.

Kama ni hivyo, Nchi nyingine Wanachama wa Itifaki ambazo hazitanufaika manufaa, nafuu au misamaha hiyo zitakuwa na maslahi ya kuendelea kuheshimu matakwa ya Itifaki kuhusu ushirikiano kama Itifaki yenyewe inaruhusu ubaguzi dhidi yao kutoka kwa Nchi Wanachama wengine? Ibara ya 2 ya Nyongeza ya 1 inaweza ikawa ndio kichocheo kikubwa cha Nchi Wanachama kuacha kushirikiana na hivyo kusambaratisha dhana nzima ya ushirikiano ambayo ndio msingi wa Itifaki hii.

**Mheshimiwa Spika,** kuna mkanganyiko mwingine uliotengenezwa na ibara ya 6 ya Nyongeza ya 1 inayohusu wawekezaji wa nchi zisizokuwa wanachama wa Itifaki ya SADC. Kwa mujibu wa ibara ya 6(1) ya Nyongeza hiyo, vitega uchumi na wawekezaji watakuwa na fursa na haki sawa katika eneo la Nchi Mwanachama. Aidha, kwa mujibu wa ibara ya 6(2), fursa na haki hizo hazitakuwa pungufu kuliko fursa na haki walizopewa wawekezaji wa nchi zisizokuwa wanachama wa Itifaki.

Hata hivyo, usawa huo umefutwa na matakwa ya ibara ya 7(1) ya Nyongeza hiyo hiyo inayoruhusu Nchi Wanachama, kufuatana na sheria zao za ndani, *"kutoa upendeleo kwa vitega uchumi na wawekezaji ili kufikia malengo ya maendeleo ya taifa."* Kwa kujua kwamba masharti haya yamefuta dhana ya fursa na haki sawa chini ya ibara ya 6, ibara ya 7(2) inazitaka Nchi Wanachama *"baadae kusajihi sera na sheria zao za ndani katika moyo wa kutokubaguana kama ulivyowekwa kwenye ibara ya 6."* Hakuna muda wowote uliowekwa kwa Nchi Wanachama kufanya hivyo. Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inaitaka Serikali hii ya CCM kutoa kauli rasmi mbele ya Bunge lako tukufu kama tafsiri hii ya ibara ya 6 na ya 7 ni sahihi au la.

**Mheshimiwa Spika,** Mfumo wa utatuzi wa migogoro ni eneo lingine la Itifaki ya SADC ambalo linahitaji kutazamwa upya. Chini ya ibara ya 27 ya Nyongeza ya 1, *"Nchi Wanachama zitahakikisha kwamba wawekezaji wana haki ya kufungua mashtaka katika mahakama,*

*mabaraza ya kimahakama au ya kiutendaji na mamlaka nyingine zinazohusika chini ya sheria za Nchi Mwenyeji ili kupata haki kwa malalamiko yao kuhusu jambo lolote linalohusu uwekezaji wowote...."* Kwa mujibu wa kifungu hiki, endapo mwekezaji atanyimwa haki ya kwenda katika mahakama ya Nchi Mwanachama, hiyo itakuwa ni ukiukwaji wa Itifaki hii.

Hata hivyo, ibara ya 28 ndio yenye umuhimu mkubwa zaidi. Ibara hiyo inawaruhusu wawekezaji kufungua mashtaka kwenye vyombo vya upatanishi wa uwekezaji vya kimataifa pale ambapo mgogoro unaohusu wajibu wa Nchi Mwanachama kuhusu uwekezaji uliokubaliwa umeshindikana kusuluhishwa kwa maridhiano na baada ya kumaliza nafuu zote za ndani ya nchi, na baada ya kupita miezi sita tangu malalamiko yalipowasilishwa rasmi. Kuhusu upatanishi wa nje ambako mwekezaji anaweza kupeleka malalmiko yake, ibara ya 28(2) inatamka kwamba mwekezaji na Nchi Mwanachama wanaweza kukubaliana kupeleka mgogoro wao katika Baraza la SADC au *Kituo cha Kimataifa cha Utatuzi wa Migogoro ya Uwekezaji*, yaani *International Centre for the Settlement of Investment Disputes (ICSID)*, moja ya taasisi nyingi za Benki ya Dunia.

Migogoro inaweza pia kufunguliwa kwa mujibu wa kanuni za upatanishi za *Tume ya Umoja wa Mataifa juu ya Sheria za Kimataifa za Biashara*, yaani *United Nations Commission on International Trade Law (UNCITRAL) Rules*. Endapo hakuna makubaliano katika kipindi cha miezi mitatu, ibara ya 28(3) inaelekeza kwamba mgogoro husika utapelekwa kwenye upatanishi kwa mujibu wa Kanuni za UNCITRAL.

**Mheshimiwa Spika,** Wakati utaratibu wa kutatua migogoro ya uwekezaji chini ya ICSID na UNCITRAL umetumiwa sana na wawekezaji kuishtaki Serikali ya nchi yetu au taasisi na mashirika yake na, kwa sababu hiyo, unafahamika na kupendelewa na wawekezaji, utaratibu wa kutumia SADC Tribunal hautekelezeki. Hii ni kwa sababu Baraza hilo limevunjwa kufuatia uamuzi wake katika kesi ya *Mike Campbell (Pty) Ltd. & Wenzake dhidi Jamhuri ya Zimbabwe*. Kesi hiyo ilifunguliwa chini ya Mkataba wa SADC (badala ya Itifaki) na kikundi cha makampuni na watu binafsi waliokuwa wanamiliki mashamba makubwa nchini Zimbabwe kupinga kunyang'anywa mashamba yao na Serikali ya Zimbabwe. Walalamikaji, wengi wao wakiwa wakulima wa kizungu, walituhumu kwamba unyang'anyi wa mashamba yao kwa nguvu ulikuwa batili kwa sababu walizuiliwa kwenda mahakamani; na kwamba walibaguliwa kwa misingi ya rangi yao.

Katika hukumu yake ya tarehe 28 Novemba, 2008, Baraza la SADC lilikubali madai ya walalamikaji. Baraza liliridhika kwamba walalamikaji *"walinyang'anywa ardhi zao bila kupatiwa fursa ya kwenda mahakamani na kusikilizwa kwa haki, ambavyo ni vigezo muhimu vya utawala wa sheria, na ... kwa hiyo, Mlalamikiwa amekiuka ibara ya 4(c) ya Mkataba (wa SADC)."* Baraza liliamua kwamba, kwa vile sheria ya urekebu wa milki za ardhi ilikuwa inawaathiri wakulima wa kizungu peke yao na kwa hiyo ilikuwa ya kibaguzi, Serikali ya Zimbabwe ilikuwa *"imewabagua walalamikaji kwa msingi wa rangi na kwa hiyo imekiuka wajibu wake chini ya ibara ya 6(2) ya Mkataba."* Aidha, Baraza hilo liliamua kwamba walalamikaji walikuwa na haki ya kulipwa 'fidia ya haki', ijapokuwa kiwango cha fidia hiyo hakikutamkwa kwenye hukumu hiyo.

Serikali ya Zimbabwe ilipinga uamuzi huo vikali na suala hili hatimaye liliingizwa kwenye duru za kidiplomasia. Hivyo basi, mnamo tarehe 20 Mei, 2011, katika kikao cha dharura cha Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC, Nchi Wanachama wa SADC ziliamua kutoteua wajumbe wapya wa Baraza la SADC na kuzuia Baraza hilo kusikiliza kesi mpya dhidi ya Nchi Wanachama. Kwa maneno mengine, Mahakama ya SADC inayotajwa katika ibara ya 28(2)(a) ya Nyongeza ya 1 haipo tena. Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inaitaka Serikali hii ya CCM kutoa kauli rasmi mbele ya Bunge lako tukufu kama inakubaliana na maelezo haya.

**Mheshimiwa Spika,** Itifaki hii ya fedha na uwekezaji kwa kuwa ilikwisha sainiwa na wakuu wa nchi mwanachama, lakini kuna mapungufu ambayo ni dhahiri, kwani hakuna kifungu kinachoeleza pindi nchi mwanachama itakayoshindwa kutekeleza yale yaliyokubaliwa ni adhabu au hatua au vikwazo gani vinatakiwa kuchukuliwa dhidi ya nchi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 12 inazitaka nchi mwanachama kutumia raslimali zake kiuendelevu wakati huo wakitilia maanani utunzaji wa mazingira. Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge, kwa mikataba ambayo tayari imesainiwa kama ile Rai Group ya kufyeka misitu ya Mufindi bila kupanda miti na hivyo kutokuwepo kwa uendelevu wa misitu hiyo. Je, baada ya kuridhiwa kwa itifaki hii mikataba ya awali itatenguliwa kuwekwa kifungu cha *"matumizi endelevu"?*

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 19 katika kiambatanisho cha 1 kuhusu ushirikiano kwenye uwekezaji, Itifaki inasema kuwa kila nchi mwanachama lazima ijisajihishe na malengo ya kuendeleza kanda na kuwa kanda ya uwekezaji ya SADC ambayo pamoja na mambo mengine inaendeleza mkakati wa mtangamano(intergration) wa kanda kwa kuhuhisha sera na sheria ili ziendane kwa nchi zote mwanachama. Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge ni kwa vipi Ibara hiyo inazifanya nchi mwanachama kuwajibika, kwani Itifaki hii aionyeshe mpango mkakati wa utekelezaji na ni muda gani nchi mwanachama zinatakiwa ziwe zimetekeleza matakwa ya kifungu hiki. ***"Accountability for performance is weakened by the fact that the FIP does not contain any timelines. Consequently, there is no deadline for implementation".***

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, haionyesha popote kuwa makubaliano ya itifaki yanayotakiwa kutekelezwa na wanachama pale mwanachama akishindwa kuyatekeleza ni hatua gani zitachukuliwa. Badala yake matakwa ya itifaki yameachwa kwa mawaziri wa fedha wa nchi mwanachama kutekeleza matwaka au makubaliano ya itifaki. ***"The open-ended nature of the FIP means Member States are never in clear breach of their commitments".***

**Mheshimiwa Spika,** Ni kwamba utekelezaji wa itifaki umejikita zaidi kwa secretariat ya SADC badala ya nchi mwanachama, "***The SADC Secretariat has no political mandate to achieve Member State reforms. It is at the Member State level that implementation must take place***" na hivyo kupelekea kutokuwepo kwa msukumo wa uwajibikaji kwa nchi mwanachama kutekeleza na uhitaji wa kutoa taarifa kwa kipindi kilichokubaliwa juu ya utekelezwaji wa vifungu vya itifaki. Kasoro hizi zinatoa mwanya kwa nchi mwanachama kushindwa kutekeleza matakwa ya itifaki hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa tathmini iliyofanywa na Mwakilishi *Mkaazi wa Taasisi ya Kijerumani ya FES ofisi ya Botswana Dr. Marc Meinardus* kwenye andiko lake la "Deepening Integration in SADC" kuhusu ***lengo la pili kifungu kidogo cha c*** kwenye Itifaki hii. Ameuliza ni kwa vipi ushirikiano kwenye masuala ya kodi utaongeza utengamano wa SADC na kusaidia nchi mwanachama kufikia malengo ya kukua kwa uchumi na mwisho kuwepo kwa maendeleo endelevu kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Ni kweli kwamba kodi inakwenda sambamba na matumizi ya nchi ambayo ni hutoaji wa huduma za msingi kwa wananchi. Hivyo ushirikiano wa kodi pia inatakiwa uende sambamba na utoaji wa huduma za msingi au matumizi ya nchi kwa ujumla. Kwa hiyo basi ni kwanini kusiwepo utaratibu wa ushirikiano kwenye matumizi kwa nchi mwanachama? Hii ni kutokana na ukweli kwamba tumekuwa na kilio cha muda mrefu kuhusu jinsi gani matumizi ya nchi yasivyoendana na mipango tunayoipanga na hivyo kupelekea kuwa hapa tulipo. Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mhe Waziri atoe ufafanuzi zaidi kwenye lengo hili.

**Mheshimiwa Spika, *Lengo la pili la Itifaki kifungu kidogo cha j*** kinachohusu ushirikiano kwenye asasi za fedha zilizo rasmi lakini zisizo za kibenki(formal financial sector), ni ukweli kwamba nchi mwanachama zimekuwa zikiendeshwa kwa asasi za fedha ambazo ni rasmi na zisizo rasmi (formal and informal financial sector). Hivyo basi kutokutambua kazi nzuri inayofanywa na taasisi zisizo rasmi ambazo kwa kiasi kikubwa ndio watoaji wa mikopo kwa wafanyabiashara wadogo wadogo na wale wenye kipato kidogo.

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ndogo ya fedha na sekta ya fedha isiyo rasmi (micro-finance and informal sector) ndio chanzo kikuu cha fedha za mitaji kwa wafanyabiashara wadogo wadogo na biashara ndogo ndogo na za kati kwa nchi mwanachama wa SADC.

**Mheshimiwa Spika,** Hivyo basi, mkakati wowote ambao hauitambua sekta ya fedha isiyo rasmi siyo mkakati makini kwa ajili ya kuleta maendeleo endelevu kwa wananchi wan chi mwanachama. Kwa hili tunamtaka Mheshimiwa Waziri atupe maelezo ya ziada. Aidha, kutokuwepo kwa ushawishi wa zera za kuzilazimisha benki zinazofanyakazi katika ukanda wa SADC kuweka sera za kuwakopesha sekta isiyo rasmi na kukopesha uanzishwaji wa viwanda vidogo na vya kati ni dhahiri hakutakuwepo na maendeleo endelevu ya kupambana na umaskini na kukuza ajira kwa nchi wanachama.

**Mheshimiwa Spika,** Inaweza kuonekana kwamba hoja hizi ni mambo ya ndani kwa nchi mwanachama, lakini kwakuwa lengo la Itifaki hii ni kuleta maendeleo endelevu kwa nchi mwanachama, hivyo ili SADC ionyeshe kuwa ni chombo makini na chenye dhamira ya kweli ni muhimu kuzitaka nchi mwanachama zifanyie kazi mapendekezo hayo na kuyatolea taarifa katika vikao.

**Mheshimiwa Spika**, Mambo ni mengi sana ya kuhoji ili kupatiwa ufafanuzi, lakini Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini suala kubwa kama hili lingepatiwa muda wa kutosha ili kuangaliwa na kupitiwa na Bunge zima kwa mtindo wa kifungu kwa kifungu.
Hivyo basi,

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani naomba kuwasilisha.

**…………………………………………..**
**Christina Mughwai Lissu (Mb)**
**Kny. Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya**
**Upinzani-Wizara ya Fedha**
**06.06.2014**

**SPIKA:** Ahsante. Kwa Ofisi ya Spika, hii ni itifaki mojawapo ambayo ilikuja kwa muda mrefu, tulishindwa kuijadili Bunge lililopita kwa sababu tulikosa muda kama ile ya *Institute* ya Tengeru, ndiyo maana Kamati iliposema tuahirishe mpaka Jumatatu tukakataa kwa sababu ni *document* waliyokuwa nayo kwa muda mrefu kwa maana ya Ofisi yangu.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge nitawataja ambao wataendelea kuchangia hapa, kwanza kabisa yuko Mheshimiwa Dkt. Terezya Huvisa atafuatiwa na Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, naomba kwanza hao waanze halafu tutaendelea.

**MHE. DKT. TEREZYA P. L. HUVISA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu ili kuweza kuridhia Itifaki hii ya *SADC* ya Fedha na

Uwekezaji. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na kuweza kusimama mbele ya Bunge hili kusema hayo machache ambayo nitachangia. Moja kwa moja niseme naunga…

**SPIKA:** Mheshimiwa dakika 10 yeyote atakayepewa muda, akimaliza dakika 10 ndiyo hasa muda wenyewe, naomba uendelee Mheshimiwa.

**MHE. DKT. TEREZYA P. L. HUVISA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Niseme moja kwa moja naunga mkono Azimio la Kuridhia Itifaki ya *SADC* ya Fedha na Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivi; nasema hivyo kwa sababu katika ulimwengu wa sasa hivi wa sayansi na teknolojia na uwekezaji mkubwa wa kidunia, ni lazima nchi maskini za Afrika zikae pamoja na kuweka ushirikiano katika mambo ya uchumi ili kupambana na *Regional Blocks* nyingine kwa mfano *European Union, United States of America, United Arab Emirates* na Kanda nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukisema tujitenge, ni kama tunakuwa kisiwa katika ulimwengu, hivyo hatutaweza kupambana kiuchumi na Mabepari wakubwa. Kwa hiyo, kuridhia itifaki hii ni suala la msingi sana kwa sababu Tanzania haiwezi kujitenga na kuimarisha uchumi peke yake.

Mheshimiwa Spika, vile vile faida zinazopatikana na kujiunga au kuridhia itifaki hii ina maana kwamba Serikali ya Tanzania au nchi ya Tanzania itaweza kulinda maslahi ya wananchi wake katika uwekezaji na mambo ya kiuchumi kwa ujumla. Pia tutaweza kukuza uwekezaji baina ya wananchi washiriki na kushirikiana na nchi nyingine za Afrika, lakini tutaweza kukuza mitaji yetu na utaalam hasa teknolojia kati ya nchi washiriki.

Mheshimiwa Spika, vile vile tutaweza kutekeleza miradi mikubwa ambayo inatupasa kushirikiana na nchi zingine jirani, pia tutaweza kudhibiti biashara ya fedha haramu yaani *Anti Money Laundering* na nyingine tutaweza kuondoa ushuru wa forodha na vikwazo vingine vya kiuchumi ili kuweza kukuza uchumi wetu, vile vile tutaweza kushirikiana katika mambo mbalimbali yanayohusu sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuridhia itifaki hii, ningependa Mheshimiwa Waziri aweze kutupa ufafanuzi kwa sababu tumesharidhia itifaki nyingi tu kwa mfano, katika mambo ya *environment* tumeridhia itifaki za *AMSEN* tumeridhia itifaki za *UNEP,* lakini mpaka sasa hivi Serikali imeshindwa kutoa michango katika itifaki mbalimbali tulizoridhia. Sasa ni kwa namna gani Serikali itaweza kutuhakikishia kwamba, tukiridhia hii itifaki hatutakuwa nyuma kutoa michango na kuwa wanachama halali bila ya kupata kigugumizi, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, tunaposoma itifaki hii tunaona faida zake ni kubwa na ni nzuri zinapendeza, lakini tukienda kwa wananchi wa chini kabisa kwa mfano wakulima wangu wa mahindi kule Songea wana tatizo kubwa sana la masoko ya mahindi, wana tatizo kubwa sana kufanya biashara na hata suala zima la uwekezaji hawalijui, ndiyo maana inatia hofu wananchi wanabaki kuwa watazamaji tu.

Sasa je, ni namna gani Serikali itatuhakikishia kwamba, wananchi wa Tanzania hawatakuwa watazamaji tukiridhia itifaki hii? Kwa mfano, tunajua kabisa soko la mahindi halipatikani na wananchi wangu unakuta kwamba msimu unaanza wa mavuno, lakini bado wana mahindi kwenye maghala, ni namna gani hizi itifaki zitawasaidia kuona hilo soko.

Mheshimiwa Spika, tuna Azimio hilo la *East Africa Community* lakini mpaka sasa hivi tunajua nchi kama *South Sudan* wanahitaji chakula Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi wanahitaji chakula, lakini wananchi wa chini wale hawajui ni namna gani wanaweza kufika

kwenye masoko hayo ili waweze kufaidika na haya masoko ambao tunayazungumzia kila siku. Hivyo, hata tukiridhia hiyo itifaki ya *SADC* bado masoko yanaweza kupatikana ya Zambia, Seychelles, Madagascar ni namna gani wananchi wa chini kabisa maskini wanaoweza kutumia masoko haya.

Mheshimiwa Spika, kama wananchi wataweza kuelewa namna ya kuwekeza na kupata masoko ya nchi jirani nadhani hofu hii itakuwa imeondoka, lakini tukibaki kuwa watazamaji bado tatizo litakuwa ni kubwa na wananchi wataona kama vile wanakuja kuporwa ardhi yao badala wao wenyewe kuwa ni *active* kuweza kutumia fursa hizi. Kwa hiyo, nadhani mambo haya mawili yakiwekwa vizuri, elimu ikitolewa ya kutosha kwa wananchi, kwanza waelewe maana ya Itifaki, lakini pia waelewe hizi fursa zinazoweza kupatikana katika nchi jirani ili waweze kulinda biashara zao na hivyo kukuza uchumi katika ngazi ya familia, ngazi ya Mikoa, lakini pia katika ngazi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, haya machache nikiweza kupata ufafanuzi, mimi binafsi nitakuwa nimetosheka na naunga mkono Azimio hili kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami nisiwe mbali sana na Dkt. Huvisa kwa sababu lengo kubwa la *protocals* hizi ni Ustawi wa Jamii, kwa hiyo, tunataka kuwa na mashirikiano na nchi zinazotuzunguka, lengo kubwa ni kuboresha maisha ya wananchi wetu kutoka katika hali ya uduni na yawe bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini napata tabu kidogo kwamba ndani ya muda mfupi kama huu kuweza kusoma na kupitia pamoja na kwamba tuliletewa hapo nyuma, lakini hatupati elimu ya kutosha, siamini kama Wabunge wengi humu ndani tunaelewa tunaridhia nini na kwa faida zipi. Napata taabu hata mimi mwenyewe kwamba wananchi wangu pale Iringa Mjini naweza nikawa na ujasiri wa kuwaelezea kwamba hii *protocal* tunayoisaini inawasaidia nini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, najaribu kui-*challenge* Serikali kwamba mambo muhimu kama haya ni vizuri sisi kama wawakilishi wa wananchi tunatakiwa tupate uelewa wa kutosha tuangalie faida zake na hasara zake, halafu tunapokuja kuridhia hapa tuwe tunajua kitu tunachokifanya.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake hizi *protocals* nyingi zinapokuja hapa zinakuwa ni kama zimamoto, tunaanza kuridhia wakati hatuna hata uelewa wa kutosha kwenda kuwaambia wananchi tunaowawakilisha, lakini kikubwa kingine ambacho nataka kusema, ni kwamba hata hii *protocal* yenyewe imechukua miaka minane kama Serikali yenyewe iko *serious* miaka minane toka Mheshimiwa Rais ame–*sign* kule Lesotho.

Mheshimiwa Spika, muda wote huu umepita, kama Kambi Rasmi ya Upinzani tumeuliza maswali haya hamjatuletea, hamjatuambia, hakuna *awareness* kwenye *public* ni kwa nini muda wote huu umepita hamjatuletea. Inaonekana hili suala siyo la muhimu na haya mambo ndiyo yanaleta tabu katika mahusiano na nchi zetu jirani.

Mheshimiwa Spika, tuna mashirikiano mengine na Afrika ya Mashariki na Watanzania tunaonekana kama hatuelewi tunataka nini. Nataka kujua kama Taifa ni wapi ambapo tunaona tunafaidi zaidi ambapo kuna fursa kama Taifa tukishirikiana na Afrika Mashariki au na *SADC* ambapo tutumbukize nguvu za kutosha kwa sababu wenzetu kwa mfano, Kenya wanataka kukimbia zaidi tunakuwa tunarudi nyuma, tunaona kama wanataka kutuibia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda *SADC* tunaonekana nako tunakwenda taratibu, sasa tunataka tushirikiane na nani kwa sababu hata hii mikataba ya *SADC* haiji kwa haraka.

Tukienda Kenya nako wanatulaumu, tunaonekana wenzetu wanapotaka kukimbia sisi tunatembea, mimi nina wasiwasi tunaonekana kama vile tuna wasiwasi kama wanataka kutuibia. Sasa sijui ni *competence* ambayo hatuna, kwamba tunaogopa kama wata-*grab,* kwa nini tusiwe weledi pale tunapoona wanataka ku-*take advantage* sisi tu-*take advantage* kwao ni kwa nini hatuweki mazingira ya kujiandaa kwa sababu hatueleweki. Huku *SADC* hatuendi vizuri, huku *East Africa* hautuendi vizuri tuko katikati huku nako tunalaumiwa.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema kingine labda hilo nitapata jibu kutoka kwako ni kwa nini toka tumeingia Bungeni hapa labda mimi kwa sababu ya ugeni, hiki ni kipindi changu cha kwanza, tuliwachagua Wabunge wa *SADC*, tuliwachagua Wabunge wa *East Africa*, tumewachagua Wabunge wa *CPA,* lakini hatupati mrejesho.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, haya mambo ya *SADC,* toka wamekwenda kwenye Bunge la *SADC,* hatujawahi kusikia wametuambia nini toka wamekwenda huko Bungeni na hili ndilo Bunge lao na sisi ndiyo wanaotuwakilisha; hawajawahi kufika hapa na kutuambia wanafanya nini, Tanzania tujiandae vipi, kuna fursa zipi na tuchangamkie vipi, hawajawahi kutuambia.

Mheshimiwa Spika, tumewachagua hawa wa Afrika ya Mashariki, wanakuja siku zote tunapoandika bajeti hapa, hawatuambii kuna changamoto gani kwenye Bunge lao, wanafanya nini. Kwa hiyo, hizi *protocal* zinakuja hawa wawakilishi wetu wanakuwa kama hawana maana na hawa wanaokwenda nje na wenyewe wakienda kwenye Bunge la *Commonwealth,* nao wanakwenda, wakirudi hapa hatusikii wanasema na sisi ndiyo tuliowachagua, sasa kuwachagua kwao sisi tunafaidi nini na wanatuambia nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda hilo litakuwa ni la kwako, itabidi unifafanulie kidogo nione faida za hawa Wabunge kwa sababu kwa kweli tunaona wanasafiri tu, labda tupige kura ya kutokuwa na imani nao, maana hawaleti mrejesho kwa Wabunge hapa ili tuone faida za wao kwenda huko nje. Kwa hiyo, ombi langu kwako, naomba Serikali hii iseme ni fursa zipi ambazo ni makini kwa sababu nimesema haya maingiliano na nchi jirani ni kwa ajili ya ustawi wa jamii, kama haileti ustawi wa jamii hatuna haja nayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mtuambie ni namna gani tunajiweka na tunapata fursa wapi kati ya *SADC* na *East Africa* ili tuweka nguvu huko, kwa sababu kila wakati tunajihami, ulimwengu wa sasa unakwenda miaka mingi, ni miaka nane imepita hatujaridhia, kama ina maslahi ni kwa nini tumekaa hatujaridhia?

Mheshimiwa Spika, lingine ili tuwe na mahusiano mazuri na nchi zingine viongozi wa Serikali mmekuwa mkizungumza sana kuhusu amani na uzalendo katika jambo hili ambalo ni zuri. *Internaly* mnazungumza sana, lakini kumekuwa na kauli za viongozi wakubwa kuhusu mahusiano ya Kimataifa ambazo ni kauli *irresponsible*. Naomba Serikali hili iliangalie kwa sababu tumesikia Mawaziri hapa kuanzia Waziri wa Mambo ya Ndani, amekuja Waziri wa Nishati na Madini na Mkuu wa Nje na nini, mmezungumza kauli zingine ambazo zinahatarisha usalama wetu na watu wengine, uchumi hauwezi kuwa imara, uchumi wetu hatuwezi tukajitenga kama mwenzangu alivyosema kwamba nadhani Mheshimiwa Mkapa alishawahi kusema lugha moja zamani na nakubaliana alisema

"*Tanzania inauhitaji ulimwengu kuliko ulimwengu unavyoihitaji Tanzania*''

Kwa hiyo, mahusiano na nchi zingine ni ya muhimu sana tunapozungumzia suala la amani ndani ya nchi, lakini vile vile amani na nchi zinazotuzunguka ni jambo la msingi sana kwa sababu vita ikizuka hapa mtu wa kwanza kugombana naye ni jirani yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni jambo la muhimu na la msingi kuhakikisha majirani zetu tunaweka mikakati ya msingi ya kutokugombana na kutoa kauli ambazo zinaweza kuhatarisha amani, kwa sababu tusipokuwa na amani na watu wanaotuzunguka hatuwezi kufanya biashara, tutagombana. Hatuwezi kuuza kwa sababu biashara inaanza na jirani zetu na amani inaanza na jirani zetu pamoja na kuwa na amani katika nchi yetu, lakini jambo la muhimu vile vile kauli za vitisho na ubabe za kuwatishia watu wengine sidhani kama zina busara za kulijenga Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba haya mambo ambayo tumezungumza Kambi ya Upinzani na hasa hilo la mwisho ambalo Kiongozi wa Kambi ya Upinzani amezungumza kwamba, ni vizuri vifungu hivi tungevipitia vizuri kwa pamoja kama Wabunge ili ninapoondoka hapa na kwenda Iringa wakazi wangu wa Mwaningo, Kihesa, Kilolo, Isakalilo na Kibwabwa, kwenda kule wanapouza michicha yao na wanataka kujua hizi fursa wanazipataje, niwe na ujasiri kama Mbunge wao na kama mwakilishi lakini nachelea kusema kuwa ninapoondoka hapa sielewi nahitaji kupata darasa zaidi, lakini ningefundishwa na hawa wenzangu ingenisaidia ili wananchi wa Kitanzania pale Miomboni waseme Mbunge anatuambia kuwa kuna fursa wafanye kazi za maana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Amenitaka nimjibu na ninamjibu hapohapo bila ya kuchelewa. Ni kweli anavyosema Mheshimiwa Mchungaji Msigwa kwamba tunao Wabunge wa *SADC*, tunao Wabunge katika *Commonweath Parliamentary Association,* wale wa *East Africa,* tunawachagua lakini wako wenyewe kule, tunao wawakilishi wetu hapa wa *Interparliamentary Union* sasa mbona mrejesho hatupati Bungeni?

Kwa mfumo na utaratibu wetu sisi, hawa wote wanaripoti kwenye Kamati yetu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ndiko wako wanakopeleka. Sasa wale ndiyo wanaotakiwa kuingiza humu ndani, siyo kila mtu anaweza kuingiza humu ndani. Kwa hiyo, katika taarifa zao za mwaka ni moja ya vitu ambavyo wenyewe wanatakiwa kufanya mrejesho. Kwa sababu ukichukua kama *SADC Parliamentary Forum,* kwanza hiyo *is even very bad,* hata kama tunapitisha *SADC Protocal* hapa, SADC *parliamentary Forum* siyo Bunge, ni mfumo wa kukutana na kuongea, ndiyo maana sasa hivi wanaomba na wao wawe Bunge kama lilivyo la East Africa, bado viongozi hawa wa *Summit* hawajakubali.

Waheshimiwa Wabunge, Bunge la *SADC* kwa kweli ni kama *club* ya Wabunge katika nchi za *SADC,* hata hizi *protocal* hizi haziendi kwao, sana sana wanaweza kuhimiza tu kwamba nchi fulani hamjaridhia mkataba huu mtasemezana pale kwa sababu sekretarieti ya *SADC-PF* wako *active* kwamba watakwenda kwenye *SADC Secretariet* kule na mnajua Makao Makuu ya *SADC-PF* ni Windhoek, Makao Makuu ya *SADC Secretariet* ni Botswana.

Kwa hiyo, ni watu wako mbali kwa kiwango kikubwa sana na hii *SADC Parliamentary Forum*. Kwa hiyo *challenge factor* iliyopo ni wenyewe kuwa na Bunge kama lilivyo hili la *East Africa,* hayo ni mambo ambayo yamezungumzwa kwa muda mrefu ingawa *Treaty* yenyewe ilikuwa inasema tunaanza kama *Forum* kwa kuendelea kuwa Bunge baadaye, kwa hiyo inaonekana kuna katatizo.

*Common Wealth Parliamentary Association* tuna *branch* hapa na mnawachagua watu hapa na Mwenyekiti wetu ni Mheshimiwa Zungu na inakutana na inatakiwa i-*feedback* humu. Tuna *branch* lakini pia *branch* ina mahusiano na *branches* zingine, kama mwaka huu sasa nchi

ya Tanzania sisi tutakuwa ni wenyeji wa *Commonwealth Parliamentary Association Africa Region* na mimi ndiyo Rais wake sasa.

Hiyo afadhali ni *active* kwa sababu inajadili mambo ya nchi mbalimbali, maana ni *association* na siyo Bunge tu, mnaweza kujadili mambo ya kisiasa na uchumi kama mnapenda na vitu kama hivyo, lakini pia tuna Commonw*ealth Parliamentary Association International,* hiyo nayo ina *leadership* yake kuanzia kwenye *branches* na watu wengine huko. Kwa hiyo, hiyo kidogo inajitegemea ni kama *association* kama ilivyo. Sasa hivi tuna tatizo na hiyo pia kwa sababu ukisoma Katiba ya *Commonweath Parliamentary Association* inasema ni *Charity Organization* iliyoanzishwa na Sheria ya Uingereza na Wales.

Sasa hapo sisi Waafrika tunasema, hapana, tunachangiaje *Charity Organization* ya Uingereza, sisi tunapata faida gani. Kwa hiyo, kuna mgogoro huu unaoendelea sasa hivi; nchi za Kiafrika zimekuja juu kwamba ama tukubali ni *Diplomatic Relationship* na sio *association* kama ilivyo sasa, tena charity. Kwa hiyo, kuna mgogoro sasa hivi kati ya *Members* wa Commonwealth pamoja na Makao Makuu yake ambayo yako Uingereza kama ilivyo ilianzishwa kwa Sheria za Wales na England, sasa sisi tunasema hapana hatuwezi kwenda huko.

Ya *East Africa* ndiyo hao wanaleta mrejesho, kila wakimaliza Bunge lao wanaleta mrejesho hapa, lakini bado tunafikiria pia waiangalie vizuri kwa sababu wakishapitisha Sheria kule na sisi tunafanyaje, si ndiyo Sheria tayari? Labda wangetuletea kupitia Kamati yetu hii kama ni Muswada, kama tunavyofanya *Public Hearing* kwa Miswada yetu mingine, basi na wao wangekuwa kabla hawajaingia kutunga Sheria kule, wakatupa *Public Hearing* tukawapa maoni yetu, lakini ilivyo sasa ni kwamba wakishamaliza wanatuletea sisi na sisi tunakuwa hatuna meno juu yake, ni taarifa tu.

*IPU* hiyo ni *Inter Parliamentary Union* ni Mabunge yote, ya aina zote duniani na mara nyingi pale ndiyo upo mchezo mkubwa kabisa wa kisiasa, lakini wao wanakuwa na bidii mara tumeletewa *workshops* hapa za mambo ya vifo vya akinamama, haki za wanawake na nini, zinaletwa katika nchi mbalimbali kwa sababu zinakuwa na programu yao ya kazi huwa tunapewa hizi semina nyingi tunazofanyia hapa.

Waheshimiwa Wabunge, lakini mambo haya yote yanatakiwa yapitie kwenye Kamati yetu ya Mambo ya Nje pamoja na Uhusiano wa Kimataifa, wao ndiyo walete humu ndani, huo ndiyo utaratibu.

Naendelea nilisema namwita Mheshimiwa Augustino Masele, atafuata Mheshimiwa Leticia Nyerere!

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ili niweze kuchangia katika hii *protocal* muhimu ambayo iko mbele yetu leo. Itakumbukwa dhahiri kwamba nchi yetu imekuwa ni Taifa muhimu sana katika ukombozi wa Mataifa ya Kusini mwa Afrika, wakati ule Mataifa haya yakiitwa nchi zilizo mstari wa mbele na Tanzania ndiyo ilikuwa ni nchi kiongozi na Katibu Mkuu wa nchi hizo wakati huo alikuwa Hashim Mbita Mtanzania. Tumetoka huko, tukaanza ushirikiano wa kimahusiano, lakini baadaye ikaonekana kuwa sasa ni vyema tushirikiane zaidi katika masuala ya kiuchumi, kiulinzi na kiusalama.

Mheshimiwa Spika, kuja kwa Itifaki hii naona kwamba ni mwendelezo tu wa harakati za Ukombozi wa Mwafrika. Lengo letu ni kuwa na Bara lililoungana, nchi moja, Bunge moja na Serikali moja huko mbele ya safari. Kwa hiyo, nchi ya Tanzania kutokana na historia yake imekuwa ni nchi ambayo imejitoa mhanga katika uwepo wa amani katika Bara letu la Afrika na kwa maana hiyo niko pamoja na Mheshimiwa Waziri aliyeleta hoja hii hapa ndani ili kusudi sisi

Wabunge ambao ni wawakilishi wa wananchi tuweze kuridhia jambo hili ambalo limeletwa na Serikali yetu. Kwa maana hiyo, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Itifaki hii ya Fedha na Uwekezaji ni Itifaki muhimu ambayo iko katika ule mkakati wa maendeleo wa *SADC* ambao lengo lake hakika ni kuja kuwa na sarafu moja ya nchi hizi za *SADC*. Kwa maana hiyo, kama hatutaweza kuiridhia Itifaki hii ina maana lengo ambalo Wakuu wetu wa Nchi ambao waliridhia huko Lesotho halitaweza kutimia kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alivyowasilisha hapa kwa kusema kwamba, Mpango Mkakati wa *The* SADC *Region Indicative Strategic Development Plan* unatoa dira ya mtengamano wa Nchi Wanachama wa SADC ambao ni soko huru la biashara, Umoja wa Forodha, soko la pamoja ifikapo mwaka 2015 na umoja wa Sera za Fedha *(Monitory Union)* mwaka 2016 na hatimaye kuwa na sarafu moja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mwelekeo wetu ni huko na kwa maana hiyo inaonekana kwamba, tulikuwa tunachelewa leo ni mwaka 2014, ina maana kwamba tuna miaka minne tu ili kufikia hilo lengo la kuwa na sarafu moja katika eneo la *SADC*. Kwa mara nyingine tu niseme kwamba iko haja ya kuridhia Itifaki hii

Mheshimiwa Spika, tunakoendelea huko mbele ni dhahiri kwamba, nchi zetu zitatakiwa kuendelea kushirikiana, maana kuna mambo mengi ambayo yanajitokeza, kwa mfano, majanga na mambo mengine kama magonjwa, ukame na uharibifu wa mazingira. Haya ni mambo ambayo yanahitaji ushirikiano na kwa maana hiyo, tusiposimama kwa pamoja itafika mahali tunaweza kujikuta kwamba tunashindwa kufanikiwa katika baadhi ya mambo kutokana tu na kwamba ule msemo usemao kwamba Umoja ni Nguvu na Utengano ni udhaifu, kwa hiyo, ni vyema tukaendelea kuwa na umoja zaidi na mshikamano zaidi ili tuweze kupiga hatua za kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe wazi kwamba nchi zetu hizi za Kusini mwa Afrika ni nchi tajiri, pamoja na kwamba tunazungukwa na umaskini lakini tu matajiri; tuna rasilimali za kutosha katika sekta za utalii, ardhi, rasilimali watu, madini na kila kitu, lakini sasa kuna baadhi ya mambo kwa mfano, Miundombinu bado ni dhaifu na kwa maana hiyo tunahitajika tushirikiane kwa pamoja uwekezaji katika viwanda na mambo mengine, tukifanya kwa pamoja ninaamini kwamba tunaweza kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, njia mojawapo ya kufikia malengo haya ni pamoja na kufanya wepesi katika haya mambo ya msingi yanayokuwa yameamuliwa na Wakuu wetu wa Nchi za Jumuiya za Nchi za Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, nisiwe na maneno mengi ya kusema zaidi ya hapo, zaidi niseme naunga mkono hoja, Bunge letu Tukufu liweze kuridhia Itifaki hii. Ahsante kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Leticia Nyerere, atafuatiwa na Mheshimiwa Losesia Bukwimba!

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na namshukuru Mwenyezi Mungu kwa Afya.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia *SADC Protocol on Finance and Investment* kama ifuatavyo:-

Pamoja na kwamba Serikali imechelewesha ili Azimio, lakini angalau wamelileta leo na kwa kuzingatia umuhimu wa Azimio hili kwa kweli tunashukuru kwamba Serikali imetuletea ili

Azimio ili tuweze kulijadili. Nasema Azimio hili ni muhimu sana kwa nchi yetu ambayo inaendelea, ni muhimu sana kwa nchi ambayo ni sehemu ya *SADC,* hatuwezi kukwepa kuwa kwenye *SADC*, hatuwezi kukwepa kwenda na uchumi wa *SADC* kwa hali yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, kuna sababu nyingi za kiuchumi ambazo tutanufaika nazo na vilevile kuna hata haya maamuzi ya kifedha ambayo tutanufaika nayo kama Taifa na vilevile hata sababu za kisiasa pia nazo tutanufaika nazo. Ukiangalia eneo la *SADC* tuna *political stability*, kwa hiyo, hii nayo inachangia katika kuendeleza uchumi katika Mataifa yetu. Ukikosa *political stability* huwezi ukawa na *economic stability* hata siku moja. Kwa hiyo, tunamshukuru Mwenyezi Mungu Serikali imetuletea Azimio hili twende sambamba na wenzetu.

Mheshimiwa Spika, ukizingatia kwamba unaposhindwa kwenda sambamba na wenzio, iwe *SADC, East Africa,* utaachwa nyuma, *you will be left* behind na ukiachwa nyuma kuja kuwafikia wenzio itakuchukua muda mrefu sana na matokeo yake huwezi kuwafikia. Kwa hiyo, ndiyo maana rai yangu kwa Serikali ni kwamba tujifunze sasa kama Serikali ama Taifa, tuanze sasa kuwa na maamuzi ya haraka, tunatoa maamuzi ya haraka badala ya kuchukua muda mrefu kabla hatujaamua.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wanaleta Maazimio, *Treaties,* nchi nyingi zinaridhia au zinatoa maamuzi, lakini mara nyingi sisi Watanzania tunakuwa wa mwisho. Tuna tatizo gani Watanzania? Tunatakiwa sasa tulifanyie kazi hilo. Je, tatizo letu kubwa ni rasilimali watu, tumewaandaaje Watanzania wetu hata *participation* yao SADC, tumewaandaa vipi? Kuridhia Azimio ni kuridhia Azimio, kuridhia Azimio *its one thing* lakini ku-*participate it's another thing*.

Mheshimiwa Spika, tuna-*participate* vipi ili tuweze kunufaika na hili Azimio letu ambalo tunakwenda kuridhia leo. Je, tuna Watendaji ambao ni makini, *competent* ambao watatuwakilisha vizuri pia ni wazalendo. Au tunapeleka watu wababaishaji ambao watakuja kutu-*let down* na kutuaibisha kama Taifa. Tumewaandaa vipi rasilimali yetu watu na tunaendelea na maandalizi gani, ili tuweze kunufaika na hii *protocol*.

Mheshimiwa Spika, Watanzania tumekuwa na tatizo na hili tatizo chimbuko lake sijui ni nini. Namshukuru Mwenyezi Mungu sisi ndiyo tulikuwa chipukizi wa kwanza kwenda Urusi na tumejifunza uzalendo na tulitamani uzalendo kwa sababu wenzetu walijifunza uzalendo na walituonesha uzalendo wao.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kila nchi ambayo nimekwenda nikaishi nimekuta wana uzalendo wa hali juu, piga ua hawezi akakana uzalendo wake, Utaifa wake kwa sababu yoyote ile. Cha kusikitisha Watanzania wengi hatujitambui, hatujielewi, hatuji-*position*, hatujui, *we don't know where we belong to.* Tupo tu tunabishania siasa, tunasahau hata kama tunatakiwa kuwa na Tanzania kama nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tunasahau kama unapokosa nchi ya kujivunia wewe ni maskini. Tunasahau kwamba jambo la kwanza la kujivunia ni nchi yako na bendera yako. Tumebaki tunabishania ujinga badala ya kubishania kujenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii *protocol* ni muhimu katika Taifa letu. Hii *protocol* tuipiganie na uzalendo wetu wa Tanzania kama haja ni elimu ya uraia iliyokosekana, Serikali itafute ufumbuzi, Watanzania wajifunze uzalendo, wapewe elimu ya uzalendo, hawaelewi, hawajijui, hawajitambui, ukisoma mitandao mnaona vituko. Mtu anajadili vitu vya kijinga, havimhusu kabisa, anataka fulani mume wake ni nani, anataka kujua Fulani mke wake ni nani, itakusaidia nini? *(Makofi)*

Watanzania tuamke sasa hivi, tufanye mambo ya kujenga Taifa letu, Taifa letu ni maskini, hakuna jinsi tunatakiwa sisi wenyewe tuwekeze nguvu katika Taifa letu na ndiyo tunaweza kujivuna kama Watanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Naona umeoteshwa na Roho Mtakatifu kabisa. Mheshimiwa Ahsante sana umesema vizuri kabisa. Mheshimiwa Lolesia Bukwimba atafuatiwa na Mheshimiwa Sabreena Sungura.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia.

Kwanza kabisa nipende kuipongeza timu yetu ya Mkoa wa Geita kwa kushinda na kuingia daraja la kwanza katika ligi iliyofanyika pale Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuunga mkono hoja kabisa kwamba Itifaki ya Fedha na Uwekezaji ni muhimu sana kwetu sisi Watanzania. Tukizingatia kwamba umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu na kwa sababu hiyo nilikuwa nikiangalia manufaa ambayo tutayapata sisi Watanzania kutokana na kuridhia itifaki hii. Nimeona kwamba ni mambo muhimu sana na ya msingi. Kwa mfano, imezungumzia habari ya kuongeza mitaji, masoko, ni mambo ambayo ni muhimu sana kwetu sisi kama Watanzania.

Mheshimiwa Spika, itifaki hii tutakapoiridhia nina uhakika kwamba hata wananchi wetu wataweza kunufaika zaidi hasa katika upande wa masoko kwa sababu itifaki imezungumzia habari ya kuongeza mitaji na hasa katika masoko ambayo kwa muda mrefu sana tumekuwa tukitegemea soko la dunia katika kuuza mazao yetu, mfano, pamba na mazao mengine.

Mheshimiwa Spika, katika Mikoa yetu kama ya Kanda ya Ziwa tunalima pamba kwa wingi na mara nyingi kila mwaka tunapata changamoto kubwa sana ya masoko na kila mwaka bei zinashuka kwa sababu soko la dunia bei zinakuwa zimeshuka. Sasa tukiridhia itifaki hii kama jinsi ambavyo tumesema kwamba tutaanzisha masoko muhimu kabisa pengine hata bidhaa zetu kama pamba tunaweza kupata masoko ya uhakika na pia tutakapoweza kuanzisha viwanda mbalimbali nina uhakika kwamba wananchi wetu wataweza kunufaika sana na itifaki hii.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, niombe kabisa nchi yetu na Serikali kwa ujumla tuangalie namna sisi Watanzania tukavyoweza kuanzisha viwanda mbalimbali kwa ajili ya kupitia mtangamano huu wa *SADC*. Vile vile nikiangalia nchi yetu tuna madini mbalimbali ambayo sasa kupitia madini haya vitu vya thamani ambavyo vinapatikana katika nchi yetu, tukiweza kuanzisha viwanda mbalimbali pengine kupitia huu umoja wa *SADC,* nina uhakika kwamba wananchi wetu wanaweza kunufaika zaidi kuliko hapo awali na kwa jinsi hiyo sasa, naunga mkono hoja kabisa kwamba nchi yetu tuweze kujiunga na itifaki hii, tuweze kupitisha haya maazimio ili wananchi wa Tanzania tuweze kunufaika na umoja huu.

Mheshimiwa Spika, vile vile nilikuwa nikisoma yale manufaa ambayo wamezungumzia hapo, kwa mfano, tumezungumza kwamba tutakuwa na sarafu moja. Sasa napata maswali kidogo kwamba nchi yetu ya Tanzania tumejiunga pia na *East Africa* na *East Africa* pia tuna mpango wa kuwa na sarafu moja. Sasa vilevile tuwe na sarafu moja ya *SADC*. Sasa nina maswali kidogo hapo kwamba sasa sisi Watanzania tutakuwa na sarafu ngapi? Tutakuwa na sarafu ya *East Africa, SADC* na Tanzania.

Kwa hiyo, hilo labda ni vyema tukaliangalia tukaona namna ambavyo tutaweza kufanya, sisi kama Watanzania tuwe na sarafu ya aina gani. Tuangalie manufaa kwamba wapi ambapo pengine tukiwa na sarafu ya aina gani itakuwa na uzito zaidi na nguvu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile umoja huu wa *SADC* ni muhimu sana kwa sababu unatupa nafasi sisi kama Watanzania pia kupata ajira mbalimbali. Kwa hiyo, niombe pia Serikali iwaandae watu wetu wa Tanzania kuweza kuwa na uwezo mkubwa hata ajira mbalimbali zinapotokea tuwe na uhakika wa kuzipata sisi kama Watanzania.

Mheshimiwa Spika, tuna vijana wetu wengi ambao wanahitaji ajira, kwa hiyo, ni uhakika kwamba pengine kupitia umoja huu itifaki hii tutakapoisaini itarahisisha zaidi Watanzania wengi kuweza kupata ajira nje ya nchi na hatimaye basi tukaweza kupata ajira za kutosha hata sisi Watanzania tukaweza kunufaika.

Mheshimiwa Spika, vile vile tunazo rasilimali nyingi sana hapa Tanzania wenzangu wameshazungumza, kwa mfano, katika upande wa uwekezaji tuna gesi asilia, tuna madini, maji ya Ziwa Victoria na Maziwa mbalimbali, lakini vilevile tuna bandari ambayo kupitia rasilimali hizi, nina uhakika kwamba kwa nchi za *SADC* tukiweza kuridhia hii itifaki tutaweza sisi Watanzania kunufaika zaidi kwa sababu tutakuwa na nguvu zaidi, kupitia rasilimali zetu, watu wengine pia wataweza kupata masoko na kuweza kufanya biashara pamoja na wao vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja kabisa kuhusu kuridhia itifaki hii ili Watanzania wengi waweze kunufaika na wananchi wa Geita waweze kunufaika na itifaki hii maana tutaweza kuanzisha Viwanda vya Madini na Viwanda mbalimbali vya Pamba. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Sabreena Sungura atafuatiwa na Mheshimiwa Rita Kabati.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia katika protocol ya *SADC*.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia, napenda nitoe salamu za pole kwa Mbunge mwenzangu Zitto Zuberi Kabwe kwa kuondokewa na mama yake na napenda kusema kwamba Mwenyezi Mungu ampe moyo wa subira na tupo pamoja katika kipindi hiki kigumu cha kuondokewa na mpendwa wetu na Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo nina machache kuhusiana na suala hili la *Protocol*. Suala la kwanza ukiangalia *protocol* hii inaonekana kwamba imepitishwa mwaka 2006, lakini uridhiaji wake umekuja kufanyika mwaka 2014. Nataka tu kujua mbona tumechelewa sana kuja kuridhia? Kwa kipindi chote hicho cha miaka karibu nane, tulikuwa tuna maandalizi gani kama Taifa. Ningependa kupata majibu kutokana na suala hili.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, nataka kuongelea kuhusu *objective* za hii *protocol*. Kwa sababu ukiangalia kwenye ibara ya 19 kuna suala zima la *harmonization* na kwa ku-*quote* ibara hii inasema:

*"State party shall pursue harmonization with objective of developing the region into SADC investment zone which among others include harmonization of investment regimes*

*including policies, laws and practices, in accordance with the best practice within the overall strategy towards regional integration."*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ibara hii unaona kabisa kwamba kama nchi tulitakiwa tujiandae na Sera na Sheria mbalimbali kuhusiana na suala hili. Sasa kipindi hicho cha miaka nane yote, tumejiwekaje? Tanzania tumekuwa na changamoto kubwa hata ukiangalia *protocol* ambazo tumesaini za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sheria nyingi bado hazijafanyiwa *harmonization,* Sera nyingi bado hazijafanyiwa *harmonization*! Sasa tunaji-*engage* vipi katika suala lingine jipya na wakati bado tuna mzigo mkubwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, labda na hapo ningependa Serikali ije itoe ufafanuzi kwamba tutaharakishaje mambo haya huku ukizingatia tuna utitiri wa Sheria ambazo zinahitaji kuletwa hapa na kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kuongelea, ilikuwa sasa ni *implementation* ya hii *protocol* vs *protocol* za Afrika Mashariki kwa sababu ukiangalia kwenye hizi *protocol* zote mbili kuna masuala ya *investment and finance* hususan kwenye *common currency*. Kwenye *SADC* wanayo *common currency,* lakini katika Jumuiya ya Afrika Mashariki wanayo *common currency* pia. Sasa sisi kama nchi tunasimama upande upi?

Mheshimiwa Spika, hapa napo naona kuna matatizo lakini labda Serikali ina majibu zaidi kwa sababu *protocol* hiyo wengine tumeipata asubuhi. Kwa hiyo, tumeshindwa kujua majibu ya masuala yote haya. Kwa hiyo, wenzetu upande wa Serikali labda waje watuambie tunatekelezaje vitu hivi viwili ambavyo vinashabihiana kwa kiasi kubwa.

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine ambalo nataka kuongelea ilikuwa ni kuhusu Wawekezaji wa ndani. Ukisoma katika *protocol* hii kwenye *section five and six* wametuambia kwamba kuwe na *fair and equitable treatment* kwa Wawekezaji ambao ni wanachama wa Jumuiya ya *SADC*.

Mheshimiwa Spika, sasa katika mazingira hayo tunasema tuwe tuna *fair and equitable treatment* kwa wanachama wetu, lakini tuna tofauti kubwa sana za kijamii na kiuchumi Tanzania tuna-*compete* vipi katika *protocol* kama hii au hatuoni kama inawezekana tukawa tunawatengenezea wenzetu wa jumuiya hii hususan wa *South Africa* na nchi nyingine ambazo zipo mbele yetu kimaendeleo, mfano, ni kama vile sisi tutakuwa juu na sisi chini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni lazima tujiandae katika mazingira haya yaani hii *section five* na *six* tuiangalie japo kwenye *section seven* wameweka *option* kwamba kuna *preferential treatment* kwa wazawa, lakini ukiangalia Sheria zetu za ndani hazimwangalii mzawa na hata ukiangalia katika suala zima la sasa hivi la uwekezaji wa gesi, wazawa wa ndani wanaitwa madalali na kupewa majina mengi.

Mheshimiwa Spika, sasa tunapopitisha *protocols* kama hizi, mzawa wa Tanzania analindwa kwenye kipengele gani kwenye *protocol* kama hii. Kwa hiyo, si kwamba siungi mkono hii *protocol,* naunga lakini hizi tahadhari lazima Serikali izitolee majibu au kama tutakubali hizi *protocol* kuzisaini, basi kuwe kuna kipengele *reservation* kwamba tunakubaliana na *protocol,* lakini eneo moja, mbili, tatu na kadhalika hapana! hilo bado tunafikiria. Ni vyema tufanye hivyo kwa faida ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine la mwisho, lilikuwa ni suala la *article* 17(27) ambayo inaelezea *access to codes and tribunals*. *Article* hiyo inasema:

*"State parties shall ensure that investors have the right of access to the codes, judicial and administrative tribunals and other authorities competent under the law of the host state for readiness of their grievances in relation of any matter concerning any investment including Judicial review of measure relating to expropriation or Nationalization and determination of compensation in the event of expropriation or nationalization"*.

Mheshimiwa Spika, *article* hii inaonesha *enforcement of laws of investors right*. Sasa tunaposema kwamba *article* inamwezesha Mwekezaji kama anakuja kuwekeza hapa na pale ambapo atapata *effect* basi kama nchi iweze kum-*compensate*. Ukiangalia katika maeneo mbalimbali katika nchi yetu kwa mfano Tarime, tumeona mara nyingi kwenye *TV* wazawa kwa sababu Sheria za nchi haziwajali, wamekuwa mara nyingi wakivamia mgodi, wakiondoka na mchanga, dhahabu, lakini kwa kipengele hiki sasa kama nchi inatakiwa ilipe madeni.

Mheshimiwa Spika, sasa tunapoingia kwenye *protocol* kama hii, hatujawawezesha wazawa labda tuwaambie nyinyi mtachimba hapa, Wawekezaji wataweka hapa. Labda kama ni ardhi, basi ninyi mtabakia na kipande hiki, Wawekezaji watawekeza labda kwenye kilimo kipande hiki. Tunaona kabisa hili suala litatuletea shida na kila siku kama nchi tutakuwa tuna *compensate* hizi *investiment companies* kwa sababu tu hatukuwajali wazawa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Rita Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Mnyaa.

**MHE. RITA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia mada iliyoko mezani kwetu.

Kwanza kabisa nianze na kuwapongeza Mawaziri wote na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa kutuletea Azimio la Kuridhia Itifaki ya *SADC* ya Fedha na Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Muswada huu umechelewa sana kuletwa hapa Bungeni, lakini pengine kitendo cha kuchelewesha huu Muswada inawezekana kabisa mmeweza kufanya utafiti wa kutosha kuhakikisha kwamba nchi yetu haingii kwenye jambo ambalo halitakuwa na manufaa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, imenifanya na mimi niunge asilimia mia moja Muswada huu ambao umeleta hapa mezani. Nchi za *SADC* ni nchi ambazo zinashirikiana katika nyanja nyingi zikiwemo za kiuchumi. Kwa hiyo, kuleta itifaki hii zitakuwa zinashirikiana katika sera, kanuni, Sheria za uwekezaji na uchumi. Kwa hiyo, kwa kuridhia, Mkataba huu ni imani yangu sasa wananchi wetu wakulima, wafugaji na hata wafanyabiashara wanaweza kupata mitaji mikubwa katika masoko katika nchi hizi.

Mheshimiwa Spika, Tanzania pia tumekuwa na tatizo kubwa sana la masoko kama ambavyo wenzangu wengi wamesema. Kwa hiyo, nina imani kabisa tukaporidhia Azimio hili pengine sasa wakulima watakuwa wamepata masoko makubwa, tumeona hata katika Mikoa yetu tumekuwa tunafanya kilimo kikubwa, lakini kinakuwa hakina tija sana kwa wakulima kwa sababu tunakosa masoko.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano wakulima wa nyanya, vitunguu na mahindi tumekuwa na mahindi mengi ambayo huwa yanawaozea wakulima, wanakuwa hawapati faida zozote. Kwa hiyo, kwa kuridhia mkataba huu, pengine kungeweza kusaidia sana tija katika kilimo cha nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, vilevile labda ningepata ufafanuzi kwamba Tanzania tumekuwa na washirika katika nyanja mbalimbali katika nchi mbalimbali, lakini nchi yetu imeonesha kuwa wazito kidogo kwa baadhi ya mambo ya mipango ya washirika. Je, sasa tumejipangaje tutakapoingia kwenye hii itifaki? Tumejipangeje kuhakikisha kwamba tumekuwa wepesi kushiriki katika mambo ambayo tumekuwa tukushirikiana na nchi nyingine ili isiweze kuleta athari sana katika nchi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nami naunga mkono Azimio hili kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Eng. Mohamed Mnyaa, Mbunge wa *SADC Parliamentary Forum* na kule ni Mwenyekiti wa Kamati ya Biashara na mengineyo, na baadaye nitamwita Mheshimiwa James Mbatia.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia Itifaki hii, na pia nakushukuru na kukupongeza wewe kwa kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya mambo kwa sababu wapo wengi ambao hawajui kwamba hizi *SADC* zipo mbili; ile ya *Secretariat* na ile *SADC-PF*. Kwa hiyo, nakushukuru kwa kutoa ufafanuzi huo.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba Serikali haitutendei haki Waheshimiwa Wabunge, kwamba Bunge hakuna siri ambayo Serikali itaficha na Bunge lisijue. Bunge linatakiwa lijue na Bunge ndiyo lenye mamlaka ya kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika mambo haya ya hizi Itifaki *(protocol)* ni kwamba tulipopitisha ile *protocol* ya sayansi, teknolojia na ubunifu, tulilalamika na kuomba Serikali ijitahidi watuletee *protocol* hizi mapema ili mtu aweze kusoma na kujua tunaridhia nini. Kwa bahati mbaya hilo halijafanyika na shuhuda mwenyewe Spika leo umeona *Protocol* yenyewe imesambazwa wakati tayari imeshawasilishwa hapa, mtu aweze kupata nafasi asome halafu ajue anachangia nini. Huu ni udhaifu ambao siyo mzuri. Hata Kamati yenyewe inayohusika walipata jana!

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo tunachukua nafasi hii kukuomba tena au kuliomba Bunge hili kwamba hizi *protocols* ziletwe mapema ili angalau kabla ya kuridhia tuweze kujua tunaridhia nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninasema hivyo kwa sababu hizi *protocols* zina mambo mengi sana na kwamba katika *protocol* 35 ninazozijua mimi, leo angalau tukiridhia hii, Tanzania bado itabakia na *protocol* 10 ambazo hatujaridhia. Tulisaini, lakini hatujaridhia. Kwa maana hiyo, leo niseme mapema kwamba na mimi naunga mkono turidhie Azimio hili na kwa maana hiyo itatusaidia. Lakini tukitizama hii hali ya hizi *protocol,* ni kitu gani kinatokea kwamba ule muda unakuwa ni mrefu kabla ya kuletwa hapa? Zipo nyingine muda ni mfupi sana. Hata hivyo, baada ya kuridhia, zile faida tunazozipata, mbona kidogo hazieleweki?

Mheshimiwa Spika, Itifaki hii ya fedha na uwekezaji ni kwamba mpaka sasa hivi ni nchi tisa tu zilizosaini na kuridhia; nchi tano bado. Hii ni ya mwaka 2006, leo mwaka 2014 ni mwaka wa nane Tanzania sasa ndiyo tunataka kuridhia itifaki hii ya fedha na uwekezaji.

Zipo nchi ambazo ziliridhia hii itifaki ya mwaka 2006, mara tu 2007 wakaridhia. Maana yake inaonekana labda kwa zile nchi zilizoridhia mwaka mmoja tu baada ya kusainiwa, inaonekana walikuwa na faida kwao kubwa, Tanzania ilikuwa hatujaona labda faida, sasa ndiyo tunaiona leo. Lakini huko nyuma tulishawahi kuridhia itifaki ya biashara *(Protocol on Trade)* na kuna uhusiano mkubwa wa hii tunayotaka kuridhia leo na ile ya *trade* ya mwaka 1996.

Tanzania tulisaini na kuridhia, tulisaini tarehe 24/8/1996 na tukaridhia mwaka 1997 tu Julai 3. Kwa maana hiyo ile kwetu sisi ilikuwa na faida, tulikaa kipindi cha mwaka mmoja tu! Itifaki nyingine zinakaa miaka mingi mno.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo basi, ikiwa ile tuliyoridhia mwaka 1997 haipishani hata kidogo au ina mambo machache sana, lakini ni sawasawa na hii ya *finance* na *investment*. Kwa maana hiyo, tungeomba Wizara hii ya Fedha, Mheshimiwa Waziri atufafanulie zile faida toka tuliporidhia ile mwaka 1997, na tumepata faida gani ya *protocol on trade* na leo baada ya miaka minane tunataka kuridhia hii ya biashara, fedha na uwekezaji?

Mheshimiwa Spika, uwekezaji na *trade,* ndiyo mambo hayo hayo! Ni lugha tu! Uwekezaji ni kuweka, lakini *trade* ni hiyo hiyo upande mmoja. Kwa hiyo, tunataka tujue sasa kama nchi tujitathmini, tumefaidika vipi na *protocol* ya biashara, na hivi leo tukisharidhia ambapo umeshatueleza hapa faida ni nyingi ambazo tunazikubali, lakini kuna tofauti gani kubwa na vipi tulivyofaidika kule?

Mheshimiwa Spika, katika haya mambo ya kuridhia pia zipo itifaki ambazo kuna nchi hazikuridhia na unaweza ukashangaa nchi zilizoridhia tumefaidika vipi? Kuna Itifaki ya Uvuvi *(Protocol on Fisheries),* utashangaa nchi kama Madagascar na Seychelles hawakusaini na hawakuridhia mpaka hivi leo na hiyo ni ya mwaka 2001, lakini Tanzania tuliridhia toka mwaka 2003. Lakini je, tumefaidika vipi na Itifaki hii ya Uvuvi. Kama Sekta ya Wizara ya Biashara ambayo inasimamia uchumi wa nchi hii, ni lazima tuelewe tumefaidika vipi?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni jambo la aibu, pamoja na kwamba tuna ukanda mkubwa wa bahari, lakini utakuta leo Tanzania kunaingizwa samaki ambao wanaitwa vibua *frozen* ambao wanakaa kwenye makontena huko miezi mitatu hadi sita, wanafika mpaka hapa katika Mahoteli ya Dodoma wapo, hawana ladha yoyote! Je, hii ndiyo faida ya kuridhia ile Itifaki ya Uvuvi au vipi?

Mheshimiwa Spika, samaki hawa wanatoka Japan, India na nchi nyingine huko! Lakini bahari tuliyopakana na nchi hizi zilizoridhia za karibu, hatuoni ule ushirikiano wetu wa kiuvuvi, tunafaidika vipi? Au ndiyo ile meli kusaidiwa kukamatwa, inayoitwa kwa jina maarufu Meli ya Magufuli iliyokamatwa na Wa-*South Africa* wakatusaidia? Ndiyo kufaidika kwenyewe kule! Hebu Mheshimiwa Waziri atueleze, kwa Sekta hii ya Uchumi, hapa tunafaidika namna gani?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kengele imeshalia kuna hili suala la kwamba kwa mujibu wa itifaki hii mwisho wake ni kuwa na sarafu moja. Huku Afrika Mashariki pia ipo ya kuwa na sarafu moja. Sasa hapa pana mgongano.

Halafu *negotiation* katika *World Trade* tunaambiwa ni lazima twende kwa utatu hivi sasa na huo utatu umezungumziwa haufiki mwisho.

Utatu wenyewe ni kwamba ili ku-*harmonize* haya mambo baina ya *group* hili la *SADC* na *East Africa,* maana yake Tanzania ukija *SADC* tupo kwa sababu zetu za kimsingi za toka ukombozi, ukija *East Africa* tupo, kwa sababu zetu vilevile, sasa inakuwa taabu! Huku kuna *monetary Union* (sarafu moja) na huku kuwe na sarafu moja, ni jambo ambalo utakuta haliwezekani, isipokuwa ile *tripartite* ifanye kazi.

*(Hapa muda wa mzungumzaji uliisha)*

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, naomba dakika moja nimalizie.

**SPIKA:** Tunafanyaje hivyo sisi?

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, ni hoja muhimu.

**SPIKA:** Sisi hatufanyi hivyo. Mheshimiwa Mbatia!

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Haya.

**SPIKA:** Wewe kaa, umeshaeleweka.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia.
Mheshimiwa Spika, Itifaki iliyopo mbele yetu ya Fedha na Uwekezaji katika nchi za *SADC* ni Itifaki muhimu sana. Nimeanza kusema kwamba ni Itifaki muhimu sana kwa sababu duniani leo tukiangalia lengo la nane la milenia, dunia imekuwa kijiji, na ni lazima tukubali kufikiri kwa mapana, *let us think globally,* dunia inakwendaje na sisi hapa kwetu tukoje?

Mheshimiwa Spika, wakati wa uhuru ukisoma nchi zote hizi 14, karibu zote hawa ni *baby* wa Tanzania. Wakati wa Mwalimu Nyerere tulisema kwamba binadamu wote ni ndugu zangu na Afrika ni moja. Ni Watoto wa Tanzania hawa.

Mheshimiwa Spika, sisi Tanzania kwenye Itifaki hii ya uwekezaji tunachukua nafasi gani ya kuongoza hawa wengine kama tulivyo na asili ya kuongoza katika Bara letu la Afrika? Tusibaki kwenye kulalamika tu, intelijensia ya uchumi ndani ya nchi yetu inatumia namna gani nafasi hii kuhakikisha Tanzania kama Taifa tunafaidika na sehemu gani? Tufanyaje Watanzania hawa wakawekeza katika nchi hizi? Tunatoa fursa gani kwa hao wengine kuja hapa na kuondokana na dhana katika akili zetu kwamba wawekezaji hawa ni wezi? *Let us think big*! Ni lazima tukubali kufikiri kwa mapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaona uchumi wetu unasuasua, tupo kwenye bajeti hapa, ni vuta nikuvute. Lakini sasa nafasi hizi ambazo zinapatikana, tangu mwaka 2006 wamesaini Wakuu hawa, kwanini sisi mpaka leo hii hatukuchukua jukumu la faida ambazo zitatokana na uwekezaji huu tukawa ndiyo Kiongozi katika *SADC* na wanaiheshimu sana Tanzania. Kwa sababu badala ya sisi kutumia fursa hizi, tunakuwa ni walalamikaji au kuona wenzetu anakuja kutuibia, badala ya sisi tukibaki na maneno, badala ya kufikiri kwa pamoja kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, nasema hili kwa sababu, ukiangalia nchi zetu duniani, *European Union, Economic integration* ya *European Union* ilianza mwaka 1948 mpaka leo hii wapo kwenye mazungumzo, miaka zaidi ya 66! Hapa kwetu ikipita miaka miwili mitatu tunaanza kulalamika, sawa. Ikishawahi kutokea, tatizo lipo, *solution* iwe nini? Yaani tuangalie mbele tufanye nini.

Ukiangalia *European Union,* wamefika sasa nchi 27, 28, mpaka *West* na *East* wanajitahidi waje kwa pamoja. Kwanini wanakuja kwa pamoja? Wanakuja kwa pamoja rasilimali kubwa kuliko yote duniani leo hii ni rasilimali watu. Kuwapa watu wako wawe na uwezo mkubwa wa kuweza kufikiri vizuri, kufikiri yakinifu *(power of reasoning)*. Tukiweza kufikiri yakinifu kwenye *protocol,* hii Tanzania tutavuna sana.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Tanzania ni wa pili duniani kwa vivutio vya utalii baada ya Brazil. Utalii peke yake leo hii hapa Tanzania kwenye *GDP* ni zaidi ya asilimia 17. Sasa tunahamasisha namna gani wenzetu hawa kuhakikisha vivutio hivi tulivyo navyo vya utalii hapa kwetu sisi ndiyo tunakuwa Kiongozi, wao ndio tunawavutia hapa kwetu, tunatengeneza

miundombinu iliyo bora wanakuja hapa kuwekeza sehemu mbalimbali za utalii. Sasa ni lazima haya tuyaone kwa mapana.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo, tuyaone kwa mapana kwa misingi kwamba hii rasilimali watu tuliyonayo, kwa mfano hapa kwetu Tanzania, kuna eneo la mraba zaidi ya kilomita za mraba 900,000, hata ukilinganisha na wenzetu wa Afrika Mashariki wote hapa, lakini hatuwezi tukashuhudia kwamba hata Afrika ya Mashariki sisi badala ya kuwa Kiongozi, tunalalamika. Kama mwenzako amekuja na ubunifu ulio mzuri wa ukuaji wa kasi wa sayansi na teknolojia iliyopo duniani leo, tunaona leo amekuja na wazo zuri, anataka kwenda kwa kasi, wewe badala ya kumlalamikia, tafuta mbinu mbadala umshinde kwa sababu leo hii siasa unayozungumzia ni uchumi, siyo siasa za kutoana ngeu, la hasha! Siasa tunazotakiwa tuzungumzie ni siasa ambazo zitaimarisha uchumi wa Tanzania. Siyo siasa za maneno tu, ambayo wanasema mkono mtupu haulambwi.

Mheshimiwa Spika, tukienda *SADC*, Wabunge wetu wanaoenda ndani ya *SADC* tunawa-*empower* namna gani? Wizara ya fedha inawa-*empower* namna gani? Inawapa elimu namna gani? Fursa zilizopo kule Tanzania wanaenda kuzieleza ndani ya *SADC* na wana-*invite investors* wanakuja kuwekeza hapa kwetu. Kwa hiyo, ni lazima waende na *mission!* Huwezi kuwaambia tu waende kule hawana *mission,* wanaenda kule tu wanajitokea wenyewe, wanatoka hapa kila mtu anaenda na lake anakuwa na ubunifu. Sisi *vision* yetu ipo wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unaweza ukaona wenzetu wa Ulaya, hizi *Scandinavian Countries* tunaweza tukajifunza kwao pale. Ni nchi ndogo ndogo sana lakini *happiness index,* nchi ambayo inaishi kwa ile *social security*. *Happiness Index* nchi ya kwanza duniani leo ni Denmark, wakifuatiwa na Swedish, ya tatu ndiyo inafuatia Netherlands. Sasa ni lazima tufikiri kwa mapana nafasi tulizonazo sisi kama Watanzania, tuwa-*empower* watu wetu wa humu ndani, hata kama ni mfumo wetu wa elimu wa kuonyesha kwamba kasi inavyoenda duniani leo hii ni watu wa namna gani tunaowatengeneza?

Mheshimiwa Spika, unajua ukitengeneza Watanzania walio wengi wakawekeza humu ndani na fursa hizi wakapewa vizuri, Serikali ikawapa uwezo, unawa-*invite* wenzako wa *SADC* kwamba njooni na mitaji washirikiane na hawa wetu humu ndani, wekezeni kwenye Sekta ya Utalii, wekezeni kwenye Sekta ya Madini, wekezeni kwenye Sekta ya Uvuvi badala ya kuendelea kulalamika tu.

Mheshimiwa Spika, hata ndugu yangu Mheshimiwa Mnyaa amesema pale, labda Sekta ya Uvuvi tuna kilomita za mraba zaidi ya 230,000, tunatumia namna gani fursa hiyo kwenye *deep sea fishing* kuwaleta hawa watu wengine wa *SADC* tukawekeza na watu wetu hapa, tukapanuka kwa mapana ili wakawekeze? Badala ya kuanza kufikiri namna ya ku-*chase* Wamachinga kodi ya Shilingi mbili, Shilingi tatu, *we have a lot to think* na tukawa ni ma-*giant* wa kufikiri hapa.

Mheshimiwa Spika, Waziri *with due respect*, ningewaomba na timu yako mlivyokaa hapo, wazo zuri ni zuri tu. Tufikiri na tuwasimamie vizuri hawa Watendaji wetu ili tuweze tukawa-*empower information* za kutosha wanasiasa wetu, ili wanasiasa wakiwa na *data* za kutosha watakuwa na haki ya kusema. Hivyo Wabunge wetu waliopo ndani ya *SADC,* tuwa-*empower* vya kutosha, wakienda pale wanajua *mission* ya Tanzania ndani ya *SADC* miaka kumi ijayo tunataka tuwe namna gani?

Mheshimiwa Spika, tuwa-*empower* Wabunge wetu wa Afrika Mashariki wajue hapa sisi ndiyo *giant,* ndani ya miaka kumi au ishirini tunataka tuwe namna gani? Haya mambo mengine

madogo madogo ya kulalamika tuondokane nayo. Sawa, tumeshafikia hapa, sasa twende namna gani huko mbele ya safari?

Mheshimiwa Spika, ningeomba kwa dhati yangu kabisa kwamba hapa tulipofikia bado tunayo nafasi kubwa sana ndani ya *SADC*, haya yaliyotufikisha hapa, sawa, tumeshafika hapa, kuna mambo ya ardhi ambayo yanajitokeza, namna gani tunatumia nafasi hii na nyingine zote.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana. Ni kuwa pamoja tu; Vyama vyote vya Siasa, Waandishi wa Habari na mambo yanaweza kuwa mazuri tu. Sasa namwite Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu. Wewe ni mchangiaji, sikuongezei muda, ni mchangiaji kama wengine.

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. DKT. PINDI CHANA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Itifaki hii ni muhimu sana hususan kutokana na *Geographical Position* ya Tanzania, ikimaanisha tupo kwenye *EAC/SADC* na kadhalika. Hivyo, ni *opportunity,* naomba kujua *method of dispute resolution in case of finance and investment dispute arises.*

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, kabla sijaridhia Itifaki hii ya Fedha na Uwekezaji, niulize suala la Itifaki ya *SADC* ya kuridhia Maazimio ya *SADC* ya *Mtwara Corridor,* ambayo nchi ya Malawi, Zambia, Mozambique, Zimbabwe na Tanzania ziliketi. Pamoja na Maazimio mengine, iliibua suala la *Mtwara Corridor* mwaka 1997 na kutiwa sahihi tarehe 15 Desemba, 2014 na ililenga Mikoa minane katika Tanzania ikiwemo Mikoa ya Rukwa, Iringa, Mbeya, Ruvuma, Pwani, Morogoro, Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Spika, katika kikao hicho Mikoa minane iliwekewa Miradi 100, madhumuni yake ilikuwa kuendeleza masuala ya mawasiliano, ujirani mwema, kufungua biashara, kilimo, utalii, afya na uchimbaji wa madini Kusini mwa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Mikoa hiyo mpaka sasa ipo nyuma, Miradi 100 ilidhamiriwa. Je, Itifaki hiyo itaridhiwa lini?

Mheshimiwa Spika, tupate ufafanuzi huo.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuwapongeza Mawaziri wote na Watendaji wa Wizara, kwa kuleta Azimio hili ili tuweze kuridhia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Azimio hilo.

Mheshimiwa Spika, nchi za *SADC* ni nchi ambazo zinashirikiana katika nyanja mbalimbali likiwemo suala la uchumi. Kwa hiyo, kwa kuridhia Itifaki hii, nchi zitakuwa na Sera, Sheria na Kanuni zinazofanana katika uchumi.

Mheshimiwa Spika, kama tutaridhia Mkataba huu ni imani yangu kuwa, Wananchi wetu; Wakulima, Wafugaji na hata Wafanyabiashara, wanaweza kupata mitaji mikubwa kutoka katika masoko ya mitaji katika nchi hizi.

Mheshimiwa Spika, ningeomba kupata ufafanuzi juu ya mambo yafuatayo:-

(i) Je ushirikiano huu utaathiri kiasi gani au utaboreshwaje na ule wa Afrika Mashariki?

(ii) Ushirikiano huu ni muhimu sana lakini nchi zetu zimetofautiana kiuchumi; je, kuna athari zozote zinazoweza kujitokeza katika kuridhia Itifaki hii?

(iii) Tanzania tumekuwa washiriki katika nchi mbalimbali, lakini nchi yetu imeonesha kuwa wazito kwa baadhi ya mipango ya washirika; je, tumejipanga vipi katika hili?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, sawasawa. Lakini ni Waziri wa Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuchangia hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha ya kupitisha Azimio la Kuridhia Itifaki ya *SADC* ya fedha na Uwekezaji. Utaona kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu inahusika moja kwa moja pamoja na kwamba Waziri wa Fedha amewasilisha.

Mheshimiwa Spika, itifaki hii kimsingi ina lengo la kuongeza uzalishaji, kupanua Soko la Mitaji, Bidhaa na Huduma, kuongeza fursa ya ajira, kuongeza uwezo wa kufuatilia mwenendo wa viashiria vya uchumi mpana na kuimarika kwa Bima na Mifuko ya Pensheni. Hii ni fursa kubwa sana kwa Tanzania na ni kweli kwamba tumechelewa, lakini leo tumeleta Azimio kuridhia na kwa hivyo badala sasa ya kulalamikia yaliyopita, tuangalie jinsi gani tutanufaika kwa kuridhia Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya *SADC* ina idadi ya watu milioni 300. Ina rasilimali kubwa kuliko eneo lingine lolote Afrika. Kama alivyosema Mheshimiwa Mbatia, rasilimali watu ni rasilimali muhimu sana. Sasa hii ni fursa kubwa kwa mitaji, kwa soko...

**SPIKA:** Nitakupa dakika 20 eh, hamku-*communicate* vizuri kwangu. Kwa hiyo…

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Kwa hiyo, Tanzania lazima ione sasa kwamba kuridhia kwa Itifaki hii ni fursa muhimu, kwa hiyo nitumie Bunge lako kuhamasisha Watanzania kuona kwamba hii ni fursa kwa Watanzania kunufaika. Kwanza, kuwa na idadi ya milioni 300 ni soko kubwa, na kwa hiyo, ningependa tuone kwamba tuna majukumu mbele yetu.

Ningependa kuongelea majukumu matatu. Kwanza, ni kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara. Kwa sababu tusipofanya hivi, wenzetu hawatakuja kuwekeza hapa na kama hawatakuja kuwekeza Tanzania maana yake sisi hatimaye tutakuwa soko la bidhaa za wale ambao watawekeza kwenye nchi yao. Tunapokuwa soko, tutakuwa tunawanyima ajira vijana wetu, tutakuwa tunajinyima wenyewe fursa ya kuongeza teknolojia, tutakuwa tunajinyima fursa ya kuongeza thamani kwenye mazao yetu na maliasili yetu tuliyonayo.

Kwa hiyo, suala la kuboresha mazingira ya uwekezaji na mazingira ya ufanyaji biashara ni la lazima. Vile vile la pili ni kuongeza kiwango cha uwekezaji kwa kuweka vivutio mbalimbali vikiwemo vya kodi, sera na sheria.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi, kuna watu hapa ambao wanaogopa kutoa kivutio cha kodi. Ni vizuri kweli tukaona kwamba tunapotoa vivutio vya kodi: Je, ni kwa kiasi gani tunapanua uwezekano wa kukusanya kodi zaidi? Kwa sababu leo kama kwa mfano, Malawi inatoa kodi kwenye mitaji kwa mfano, nasi tunaweka kodi kwenye mitaji, maana yake mwekezaji atataka kwenda Malawi na hatimaye akiwekeza Malawi, atauza bidhaa zake Tanzania na hatawekeza kwetu. Unapowekeza kwetu, kwa mfano nitumie Liganga na Mchuchuma; Liganga na Mchuchuma ni uwekezaji wa msingi kabisa.

Mheshimiwa Spika, pengine huwezi ukaona faida ya kuwekeza Liganga, lakini kutokana na chuma cha Liganga tutakuwa na uwekezaji mbalimbali kwa mfano, kutengeneza magari. Siyo kuunganisha sehemu za magari, kuwekeza kwenye kutengeneza magari. Kutengeneza reli yetu wenyewe kutokana na chuma chetu. Tunaweza tukakusanya kodi nyingi zaidi kutokana na makampuni yatakayotokana na Liganga kwa kuiwezesha Liganga ianze kwa kutoa msamaha wa kodi kwenye uwekezaji wa Liganga.

Kwa hiyo, tuna changamoto ambayo lazima tuiangalie. Kama hatutaweka sera zetu zikafanana na za nchi za *SADC* baadaye tutajikuta sisi ni soko badala ya kuwa wawekezaji kwenye viwanda mbalimbali, wawekezaji kwenye kilimo na kwenye madini.

Tatu, ni kwamba tunapaswa kuimarisha miundombinu ya bandari, barabara, reli na viwanda vya ndege, kwa sababu ndege inatua pale ambapo uwanja wa ndege umetayarishwa vizuri, umeandaliwa vizuri. Kwa hiyo, mwekezaji anatua kwenye nchi ambayo kwanza ana uhakika wa kupata faida, na pili ana uhakika wa usalama wa mali yake na yeye mwenyewe.

Kwa hiyo, tukijipima na nchi nyingine, lazima tujione Tanzania tutanufaika vipi na Itifiki hii. Kama hatutafanya hivyo, nina wasiwasi kwamba tutageuka kuwa nchi ya biashara badala ya kuwa nchi ya uzalishaji, nchi ambayo inavutia mitaji, tutakuwa ni nchi ambayo inavutia bidhaa na huduma na wananchi wetu wanakosa ajira na manufaa mengine ambayo nimeyasema huko. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wameuliza, baada ya kuridhia Itifaki hii inakuwaje, hasa pale ambapo tunazingatia tuko Afrika Mashariki? Hatima ya Itifaki hii ni kuwa na sarafu moja na huko Afrika Mashariki tunataka tuwe na sarafu moja na soko la pamoja.

Kwa hiyo, lililo kubwa mbele yetu ni kuhakikisha kwamba ule utatu, *tripartite* inafanikiwa, ama sivyo tutakuwa na kukinzana kwenye *regency* hizi mbili. Tumefanya makubwa sana kuhusu *tripartite* kwamba tutakuwa na Afrika Mashariki, *SADC* na *COMESA* ambayo itakuwa pamoja. Tukiwa pamoja tutakuwa na idadi ya zaidi ya milioni 700. Ni soko kubwa! Tutakuwa na eneo kubwa lenye rasilimali nyingi zaidi.

Kwa hiyo, kuridhia Itifaki hii itatufanya sisi sasa tufanye bidii ili tuweze kuwa na *tripartite* na eneo kubwa zaidi na Muungano mkubwa zaidi na Jumuiya kubwa zaidi na mimi naamini Tanzania kama ilivyopigania uhuru wa nchi za Kusini. Sisi leo tuko *SADC* kwa sababu tulijitolea kwa hali na mali. Kama tulijitolea kwa hali na mali, tuna kila sababu ya kunufaika na Jumuiya ya *SADC*.

Je, tumenufaika vya kutosha tukilinganisha na hali na mali tuliyojitolea huko awali? Nami najua nchi nyingi zinapenda sana kuwa na Tanzania, lakini narudia tena maeneo yale matatu lazima tuyafanyie kazi na tuwe nchi ambayo inavutia wawekezaji badala ya kuogopa wawekezaji na Mheshimiwa Mbatia amesema hivyo. *(Makofi)*

Kuna Sheria nyingi sana zinapita huko na Sheria moja ambayo mimi ningependa kuongolea ni suala hili la kodi kama kivutio cha wawekezaji.Kuna watu ambao wanafikiria kwamba pengine tunatoa kivutio cha kodi ili kuinyima nchi yetu mapato. Hakuna namna ambayo ukivuna mazao kidogo ukayala mazao yale yote ukategemea mwaka ujao utavuna. Huwezi!

Kwa hiyo, ni lazima kujitolea kwa kiasi fulani kutoa vivutio vya kodi, lakini lazima tuhakikishe baada ya hapo tutakusanya kodi kiasi gani kwa lugha ya Kiingereza, tunasema tunapanua wigo wa kukusanya kodi. Lakini tusipojitolea leo, haiwezekani tukaongeza wigo wa kukusanya kodi.

Kwa hiyo, naomba Bunge hili lizingatie hilo. Najua kwamba ni jambo ambalo siyo rahisi kulielewa, kwa sababu ni bora kula leo kuliko kuhakikisha kwamba unaongeza chakula chako baadaye. Inataka *sacrifice* ya aina fulani.

Mheshimiwa Spika, ukisoma kifungu cha (6) kinasema: "*investment and investors shall enjoy fair and equitable treatment in the territory of any State Party.*"

Sehemu ya pili inasema: "*treatment refers to in paragraph one shall be no less favorable than that granted to investors in the third State.*" Hii inatia wasiwasi kwamba kama uchumi wetu uko chini ya nchi nyingine kwa mfano Afrika Kusini: Je, tukiwa sawa? Haiwezekani ikawa hivyo! Kuna mipangilio ambayo tunawekeana ili tuwe na *fair treatment*. Hii ndiyo maana ya hiki kifungu, kwamba ili kuwe na *fair treatment* lazima tuone nchi ambayo chumi zake ni chini, na zile ambazo chumi zake ni juu na tukaweka mambo ambayo yatafanya kuweza kupata mitaji, kuweza kufanya biashara na ushirikiano ukawa rahisi.

Tanzania kuwa miongoni mwa nchi za *SADC* tutatakiwa kuhakikisha kwamba Sheria na Sera zetu tunazozitunga na kupitisha kwenye Bunge hili hazikiuki kabisa Azimio hili kwa sababu endapo tutafanya hivyo wawekezaji wataenda kule ambako kuna mazingira mazuri ya uwekezaji na baada ya kufanya uzalishaji watauza bidhaa zao Tanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda kupongeza sana Kampuni za Tanzania ambazo zinawekeza Malawi, Mozambique na Zambia. Lakini mimi ningependa wapanue uwekezaji wao uwe mkubwa zaidi ndani ya nchi yao kabla hawajaenda kwingine. Kwa sababu ndege wako utamtegemea zaidi kuliko ndege wa mtu mwingine. Kwa hiyo, pamoja na kuweza kuianisha Sheria zetu, lazima tuangalie maslahi ya Tanzania na ili tunufaike na soko hili la pamoja badala ya Tanzania kunufaika na soko la *SADC* kama ilivyotarajiwa awali.

Kifungu Na. 4 cha Itifaki hii kinazungumzia masuala ya *PPP (Public Private Partnership),* ni matumaini ya Serikali yetu, kwa sababu mapato yetu ya Serikali ni madogo na tungependa yaende zaidi kwenye maeneo ya afya, elimu, Mahakama, yaani maeneo ambayo hakuna faida, lakini kunakuwa na manufaa mengine. Kwa sababu huwezi ukawa na nchi ambayo wananchi wake wana afya ya chini; hawawezi kulima! Hawawezi kuwa viwandani! Kwa hiyo, suala la afya nalo ni muhimu.

Sasa kuna maeneo ambayo tukiweza kuiwezesha *Private Sector* inaweza ikawekeza na unakuta kwamba nchi kama ya kwetu unaweza kuwa na *private sector* ambayo ni ndogo, lakini wakishirikiana na *Private Sector* ya Afrika Mashariki au Afrika Kusini au *Mozambique* tunaweza tukawekeza kwa kiasi kikubwa zaidi katika miundombinu.

Kuna miundombinu *by their nature* kwa msingi wake haina faida inapaswa kuwezesha uwekezaji mwingine. Lakini Serikali ikiweza kuweka mipango mizuri kwa Sekta Binafsi kushiriki

kwenye miundombinu, inaweza ikapata ushiriki mkubwa wa Sekta Binafsi, nami naamini, miradi ya *PPP* itakuwa mikubwa kama ushirikiano wetu kupitia itifaki hii itaweza kuimarishwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile ningependa kuongelea kifungu cha 17 kinachoongelea makubaliano kati ya nchi wanachama kuepuka utozaji wa kodi mara mbili.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida uwekezaji unatokana na faida. Kama unatokana na faida, maana yake huyu ambaye ana faida ameshalipa *corporate tax.*Sasa kama mtu anakuja kuleta mtaji wake kutoka Malawi kwa mfano kuja Tanzania, huko ameshatozwa kodi, wewe ukatoza kodi. Kwanza, unapunguza mtaji wa kuwekeza na kwa hiyo, unapunguza uwekezaji wenyewe. Lakini kutoza kodi mara mbili siyo sawa.

Kwa hiyo, ningeomba sana Bunge hili litazame mambo hayo ambayo nimeyaibua mimi tuone kama tunakwenda sambamba na wenzetu ili tunufaike na Itifaki hii ambayo tunairidhia leo hii.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuleta itifaki hii. Tutanufaika zaidi kutokana na uwekezaji. Tutanufaika zaidi kama tukilinganisha uchumi wetu mpana na uchumi wa nchi nyingine. Tutanufaika zaidi endapo tutawahamasisha Watanzania kuwekeza kwenye nchi yao, na baada ya kuwekeza hapa wakawekeza kwenye maeneo mengine ya *SADC*. Tutanufaika vile vile na sisi kujifunza kutoka kwa wengine.

Kwa hiyo, Itifaki hii ni muhimu sana na ninashukuru sana kwamba yeye ni mpya, lakini hatimaye katika upya wake ameweza kuifanya Itifaki hii ikafika kwenye Bunge lako Tukufu na mimi naomba Wabunge wote wahamasishe Watanzania ili tuwe na Watanzania walio wengi wanaowekeza ndani ya nchi yao na wao watakuwa ni Mabalozi wazuri kwa wale wanaotoka nje kuwekeza kwenye nchi yetu ya Tanzania. Lakini baada ya kupata uwezo zaidi wakawekeza kule kwingine ili na sisi tuchangie uchumi wa eneo hili la *SADC* zaidi ya kuchangia uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, narudia usemi wa aliusema tena Mheshimiwa Mbatia ambao Mheshimiwa Mkapa aliusema kwamba, Tanzania itanufaika zaidi na dunia, kuliko dunia itakavyonufaika zaidi na Tanzania. Lakini tutapata manufaa hayo kama tutaweka mazingira mazuri ya uwekezaji wa biashara na kama tutachunga manufaa yale yasiende nje, bali yabakie ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii uliyonipa, nami nitasaidiana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuhakikisha kwamba tunatekeleza Azimio hili baada ya Bunge lako kuridhia. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante. Unaunga mkono hoja. Haya.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, niliunga mkono hoja kutoka mwanzo na narudia tena kwamba naiunga hoja hii kwa nguvu zangu zote na nitahakikisha kwamba nasaidiana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Nashukuru kwa mawasilisho hayo, lakini kubwa mimi nadhani kwa kupitia hii Idara yako wewe ama Wizara yako, wako vijana wengi wanaweza kufanya mambo

madogo madogo lakini mwisho wake yanakuwa makubwa. Mimi nadhani hilo ni kubwa zaidi kuliko jambo lingine.

Waheshimiwa tunayo mambo mawili. Kwanza leo ni siku ya Ijumaa, lakini pili, niliwatangazia kwamba tunaenda kufungua *Gym* pale. Tatu, napenda watoa hoja nao wakajiandae kwa kushirikiana na wataalam wao huko, kusudi mchana tukirudi saa 11.00 tuweze kupata majibu ya kuanzia kule kwa Wizara inayohusika.

Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.34 Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulipositisha shughuli za Bunge kipindi cha mchana, wachangiaji wote walioomba walikuwa wamekamilika.

Kwa hiyo, nawapa nafasi wenye hoja tukianza na Naibu Waziri, Mheshimiwa Malima, dakika 20.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):** Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza naomba kwa ridhaa yako nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hapa, lakini pia niishukuru michango iliyotoka kwa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali kuhusiana na Itifaki hii ya *Finance and Investiment* inayokuja hapa kwa ajili ya kuridhiwa.

Mheshimiwa Spika, hoja zilizokuja ni nyingi na tumegawana, lakini mimi kwa upande wangu nataka nizungumzie haya machache kama nafasi itakavyoniruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni katika suala lililozungumziwa kuhusu madhumuni ya uanzishwaji wa *SADC* na *EAC*. Lililokuwa linazungumzwa ni kwamba, aah, sasa kama Tanzania tunaingia kwenye Itifaki hii moja *SADC,* lakini inakuwaje kama tunaingia kwenye Itifaki zinazofanana kwenye upande wa *EAC?*

Mheshimiwa Spika, kwanza, labda niseme tu kwa manufaa ya Waheshimiwa Wabunge, ambalo ninalifahamu na wote wanalifahamu ni kwamba sisi Tanzania ni nchi pekee katika *blocks* hizi mbili ambazo ni wanachama wa pande zote mbili, kwa maana ya kwamba *SADC* ni peke yetu sisi ambao ni wanachama wa *EAC* na *EAC* ni sisi peke yetu ambao ni wanachama wa *SADC*.

Mheshimiwa Spika, hili siyo jambo la *accident*. Ukiangalia, lina misingi ya kihistoria na lina misingi ya mahusiano yetu ya kiuchumi na nchi hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, msingi wake wa kihistoria, kama unavyofahamu ni kwamba Tanzania tulikuwa mwanachama wa Umoja wa Afrika Mashariki *(East African Community)* mpaka mwaka 1977 ulipo-*disolve,* lakini wakati ule tukiwa Kenya, Tanzania na Uganda. Kwa hiyo, tulikuwa na msingi yetu na mahusiano yetu ya kiuchumi ambayo yana msingi ya kihistoria tangu huko nyuma.

Mheshimiwa Spika, sasa mwaka 80 Wakuu wa Nchi ambao wakati ule walikuwa wanaitwa *Front Line States,* zile nchi tano mabazo ndizo zilikuwa nchi za mstari wa mbele; nazo zilikuwa Tanzania, Mozambique, Zambia, Botswana, nadhani na Angola; nchi tano hizo, tukaamua kwamba tutakuwa na *Economic Community Block* ya kuanzia ambayo wakati ule ilikuwa inaitwa *Southern African Development Co-ordination Conference*. Iliundwa tarehe

1Aprili, mwaka 1980 Lusaka kwa matarajio ya kwamba zilikuwa nchi nyingine zinaingia kama Zimbabwe na wakati huo tungechukua na Swaziland, na kadhalika na nini ziingie mle ili kuyapa nguvu zaidi sasa yale mahusiano ambayo yalikuwa ni ya kisiasa, kuyapa nguvu ya mahusiano ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumekuja na mahusiano yale mpaka mwaka 1992 ambapo sasa Wakuu wa Nchi wakaona sasa hii *SADCC – Southern African Development Co-ordination Conference,* imeshakua, yaani katika misingi yake imekuwa kitu kikubwa zaidi. Wakati huo tena Zimbabwe imeshakuwa huru na Namibia imeingia na *South Africa* inaelekea kwamba sasa tutakuwa na *block* kubwa zaidi. Kwa hiyo, badala ya kuwa na *Southern African Co-ordination Conference,* tukawa na *Southern African Development Community*. Sasa hii kimsingi, lengo lake lilikuwa ni kuwa na Jumuiya ambayo inakwenda kuanzisha kitu chenye malengo mapana zaidi ya kisiasa na ya kiuchumi na ya kijamii, kwa maana ya *Economic Intergration.*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo sasa wanatengeneza kitu kinaitwa *Treaty 1992*. Baada ya hapo sasa, sisi huku kwenye jamii yetu ya Afrika Mashariki tuna jambo letu ambalo mahusiano yetu na sisi huku yanaanza kubadilika, yale mambo ya unyang'au sijui na mgogoro tuliokuwanao mwaka 1977 mambo yamekwenda yakibadilika, mahusiano yameboreka, kwa hiyo, nasi wakati huo tukawa tunazungumzia jambo letu wenyewe sisi watatu kulifufua. Sasa mwanzoni lilikuwa linaonekana kwamba, aah, sasa Tanzania tunaweza tukawa na mgogoro, kwa sababu huku kuna *SADC na* huku kuna *East African Community!*

Mheshimiwa Spika, kimsingi nataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa misingi ambayo hawa waliotutangulia waliiweka, hatuna mgogoro wa kushiriki *SADC* na hatuna mgogoro wa kushiriki *EAC*. Katika hilo, labda niseme tu kwamba, baadaye historia imekuja kutuunga mkono kwa sababu sasa baadaye tena hizi *blocks* zote mbili ukijumuisha na *COMESA* zimeunda kitu kinaitwa *Tripartite,* ambayo ina malengo makubwa zaidi ya kiuchumi ya kuwa na mfumo mmoja wa forodha, na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa najibu ile hoja ya kwamba, labda tukiwa huku kwenye *SADC* na tukiwa huku kwenye *East African Community* tunaweza tukawa na mgogoro wa maslahi, hapana. Hili jambo wazee walikuwa wameliangalia na limeonekana halina mgogoro.

Mheshimiwa Spika, kuna swali lingine limeulizwa kuhusiana na hilo hilo ambalo limesema kwamba, aah, tunahitaji kuwa kwenye maeneo, yaani tuna fursa zaidi. Wapi tuna fursa zaidi kati ya *East African Community* au *SADC?* Sasa jibu ni kwamba, tunahitaji kuwa kwenye maeneo yote ya Kikanda ili kuiwezesha nchi yetu kunufaika na soko kubwa zaidi. Huku *SADC* kuna soko kubwa zaidi kuliko *East African Community,* kwa hiyo, tuna manufaa sisi kama nchi ya kuwa na mahusiano katika *blocks* zote mbili.

Mheshimiwa Spika, labda niseme jambo moja tu, kwa mfano, kwenye *East African Community* sisi nchi tano kwa pamoja, watu wote kwa pamoja nadhani ni kama milioni 125 au milioni 130. Tukichukua *block* ya *SADC,* kuna soko ambalo linajumuisha watu zaidi ya milioni 300. Kwa hiyo, ukichukua haya masoko mawili, tuna soko la pamoja la watu zaidi ya milioni 400 au *around* milioni 400. Kwa hiyo, sisi tuna hiyo *added advantage* ambayo inatuwezesha kushiriki kwenye masoko yote mawili.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala lililozungumzwa kuhusu kuridhia Itifaki.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Nagu alikuwa amelizungumza vizuri sana. Nilitaka kutoa mfano mmoja tu kwamba sisi Tanzania kuna mambo ambayo tunapata kwenye *EAC* ambayo hatupati kwenye *SADC*.

Kwa mfano, kuna mambo ambayo *SADC* wamekubaliana tangu 2008 kwamba tutakuwa na *Free Trade Area,* tutakuwa na *Customs Union,* tutakuwa na *Monitory Union* na ratiba zake zikapangwa; kwa sababu mbalimbali, ratiba ile imekuwa imechelewa kufikiwa. Ukija kwenye upande wa *East African Community,* ratiba ile tumejipangia, lakini ratiba ile *East African Community* inaonekana inakwenda vizuri zaidi. Kwa nini?

Mheshimiwa Spika, ni kwa sababu, hii Jumuiya ya hizi nchi tano kijiografia na kisiasa na kiuchumi ina mambo mengi ya karibu. Ina *common issues* nyingi zaidi ambazo zinawafanya waweze kukubaliana kwa urahisi zaidi kuhusu mustakabali wa kwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, upande huu wa *SADC,* tuna mambo makubwa pia. Mimi nakumbuka mwaka 2013 kwa mfano, nitoe mfano tu mmoja.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013 nikiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika tulikwenda kwenye Mkutano wa Mawaziri wa *SADC* wa Kilimo. Kufika pale tukakuta soko lile, watu wa Seychelles wanalalamika kwamba Seychelles pale wakitaka kununua kuku au wakitaka kununua ng'ombe na nini, wanakwenda kuchukua ng'ombe wao Australia. Sasa wakawa wanatung'ang'ania wanasema, ninyi Watanzania mna ng'ombe zaidi ya milioni 24, *what are you doing to address our issues within the SADC? Is a common market!*

Mheshimiwa Spika, soko kubwa la ng'ombe lingine linaonekana liko labda Botswana na Namibia, lakini Tanzania *we have a huge* fursa hiyo mojawapo ya kuingia kwenye soko hilo, isipokuwa sasa kuna mambo ambayo yanaendana na misingi ya kibiashara ambayo yanafungua fursa zile. Kwa hiyo, nilitaka kutoa mfano huo.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine ni kwamba, nikiwa Naibu Waziri wa Niashati na Madini, tulikwenda Botswana, tukawa tunazungumzia suala la *Power Pool.* Kwamba, Tanzania kwa sababu ya *resources* tulizokuwanazo kwenye *energy,* tukiweza kuzipata na hizi zote tutakuwa sisi wenyewe ni *producer* wakubwa, wazalishaji wakubwa wa umeme kwa ajili ya Kanda hiyo nzima ya *SADC*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitaka kusema tu kwamba, hapa tupozungumzia masuala ya *finance and investiment,* yaani masuala ya uwekezaji na masuala ya fedha kwenye *SADC Conference* sisi kama Tanzania tusihofu.

Kuna suala nadhani Waziri wa Fedha Kivuli amezungumza pale, kwamba tusihofu kuhusu suala la kuingia, kwa sababu ukihofu ndiyo utabaki hapo hapo nyuma. *Those who do not dare, do not conquer.*

Sasa sisi Tanzania tuna fursa zetu; kwamba sisi wenyewe hatujatumia fursa zetu tukaweza kuingia kwenye masoko haya na kuweka nguvu yetu pale, *is another issue all together.*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kwenye *SADC,* labda niseme tu kwamba, sisi *were always considered the second largest economy*. Sisi ndio ilikuwa chumi ya pili kwa ukubwa *SADC* kihistoria, baada ya *South Africa*. Sasa tumepigwa bao kwa sababu, wenzetu wa Angola wana mafuta.

Kwa hiyo, *they have become the second.* Tukiendelea kubaki nyuma, tutaendelea kupigwa bao kwa sababu, wenzetu wa Msumbiji wanashindana na sisi kwa gesi; wenzetu wa Namibia wanashindana kwa madini.

Kwa hiyo, ni masuala ya sisi wenyewe, nadhani alizungumza Mheshimiwa Dkt. Nagu akasema ni kujitambua kwamba sisi kama Watanzania tuna fursa gani? Tuna uwezo gani? Ni wapi ambapo tuna *competitive advantages* ambazo zinatuwezesha tukiingia au tukiwemo mle kwenye *SADC* tuwe na nafasi yetu?

Mheshimiwa Spika, hizi jumuiya kama Jumuiya ya *SADC is no longer a political organization.* Kama mnakwenda pale, mnapiga blabla, sijui huku kuna uchaguzi, sijui huku kuna nini, wenzetu wanatazama hizi kama *economic opportunities.*

Sasa tukiacha kuziangalia kama fursa za kiuchumi, tutakuwa miaka yote tunakwenda, tunapiga blabla, na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunavyoridhia Itifaki hii ni kwa sababu ni kama vile tunaingia sokoni sasa na sisi tukaweke mazao yetu pale ili yaweze kupata nafasi ya kuuzika.

Mheshimiwa Spika, kimsingi, kama nilivyosema, ziko nchi ambazo zinaangalia hizi, *South Africa,* hao hao *South Africa! South Africa* uchumi wote ni kama Dola bilioni 370, nchi nyingine zote 13 uchumi wetu kwa pamoja ni Dola milioni 570. Kwa hiyo, *South Africa* uchumi wake ni asilimia 60 ya *block* nzima.

Mheshimiwa Spika, hata leo pamoja na ukubwa wake wote ule, ukiwaambia *South Africa* bwana, haya basi ondokeni, bakini wenyewe, hawatakubali. Kwa sababu, wao bado wana-*consider* hili soko linalotuzunguka kama ni eneo la fursa ya wao kujitanua zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba tu kwamba, nimetambua kuna Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia na wamesisitiza hili jambo la kusema jamani, Tanzania sijui, tukijiweka kwenye unyonge tutabaki kwenye unyonge. *These are economic opportunities.* Dunia inabadilika!

Mheshimiwa Spika, nilitaka tu kutoa mfano kwamba wakati *SADC* inaanza, ilianza na nchi tisa au nane hivi na sasa hivi ina nchi 14.

Kwa hiyo, mazingira yale ya nchi nane wakati ule na sasa hivi ina nchi 14 na mazingira ya nchi tofauti, lakini hata kwenye *European Union* nao wana mfano huo. Walianza nchi tofauti, lakini *Eastern Blocks* zilivyomong'onyoka, wamechukua zile nchi wameziingiza ndani. *Why?* Kwa sababu, *it is always the basic economic theory* ya kusema una watu, una soko.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nami nilikuwa nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba turidhie Itifaki hii kwa sababu ina maslahi mapana. Lakini jambo lingine kubwa ni kwamba hata pale ambapo tunapenda sisi kama nchi kufanya marekebisho kwenye Itifaki hii, ni lazima muwe mmeiridhia kwanza.

Kwa hiyo, hatuwezi tukaona vitu ambavyo tunasema aah, sisi hiki hapana, sisi hiki ndiyo, kama hatujairidhia. Kwa hiyo, tunairidhia halafu tunaingia mle ndani. Sasa tukiingia mle ndani tukiona labda kuna mambo ambayo hayajakaa sawasawa, tutakwenda kurekebisha mlemle ndani.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo nilikuwa nimependa kulisemea ni hili suala la mwelekeo wa *SADC* yenyewe, kwa sababu, mwelekeo wake kama nilivyosema ni masuala zaidi ya kiuchumi.

Hii migogoro ya kisiasa ambayo inatukwaza kwenye *SADC,* labda Zimbabwe imefanya uchaguzi, Kongo; ina maana hizo ndizo nchi mbili ambazo zina mgogoro; vita vya ndani vya Angola, na kadhalika, tunavuka hapo, tunakwenda tukivuka *as an institution.* Jambo linalofuata ni fursa za kiuchumi. Sasa sisi tukiwa tumekaa bado tuna hofu kuingia na kutoka, kuingia na kutoka!

Mheshimiwa Spika, kuna suala limezungumzwa la *Capital Flight* hapa, nadhani Mheshimiwa Waziri naye atakuja kulizungumzia. Lakini kuna suala lingine la *Human Flight,* wale wataalamu wetu wanatoka wanakwenda huko. Mimi niliwahi kwenda Botswana nikakuta Mkurugenzi wa Jiji la Gaborone, Mji Mkuu wa Botswana ni Mswahili.

**SPIKA:** Mtanzania?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):** Mheshimiwa Spika, ni Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, ni Mtanzania. Madaktari kibao, Watanzania. Ukisema unaitisha Mkutano wa Watanzania, wanakuja watu chungu nzima! Walimu wa Chuo Kikuu, Walimu wa nini; wanachofuata nini? Wanafuata fursa *(economic opportunities) and you can't stop a human being when he is going for opportunity.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasi haya mazingira tunayoyatengeneza hapa kwa kuridhia kwenye Azimio hili ni kwamba, tunataka kuipa Tanzania nafasi yake ya kiuchumi kwenye Jumuiya hii.

Matarajio yetu ni kwamba uwekezaji, lakini pia na misingi ya mahusiano ya fedha na nchi zetu nyingine hizi na Taasisi za kifedha zinatupa Tanzania uwezo mkubwa wa ushiriki na kupanuka zaidi katika nguvu ya uchumi katika Jumuiya yetu hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niwasihi Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba, turidhie Azimio hili na kama kuna mambo ambayo yako huko mbele ambayo tunaona bado yana maslahi kwa Taifa letu, tukienda huko kwenye vikao husika bado ndiyo tutakuwa na fursa zaidi ya kutengeneza nguvu zaidi ya kuweka mambo ambayo yana maslahi kwa Tanzania, lakini katika mfumo wa maslahi ya Jumuiya nzima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa hayo, naomba nishukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini pia nitamke kwamba naunga mkono hoja ya kuridhia Azimio hili la Itifaki. Nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante, sisi tukienda kwenye Mkutano wa *SADC,* wale Watanzania pale wanakusanyika, wako zaidi ya familia 100. Hata aliyekuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Windhoek alikuwa Mtanzania na tunao wengi; na Walimu, Manesi wako kule na *Engineers.*

Sasa namwita Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mwigulu Mchemba!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA):** Mheshimiwa Spika, nami nichukue fursa hii kukushukuru kwa nafasi hii ili jiweze kusema machache kwa niaba ya Waziri wa Fedha.

Niseme tu kwamba kuna hoja zilizotolewa ambazo zinahitaji kujibiwa, lakini kuna ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge ambao unatusaidia sisi kama Wizara na sisi kama Serikali kuweza kuboresha namna tunavyoyashughulikia masuala ya nchi inapokwenda kwenye kusaini Itifaki hizi.

Mheshimiwa Spika, limetolewa jambo la ushirikishwaji linalohusu elimu. Nitamke tu kwa niaba ya Waziri kwamba sisi kama Wizara hilo tunalichukua na tutachukulia kwamba ni suala endelevu kwa suala hili hili la *SADC*, lakini hata kwa masuala mengine yanayohusu kuingia Itifaki katika michakato hii ama ya *SADC* ama ya *EAC* ama hata *negotiations* nyingine zote ambazo zinahusu Taifa letu. Kwa hiyo, kwenye hili tutaliendeleza.

Mheshimiwa Spika, lilikuwepo suala la kwamba, kama jambo hili lina manufaa, kwa nini tumechelewa?

Mheshimiwa Spika, hilo nalo tumelichukua, tumepewa kama ushauri na sisi tutalichukua. Kwa kweli, ni jambo ambalo kwa heshima ya Taifa tunatakiwa tusionekane kila wakati kuwa ni watu wa kuchelewa. Hii itakuwa imeanza kuwa tofauti.

Mara zote katika historia Tanzania imekuwa nchi ambayo inaongoza kwenye mambo ya aina hii.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ilikuwa mstari wa mbele, ndiyo ilikuwa kiongozi kwa *SADC*.

Hata kwa Afrika Mashariki Tanzania ndiyo kiongozi na jiografia yetu imetuweka hapo na kwa mambo mengine pia Tanzania ndiyo kiongozi. Kwa hiyo, ushauri wa Wabunge tutauchukua na niseme tu kwa hili imetokea kwa sababu ya mazingira tuliyokuwa nayo. Jambo la kuwa na *blocks* mbili ambazo zote zina lengo la aina ileile ambako Tanzania inalazimika kuwepo kwa mujibu wa faida na kwa mujibu wa historia, kwa kweli lilikuwa linahitaji uchambuzi wa kina.

Mheshimiwa Spika, Kama alivyotangulia kusema Naibu Waziri mwenzangu, historia ilikuwa inatubana sana kwamba hatuwezi kwa kweli tukaiacha *SADC* na tukaeleweka. La pili vilevile historia pamoja na aina ya mahusiano tuliyonayo kwenye Afrika Mashariki ni jambo lingine nalo ambalo hatuwezi tukaeleweka. Kwa hiyo, ilibidi ifanyike tathmini na uchambuzi mkubwa na kuangalia tunakoendelea sasa tutaendaje kitu ambacho kilihitaji muda.

Mheshimiwa Spika, niwape *comfort* tu Wabunge na Watanzania kwamba tunaloliangalia kwa mbele ni kwamba kuna hizi hatua ambazo zina manufaa kwa Taifa kwa mfano, Soko Huru, Soko la Pamoja ni vitu ambavyo unaweza ukawepo *SADC* na ukawepo Afrika Mashariki. Utakumbuka wakati Tanzania imejitoa *COMESA* baadhi ya wafanyabiashara walisema uamuzi ule haukuwa sahihi kwamba tungeweza kuendelea ili wafanyabiashara wanaotaka kufaidi fursa kule waendelee kufaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa mazingira hayo, Watanzania wasiwe na mashaka sana kwamba sasa kama lengo la huku ni hilo na la huku ni hilo, kama Taifa kwa nini tusichukue upande mmoja na mimi niseme tu tusije tukaipoteza historia yetu na kazi yetu iliyotukuka katika pande zote mbili bali tuwe na lengo lile ambalo ni la dunia nzima kwa kweli la mtazamo wa kuungana. Kwa hiyo, tuende kwenye ile hoja ya utatu yenye lengo la kuunganisha *SADC, COMESA* pamoja na Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwenye hili utaona kwamba hata haraka haraka tu tukijiuliza kwa mfano bandari yetu ya Dar es Salaam matumizi yake yana tija kote kwa nchi za *SADC* na kwa nchi za Afrika Mashariki. Hivyo hivyo kwenye masuala ya rasilimali watu, hivyo hivyo kwa masuala ya biashara. Kwa hiyo, la msingi zaidi ni sisi kama ambavyo tumekuwa tukifanya kuwa kiunganishi katika mambo yanayohusu ukanda wetu huu tuendelee kuliona kwamba jambo la utatu kuwa na lengo la pamoja la kuunganika mwishoni ni jambo ambalo litatuletea faida zaidi.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa Afrika Mashariki, uhusiano wetu si wa kisiasa tu, una undugu ndani yake. Wamasai wa Mara na Wamasai wa Kenya ni watu ambao ni ndugu, hivyo hivyo kwa Kagera, hivyo hivyo kwa Ngara, kwa hiyo, ni zaidi ya mipaka. Ukienda kwa nchi za Kusini kwa kweli, ukikumbuka hata hotuba ya Mheshimiwa Rais kwenye msiba wa Mandela utaona Tanzania ina nafasi gani katika hizi nchi za Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye hili la itifaki kuanza kazi, kama nilivyosema asubuhi kwamba kuanzia tarehe 16 Aprili, 2010, itifaki hii ilipata nguvu ya kisheria ya utekelezaji baada ya nchi tisa kati ya kumi na nne za *SADC* zilizosaini itifaki kuwasilisha hati za kuridhia. Nilipokuwa nasema hili nilikuwa nahesabia kwamba Madagascar kwa kipindi ilisimamishwa uanachama wake tangu mwaka 2009 hadi sasa tunavyoongea. Kwa hiyo, kwa kile kilichotokea kwa Madagascar maana yake kiliweza kutengeneza theluthi mbili kuweza kupatikana. Hivi tunavyoongea sasa hivi tayari nchi kumi na moja zimesharidhia itifaki hii, kwa hiyo tulibaki sisi Tanzania, Zimbabwe na Shelisheli. Sasa ukiangalia historia iliyokuwepo, kwa kweli Tanzania haipaswi kukaa sehemu moja na Shelisheli na Zimbabwe kwenye suala hili la *SADC* ambapo Tanzania imekuwa na nafasi kubwa katika kuhakikisha kwamba hii *SADC* inakuwepo.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo lingine liliulizwa kwamba ni sababu gani Serikali haikuleta Bungeni mikataba ya uwekezaji ili iweze kupata ridhaa na nguvu ya kisheria. Mikataba ile ambayo tulikuwa tunaiongelea kwenye hizi nchi za *SADC* ilikuwa ya kibiashara zaidi na ilikuwa ni *bilateral* kwamba Tanzania inaingia mkataba na Malawi ama Tanzania inaingia mkataba na Zambia au na Zimbabwe. Kwa hiyo, kwa hii na kwa sheria tulizonazo ilikuwa ni mikataba tu ambayo iko kwenye himaya za kiutendaji na yenyewe ni ya kibiashara, unaweza ukaona kwenye maelekezo ambayo yalitolewa na Mwanasheria Mkuu.

Mheshimiwa Spika, hili la kwamba kwa nini Serikali ilisaini mikataba kabla ya kuridhia itifaki hii, ni kwamba Tanzania ilikuwa na ulazima wa kutengeneza mazingira ya kibiashara kwenye nchi ambazo inafanyanazo biashara kwa kiwango kikubwa zaidi. Biashara kati ya Malawi, Zambia, Zimbabwe utaona ni ya kiwango kikubwa kuliko nchi nyingine zile zilizoko pembeni zaidi mwa Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, hili la wapi tuna fursa zaidi, nimeshalielezea na Naibu Waziri mwenzangu ameshalisema na tunayo hiyo mifano. Tunaendelea kupongeza kazi ambayo ilifanywa na sisi kwa kweli kama *generation* ya leo tusingependa kazi iliyofanywa na Waasisi wetu, Mwalimu Nyerere na *generation* ya uongozi wake, sisi leo tuje tuimalize. Tutaendeleza kucheza *midfield,* kucheza kiungo katika kuunganisha ukanda huu kazi ambazo alizifanya Mwalimu Nyerere na kwenye hili niseme tu kama mmoja wa viongozi vijana, niwaahidi Watanzania tutaliendeleza na kazi hizo zitaendelea kutukuka.

Mheshimiwa Spika, uwezekano wa sarafu moja kwenye *EAC* na *SADC*, hatuwezi tukawa na sarafu moja tukiwa *SADC* na wakati uleule tukawa na sarafu moja Afrika Mashariki. Litakalofanyika ni lipi? Wakati tunafanya uchambuzi wa kuweza kuwa na sarafu moja Afrika Mashariki, vigezo vinavyotumika vimeanishwa kwenye mfumuko wa bei, vimeanishwa kwenye uchumi mpana, hivi hivi ndivyo vinavyotumika kwenye *SADC*. Kwa hiyo, lililopo kwa utaratibu na mazingira ya nchi chache za Afrika Mashariki, uwezekano mkubwa ni kwamba tutaweza kuingia kwenye sarafu moja kwa Afrika Mashariki kabla ya *SADC* na hii inatokana na ukweli kwamba nchi za SADC ni nyingi, kwa hiyo mgawanyiko ama ile *divergence* ya mambo makubwa ya uchumi mpana ni makubwa zaidi. Vilevile *convergence* ya nchi za *SADC* kuwa na mfumuko wa bei unaolingana ama kuwa na upungufu wa bajeti unaolingana, utafikiwa kwa muda mrefu zaidi kuliko kwa nchi za Afrika Mashariki. Kwa hiyo, likifika hili tukiwa tuko kwenye sarafu moja ya Afrika Mashariki halina madhara sana kwa nchi kwa sababu nchi itaendelea kufaidi yale

yanayohusu biashara ambayo na yenyewe ni ya msingi ambayo si vyema kuyaacha tu kama nchi isishiriki kisa imeshakuwa na sarafu moja ya upande mwingine.

Mheshimiwa Spika, ni kama hivi sasa hivi tunavyofaidi mambo ya kibiashara hata kabla hatujawa na sarafu moja na wenzetu wa Afrika Mashariki, hivyo hivyo tunaweza tukawa na makubaliano ambayo ni ya kibiashara, ya soko huria ama ya soko la pamoja wakati tuko na sarafu moja na sijajua kama tutairejesha kama ni shilingi ya Afrika Mashariki ama namna gani na tukaendelea kutoa fursa kwa watu wetu.

Mheshimiwa Spika, jambo moja ambalo napenda niliseme, pamoja na kwamba tunasemea hizi kama fursa, tuna mambo ambayo tunatakiwa kama Taifa lazima tubadilike. Tunasemea zaidi kuhusu fursa lakini tunalazimika kutambua kwamba tunapoungana, tunapokwenda kwenye *globalization*, kwenye ushirika wa aina hiyo, ni vyema Tanzania tukatambua kwamba tunaenda kwenye ushindani. Tunapokwenda kwenye ushindani, kuna baadhi ya mambo ni lazima tuyarekebishe. Baadhi ya mambo hayo ni pamoja na vikwazo ambavyo vinaweza vikaikwaza nchi hata kama ina fursa ama vikwazo ambavyo vinaweza vikawakwaza wananchi hata kama kuna fursa.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano, tunaweza tukawa tumeshaingia kwenye soko huria ambalo linaruhusu mazao ya wakulima kutoka Tanzania kwenda Malawi lakini ikitokea kuna vikwazo vya ndani ya nchi maana yake kutakuwepo na mikataba lakini wananchi wetu hawataweza kufaidi. Tunayo mifano mwaka juzi kitu kama hicho liliwahi kutokea tamko kwamba kutokana na kujitosheleza kwa chakula ndani ya nchi wakulima wasiuze mahindi yao ama mazao yao nje ya nchi, hiki ni kikwazo ambacho kinaweza kikawasababisha wakulima wawe maskini licha ya mikataba kuwaruhusu wao kuwa na soko katika sehemu nyingine na kuweza kunufaika na kilimo chao. Niseme tu sisi kama Serikali, sisi kama Wizara hatutegemei kushauri tena hivyo kwamba mkulima alime mwenyewe lakini asipate fursa ya soko huria ama manufaa yanayotokana na soko huria.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ambalo ningependa nitoe rai linalohusiana na kwamba tunapoingia kwenye itifaki hizi inamaanisha ushindani. Ni lazima Watanzania, ni lazima wataalam na ni lazima viongozi wa kisiasa tubadilike. Niliwahi kushuhudia mwaka 2009 nikiwa Mchumi Benki Kuu kule Arusha, kulikuwepo na makubaliano haya haya ya Afrika Masharika siyo haya ya *SADC,* ikatokea kikao kinachohusu *negotiations,* kilikuwa kinafanyika Arusha, mimi nilienda kwa sababu nilikuwepo pale na nilikuwa na *interest* kwamba jambo linaloongelewa ni la kiuchumi. Watu wa Uganda kwa ajili ya kutoa uzito kwenye jambo hilo walikuja na basi, walikuwa kama 25 mpaka 30 hivi, Wakenya walikuja na magari na wenyewe walikuwa kama 20 mpaka 25, Rwanda walikuja kama 15 hivi, sisi Tanzania huku tukiwa Mwenyekiti wakati huo Rais ndiyo alikuwa Mwenyekiti wa Afrika Mashariki, kwa hiyo sisi Tanzania tulikuwa Mwenyekiti wa kikao kile tulikuwa na watu wanne yaani mimi nilienda na bosi wangu pale Moto Lugobi tukaongezeka tukafanya Watanzania wawe wanne. Kwa hiyo, utaona kwamba mnapokwenda kwenye *negotiation serious* kama hizo ambazo zinahusu ushindani, tunahitajika sana kuona kwamba *negotiotions* hizi siyo fursa tu peke yake bali ni ushindani.

Mheshimiwa Spika, kuna suala limesemwasemwa sana hapa na Wabunge, nakumbuka amelisema Mheshimiwa Leticia linalohusu uzalendo. Kwenye hili la *negotiations* ni lazima Watanzania, wataalam pamoja na viongozi tunapokuwepo kwenye *negotiation* ni lazima tuchukulie kwamba ni jambo la kufa na kupona kwa sababu likishasainiwa tutabaki kulia wenzetu watachukua hizo fursa. Kwa hiyo, uzalendo unakujaje hapa, nikafuatilia mfano huu nilioutolea kwamba pale Arusha watu walikuwa wawili maana yake sisi wawili tulienda tu kuunga mkono lakini nikafuatilia kikao kilichofanyika nje ya nchi Watanzania walikuwa zaidi ya thelathini. Kwa hiyo, maana yake hapo hakukuwepo na uzalendo kulikuwepo na ubinafsi zaidi

ya kwamba ukienda nje kidogo nadhani kuna nyongeza nyongeza nyingine ambazo ni zaidi ya mkutano ukifanyikia ndani ya nchi. Kwa hiyo, kwenye hili tunapokwenda kwenye hizi fursa ni lazima tuwe *aggressive*, lazima tuwe *serious* na si kuwa waoga ni lazima tuwe *serious* hapo ndipo tutakapoweza kuzivuna fursa hizi kwa sababu vinginevyo hatutakuwa pazuri.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningeomba nilisemee linahusu taratibu gani zitawekwa kuzuia utoroshwaji wa mitaji kwenda nje ya nchi, Wabunge walizungumzia hili suala la *capital flight*. *Capital flight* inakuwepo iwapo kuna tofauti kubwa za kiuchumi kati ya nchi wanachama. Sisi tunapoongelea kiutaalam kuunganisha hizi nchi na vile vigezo vya *convergence* vinavyowekwa kwa namna moja vinasaidia kupunguza utoroshaji wa mitaji kwa sababu kama kutakuwepo na uwiano wa mwenendo wa uchumi, hii inasaidia kuwa na *capital gain* badala ya kuwa na *capital flight* kwamba hakuna motisha ya watu kutorosha mitaji kwa sababu kule anakotaka kupeleka nako kuna uwiano na anakotoka. Kwa hiyo, kufanya tathmini ya kuandaa mpango wa kuondoa vikwazo vyenye urari wa rasilimali ikiwa ni pamoja na kuboresha Sheria za Usimamizi wa Fedha za Kigeni ya mwaka 1992 na Kanuni za Fedha za Kigeni za mwaka 1998, vyote vinalenga, pamoja na kwamba tunaingia kwenye itifaki ya aina hii, tuwe tumesaidia nchi kutokuingia kwenye hasara hiyo ya utoroshaji wa mitaji.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa sera madhubuti za kiuchumi zitakazoleta utulivu wa uchumi mpana yaani *macroeconomic stability,* ni moja ya sera ambazo tunategemea zitasaidia kudhibiti mfumuko wa bei na hivyo kuwa na uwiano katika hizi nchi na kufungua biashara zenye usawa na kuimarika kwa thamani ya shilingi na kuweka mazingira mazuri katika kusimamia riba, utakumbuka ni jambo ambalo limezungumziwa sana katika Bunge wakati tunaleta bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa nidhamu ya matumizi, ni jambo lingine ambalo lilisemwa, kuongezeka kwa mapato ya Serikali na kupungua kwa nakisi ya bajeti. Ni vile vigezo ambavyo tunategemea tunapokuwa tunalenga kufikia haya malengo mapana ya *SADC* na ya Afrika Mashariki, kuna jambo la mfumuko wa bei, kuna jambo la nakisi lakini kuna jambo la uchumi mpana. Kwa hiyo, hii inaihakikishia kwamba Tanzania inatekeleza makubaliano ya kufikia viashiria vya kiuchumi wa jumla ambavyo kila mwanachama anatakiwa kufikia endapo atakuwa amenuia kwenda kwenye hiyo kuwa na asilimia 4.2 na nakisi ya bajeti ya pato la taifa *(budget deficit ratio to DGP),* hii itatuhakikishia kwamba makubaliano yanazingatia viashiria vya kiuchumi na kupungua kwa nakisi ya urari na biashara ya nje pamoja na mauzo ya nje na hii inaweka pia uwiano hata katika mambo ya kukopa. Kwa hiyo, tunapokuwa tunatekeleza hivi, tunakuwa na faida ambazo kama taifa tunaendelea kuzipata.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mojawapo ya kazi ambayo inatakiwa kufanyika ni kuainisha tofauti za vivutio katika ukanda na kupendekeza namna ya kufikia viwango vya uwiano na aina ya vivutio kwa wawekezaji na maeneo ya kimkakati ili kuiweka nchi katika nafasi ambayo itafaidi katika uwepo wa itifaki hii pamoja na hatua nyingine ambazo zinategemewa kuwepo. Kwa hiyo, kama Tanzania inaweza kutumia vivutio mbadala na tafiti nyingi zilishafanywa. Kuna tafiti za Benki ya Dunia, za *USAID* na wameongelea kwamba upatikanaji wa huduma za kijamii kama vile maji, umeme wa uhakika na barabara, ni moja ya vitu ambavyo vitafanya Tanzania iwe kivutio cha uwekezaji na hivyo kuweza kuifanya Tanzania inufaike na kuwepo kwenye itifaki hii. Kuwepo kwa amani na utulivu, ni jambo ambalo Mheshimiwa Msigwa alilisemea vizuri asubuhi na ni jambo ambalo ni la msingi sana katika mambo haya ya kwenda kwenye itifaki hizi na mahusiano ya kibiashara na yenyewe ni sehemu ambayo ni kivutio cha uwekezaji ambacho ni cha asili, cha lazima na si cha kimaslahi au kifedha lakini kina nafasi yake kubwa.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya uwekezaji kwenye sekta husika, hili lina uhusiano wa moja kwa moja na soko unapopima vivutio vya uwekezaji. Kwa hiyo, kwenye hili napo ni vyema Tanzania tukajitathmini na uwekezaji wa aina hii una *multiplier effect* kwamba upatikanaji wa malighafi hiyo maana yake unaenda mpaka kwa wazalishaji wa malighafi hiyo kwa hiyo ni kitu ambacho kinaweza kuleta faida kubwa kwa Taifa letu. Kwa hiyo, uwepo wa siasa safi na utawala bora ni jambo lingine.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia mimi nitoe rai tu kama nilivyosema awali kwamba lazima Tanzania tuwe *aggressive,* tuwe *pro-active* yaani tuchangamkie fursa lakini na sisi wenyewe tuhakikishe kwamba kila mmoja wetu anatimiza wajibu ambao anahusika na ambao utaleta tija kwa taifa letu na kuwezesha wananchi kunufaika na itifaki hizi.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache nitamke kwamba naunga hoja hii mkono na nakushukuru tena kwa fursa hii.

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa mtoa hoja, una dakika arobaini.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata fursa hii ya kuelezea maeneo ambayo Wabunge wengi wametushauri na wametupa changamoto vilevile kuendelea kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba kuchukua fursa hii kupitia kwako na kupitia Bunge letu Tukufu kumpongeza sana Katibu Mkuu wa *SADC*, Dkt. Stergomena Tax ambaye ni Mtanzania. Amekuwa pale muda mfupi lakini ameonesha utofauti wa utendaji. Mara ya mwisho mwezi Machi wakati tumekwenda katika mkutano wa Mawaziri wa Fedha wa *SADC* takriban Mawaziri wote walishangaa kutokana na kazi zake, ndiyo kwa mara ya kwanza Mawaziri kabla ya mkutano siku mbili wameweza kupata *document*s katika muda muafaka, wameweza kujadili na tumeweza ku-*conclude*. Kwa hiyo, ametupa heshima Kama Tanzania, tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja zote za Waheshimiwa Wabunge zilikuwa za msingi tunawashukuru sana. Kulikuwa na hoja moja ambayo Wabunge wengi waliizungumzia kuhusiana na kuchelewa kwa itifaki toka wakuu wa nchi waliposaini mwaka 2006. Tunakiri uchelewaji huo lakini kwa upande mmoja uchelewaji huo sisi kama Serikali ulitupa fursa ya kufanya utafiti na uchambuzi wa kina kuwashirikisha wadau kuona kwamba vipi tutaweza kwenda na hii *protocol* wakati sisi tuna *protocol* inayofanana katika Jumuiya hii ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, mchakato ulikuwa mrefu sana lakini wakati tunaendelea na *process* ya kufanya *analysis* na kushauriana na wadau lakini vilevile Tanzania nayo ilikuwa inakwenda katika mabadiliko ya kisiasa, mwaka 2010 tumekuwa na uchaguzi mkuu, kwa hiyo tulikuwa tunafanya hivyo na mpaka mwaka jana tukaifikisha hapa. Hata hivyo, ni kwa sababu tu ya kutaka kujiridhisha ili yale mambo ambayo tulikuwa tuna wasiwasi yasije yakaathiri mtengamano wetu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki lakini vilevile katika *SADC*. Hii ni changamoto na tunaichukua ili kwa *protocols* zinakuja tuziharakishe zaidi lakini tupate nafasi ya kuwashirikishe wadau kama inavyopaswa. Kwa hiyo, hili lilikuwa ndilo la msingi toka wakati ambapo tulisaini mwaka 2006 na Tanzania tulichukua na tulikuwa tukiifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, eneo umuhimu ambalo lilizungumziwa hususan na Kambi Rasmi ya Upinzani ni kuhusiana na Mahakama hii ya *SADC*. Kama ilivyoelezwa ilikuwa ni kweli kwamba Zimbabwe ililalamika kupitia vyombo vya *SADC* kwamba Mahakama ile ya *SADC* ilijinyakulia mamlaka ambayo haikuwa nayo katika kuamua ile kesi baina ya wawekezaji na Serikali. Kwa hiyo, ikakataa kutekeleza uamuzi wa Baraza hilo la *SADC* kwa msingi kwamba hilo ilikuwa si

jambo bayana kwenye mikataba ya ushirikiano wa *protocol* ya Baraza la *SADC* lilikuwa ni kati ya wawekezaji na Zimbabwe yaani ni nchi na wawekezaji wake. Kwa hiyo, kulitokea sintofahamu, kutokana na hayo wakuu wa nchi hizi za *SADC* wakawaagiza sasa Mawaziri wa Sheria na Wanasheria Wakuu kupendekeza marekebisho ya *protocol* kwa kuweka bayana kwamba migogoro ambayo itapelekwa pale yaani kwenye *SADC tribunal* itakuwa ni baina ya nchi na nchi zile zilizomo kwenye *SADC* kuliko baina ya nchi na watu binafsi ama makampuni. Kwa sasa *tribunal* haifanyi kazi kwa sababu kumekuwa kidogo na huo mkanganyano na vilevile Majaji wa *SADC* hawakuongezewa muda. Kwa hiyo, sasa hivi Wanasheria Wakuu pamoja na Mawaziri wanaohusiana na sheria wana-*negotiate* upya jinsi gani sasa *tribunal* itakuwa inafanya kazi. Kwa hiyo, huo ndiyo ulikuwa msingi mkubwa na kwa sasa *SADC tribunal* haifanyi kazi na kwa maana hiyo sasa utaratibu ukishakukamilika basi mapendekezo yatapelekwa kwa Marais kukubali, marekebisho yenyewe yataingizwa katika *treaty* ya *SADC* pamoja na *protocol* ili kushughulikia sasa migogoro ambayo itajitokeza lakini migogoro ambayo itajitokeza ni ile ambayo itakuwa ni baina ya nchi na nchi wanachama wa *SADC* na siyo kama vile ilivyokuwa imetokea Zimbabwe. Kwa hiyo, hilo nilikuwa nataka tu kuweka *clarification* hiyo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna eneo lingine, kulikuwa na wasiwasi pale tulipokuwa tumeeleza kwamba nchi tisa ndizo ambazo zimetia saini mkataba na kwa sababu *protocol* yenyewe inasema kwamba mkataba utakuwa *effective* ikiwa tu *two third,* sehemu mbili kati ya tatu, kwa hiyo ukilinganisha pale kwa nchi tisa bado itakuwa haijatimia. Wakati itifaki hii ilipokuwa inasainiwa, *actually* ilipata nguvu kisheria tarehe 16 Aprili, baada ya nchi tisa kati ya 14 za *SADC* zilizosaini itifaki hii kuwasilisha hati za kuridhia lakini kwa muda huo Madagascar ikawa imesimamishwa uanachama wake toka mwaka 2009. Kwa hiyo, mpaka kufikia Juni, 2014 nchi kumi na moja tayari zimesharidhia itifaki hii zikibaki sisi Tanzania, Zimbabwe na Seychelles. Kwa hivyo, utaona kwamba nchi kumi na moja kati ya zile kumi na nne, tayari zimesharidhia itifaki hii na kwamba kisheria ipo kwa sababu Madagascar ilikuwa imesimamishwa, haijaingia katika ile idadi ya nchi tisa katika kumi na nne. Kwa hiyo, kwa ufupi ipo kisheria.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna eneo ambalo Waheshimiwa Wabunge mmelisemea sana kuhusu utoaji huu wa elimu, tunalichukua, tutakuwa tunalifanyia kazi na kila tutapokuwa tunapata fursa, tutakuwa tunaelezana hususan kwenu kwa sababu ninyi mnawawakilisha wananchi na lazima wananchi wawe wanajua faida watakayopata kama wananchi wa kawaida katika kuridhia *protocol* hii. Wenzangu wamesema faida nyingi lakini sasa hivi zipo hizi fursa, ni kitu cha kuwaeleza wananchi kwamba hii maana yake ni kitu gani, hiki tunachokifanya maana yake ni kitu gani. Kweli alizungumzia sana Mchungaji Msigwa, kwa hivyo hili tunalichukua na tutakuwa tunalifanyia kazi. Wakati muafaka ambapo tutakuwa tunapata nafasi tutakuwa tunalizungumza kadiri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limezungumzwa nadhani na Mheshimiwa Mnyaa kwamba wapi tuna fursa zaidi sasa *SADC* ama *EAC*? Kwa sasa hatuwezi kusema kwamba tuchague wapi kuna fursa zaidi kwa sababu kila *block* ina faida zake. Tanzania tuko kwenye eneo la kimkakati, ukiangalia bandari yetu inatumiwa na nchi ambazo ziko Afrika Mashariki mfano Burundi lakini Tanzania bado tumepakana na wenzetu walio Kusini kwetu *SADC*, wanatumia vilevile zile *border post* ambazo tumezitengeneza, kwa hiyo, tunapata *advantage*. Mwenzangu kaeleza soko la Afrika Mashariki sasa hivi liko *around* watu milioni 125 lakini soko la *SADC* ukichanganya pamoja ni watu milioni 300. Kwa hiyo, hiyo ni *advantage* nyingine, yako mengi zaidi. Kwa sasa Tanzania hatuwezi kusema tunachagua moja tunaacha nyingine lakini kikubwa kwamba tunafaidika kote, *SADC* tunafaidika, *East Africa* tunafaidika. Tuna historia yake maalum kwenye *East Africa* lakini Tanzania huwezi kufuta kazi iliyofanya kwa uhuru wa Nchi za Kusini mwa Afrika. Sisi ni *unique,* Tanzania ni *unique* pale hatuwezi tukaacha tu hivi hivi au tuseme tunachagua moja kwingine hapana. Kwa hivyo, kote kuna faida zake lakini kwa sababu kuna yale maeneo ambayo pengine yanatofautiana au yanayoleta ukakasi ndiyo

maana kuna kitu kinaitwa *triple treaty* yaani ni mazungumzo baina ya Afrika Mashariki, *COMESA* na *SADC* ambapo tutaweza ku-*harmonize* mambo mengi ili yasije yakakwazana katika hizi *blocks* ambazo tumejiunga. Wenzetu Kenya wako *COMESA* lakini wako Afrika Mashariki, sisi tuko *SADC* lakini tuko Afrika Mashariki. Kwa hivyo, inategemea nchi inaji-*fit* vipi katika *blocks* hizi lakini zote zinakuwa ni muhimu kwa faida ya nchi.

Mheshimiwa Leticia Nyerere alizungumza vizuri na wenzangu wamelizungumzia vizuri.

Mheshimiwa Lolesia Bukwimba yeye aliulizia kuhusu habari ya soko. Nadhani ametoa maelezo mazuri kwamba faida nyingine kubwa ambayo inajitokeza ni kuwa na soko pana zaidi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tushirikiane katika kuwaelimisha wananchi kupitia vikundi vyao vya ushirika kwamba hizi ndizo fursa ambazo zinapatikana. Kwa sasa kupitia Wizara yetu ya Viwanda na Biashara kuna kitu tunaita *simplified trade regime* yaani ni zile fursa ama michakato ambayo iko *simply* sana bila kufuata hizi *process* ambazo ziko *completed* za kisheria. Kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara, wananchi wanayo fursa ya kuweza kufanya biashara na nchi ambazo ziko *SADC* kwa kutumia hizi *simplified trade regime*. Kwa mfano, bidhaa kama mahindi, maharage, vitu ambavyo haviko *complicated* basi hii fursa ipo na hii inaratibiwa na wenzetu Wizara ya Viwanda na Biashara nadhani kwa pamoja kama Serikali tutashirikiana sasa kutoa hii elimu ili kusajihisha wananchi wazalishaji kutumia fursa hizi. Bado kuna *guidelines* zinazomwezesha mfanyabiashara mdogo tu kuweza ku-*trade* baina ya nchi zetu *within East Africa as well as SADC*.

Mheshimiwa Spika, lakini faida nyingine ambayo inapatikana hapa ni kwamba sasa hivi tuko kwenye *free trade area* yaani lile eneo huru la kibiashara, vikwazo vinaondolewa, kwa hivyo wafanyabiashara wetu nchi wanaweza kwenda sehemu nyingine. Sasa hivi Tanzania tunajitahidi sana katika kuondosha hizi *non trade barriers* kuweza kuhakikisha kwamba wananchi wetu wana-*move* na wananchi wa nchi nyingine wanakuja. Cha msingi na cha muhimu Watanzania ni lazima tuzichukue hizi fursa. Wenzetu wako *more advance* wanachukua hizi fursa sana na wanazitumia na sisi tuwe tunazichukua fursa hizi na tuzitumie kwa maslahi ya wananchi lakini kwa maslahi ya Taifa kwa ujumla. Soko linapanuka, vikwazo vya biashara vinaondoka, kwa hiyo tuchukue *advantage* ya kuzalisha zaidi ili kupeleka kule kwingine ambako kuna mahitaji zaidi, sisi tutaendelea kutoa elimu ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, eneo zuri ambalo liko *more practical* ni kuhusiana na uanzishwaji wa *One Stop Border Post*, tumekuwa tukizianzisha *post* hizi kwenye zile sehemu za forodha ambazo ziko mipakani ambazo zinaweza kurahisisha biashara baina ya watu wetu na baina ya watu wa nchi nyingine. Kwa mfano, Malawi tumetia saini na kesho kutwa tunaanzisha hii Zambia, Tunduma kule watu wanafanya kazi vizuri. Kwa hiyo, hizi ni fursa za kuweza sasa kurahisha biashara baina ya *blocks* zetu ambazo Tanzania zipo.

Mheshimiwa Spika, jambo la msingi sasa hivi tunakokwenda katika hii *globalization* ni kwamba mataifa makubwa yanatizama zaidi *region,* yanatizama zaidi ile kanda kuliko kuangalia nchi moja, moja. Tumekwenda katika mikutano ya *African Development Bank* (Benki ya Maendeleo ya Afrika), kinachosisitizwa kule ni kwamba sasa hivi nchi zikae kwa pamoja ili tuweze sasa kufanya miradi ya pamoja hususan ya miundombinu sasa hivi ndiyo mtazamo wa dunia. Kwa hiyo, Tanzania lazima na sisi tuchukue fursa hii kwamba tukiwa tuko peke yetu pale, kuna fursa nyingi ambazo tutazikosa. Sasa hivi mtizamo dunia uko kwenye *regional integration* na *harmonization,* huko ndiyo tunakokwenda. *East Africa* tuna miradi yetu ambayo kama *region* tunaifanya kwa pamoja, miradi ya umeme, miradi ya barabara. Vilevile tunakokwenda *SADC*

nayo kutakuwa na miradi ya barabara kuziunganisha nchi ambazo ziko kwenye *SADC* na hilo ndilo ambalo tunalitaka ama ambalo linatakiwa sasa hivi katika mtazamo wa kidunia.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, tusiache hii fursa tuliyokunayo kwa kuogopa lakini tuwe na nguvu zaidi ya kwenda kuchukua hizo fursa kusimama zaidi. Kuna changamoto zake kwa sababu tuna hofu maana kama binadamu lazima utakuwa una hofu, lakini hapana, hofu tuijenge lakini tuchukue ile hofu kwamba ndiyo nafasi zaidi ya kujiweka vizuri zaidi katika uchumi wetu kwenda mbele zaidi. *Otherwise* kama tutakuwa tumekaa sisi peke yetu, hizi fursa zitatukimbia na wenzetu watakuwa wanazichukua.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusiana ni *single currency* limeelezewa lakini kikubwa ukichukua Afrika Mashariki, ukichukua *SADC* kote kuna *single currency*. *Process* ya Afrika Mashariki kuwa na *single currency* iko hatua mbele zaidi na wiki ijayo tutapata fursa pia ya kuona hiyo *protocol* ya *monitory union* iko mbele zaidi na sisi kuna maeneo ambayo tayari tumeshayafikiria kuyatekeleza. Kuna maeneo ya takwimu, kuna maeneo ya benki na kadhalika. Tulichojiwekea sasa hivi ni kwamba *single currency* ya Afrika Mashariki iwe tayari imefikiwa miaka kumi baada ya kuridhiwa, kwa hiyo *tentatively* tunaweka hapa labda 2024 ndiyo *single currency* itaanza. Hapa kwenye *SADC* imewekwa 2018 lakini hakuna kitu ambacho tumekifanya.

Mheshimiwa Spika, sasa *process* yetu ambayo tunakwenda nayo kwenye Afrika Mashariki hatuwezi kabisa kuachana nayo, ni *process* nzuri na inatufanya sasa tujiweke tayari kwa ajili ya utengamano wetu wa Afrika Mashariki lakini itakapokuja huku hata kama tutaingia katika hatua hii bado Tanzania itakuwa na fursa ya kuchagua, kama huku tutakuwa tulishaingia kwenye *currency* moja na Afrika Mashariki basi huko tutakuwa hatuna haja, hatufungwi kwamba lazima kwenye *SADC* nako tuingie kwenye *single currency*, haiwezekani nchi moja ikawa ina *currencies* mbili kama ndiyo fedha yake. Kwa hiyo, hilo hatuna wasiwasi nalo tutakwenda vizuri na kama nilivyosema kwamba tukiridhia haya, kuna maeneo ambayo tunaweza tukaenda nayo *with reservation* yaani tunakwenda na angalizo. Kwa hiyo, hizo ndizo *processes* mbili ambazo tunakwenda nazo, wakati tunasaini ama tuna-*ratify protocol* hii kuna maeneo ambayo bado tutakuwa hatujatekeleza lakini vilevile Afrika Mashariki kuna maeneo ambayo tutakuwa tumeshayatekeleza kwa nafasi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelizungumzia kuhusu ushiriki wa Serikali katika *blocks* mbili, tuko vizuri, tumejipanga vizuri tunashirikiana kotekote. *SADC* kuna maeneo yake ambayo tunashirikiana lakini vilevile *East Africa* kuna maeneo ambayo tunashirikiana lakini maeneo mengi yanafanana na ndiyo maana sasa kukawa kuna hayo mazungumzo ya utatu *(triple treaty)* kati ya *COMESA*, Afrika Mashariki pamoja na *SADC* kwa sababu ni mambo mengi ambayo tunafanana. Kwa hiyo, hilo halina tatizo sana.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna swali kwamba ni nchi gani za *SADC* ambazo zina uwezo zaidi kiuchumi ikilinganishwa na Tanzania, zipo. Kwenye *SADC*, Afrika ya Kusini ndiyo Taifa ambalo lina uwezo zaidi kiuchumi kuliko nchi zote wanachama zikichanganywa pamoja. Peke yake kwa takwimu za mwaka 2012, pato lake ni dola za Kimarekani bilioni 357 ambalo ni asilimia 60 zaidi ya wanachama wote wa *SADC*. Vilevile Tanzania bado ni nchi mojawapo ambayo nayo ina nguvu zaidi katika *SADC* ikiwa ni ya tatu, sasa hivi tuko katika dola za kimarekani karibu bilioni 22, Angola wenzetu wametangulia zaidi. Kwa hiyo, hii nayo kuwa wa tatu si mbaya lakini bado inatupa changamoto ya kutumia fursa vizuri hususan fursa za kujenga viwanda zaidi hapa nchini. Kwa sababu Afrika Kusini imejikita zaidi katika uzalishaji viwandani na kuuza, kwa hiyo pato lake ni bilioni 357 wako mbali. Wenzetu sasa hivi wanajikita sana katika masuala ya uchumi hususan tutaona kwamba nchi ambazo zimetoka kwenye *conflict* zina *concentrate* sana

kwenye masuala ya kiuchumi, Tanzania sisi tuko vizuri kwa muda mrefu, amani imetawala nchi yetu kwa hiyo fursa kwetu ni kubwa zaidi katika kuwekeza kwenye uchumi. Ni vizuri tuko namba tatu lakini bado tuna kazi ya kufanya na kwa maana hiyo sasa ndiyo inatupa mwanga zaidi wa kutumia hizi *regional integration initiatives* ili kuweza kujiweka vizuri kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, lingine lililoulizwa ni kwamba, je, itakuwaje kama hatutaridhia *SADC*, fursa zilizokuwepo sasa tutakuwa hatuzipati tena. Uzuri wa hili jambo ni kwamba tumelifanyia *analysis* ya kutosha ni jambo zuri, changamoto tuliyokuwa nayo ni kwamba je, wananchi watachukua nafasi gani katika kutumia fursa zinazojitokeza lakini hapa bado hatuja-*ratify* lakini kuna taasisi ambazo zinashirikiana vizuri zaidi. Kwa mfano, kuna *network* ya Benki Kuu za nchi za *SADC,* ziko vizuri zimewekeana mikakati, kuna *microeconomic indicators* ambazo wamewekeana wao wenyewe kuweza kuzifuata na taasisi zetu za bima zinafanya vizuri sana kwenye eneo hili la SADC. Kwa hiyo, faida tayari zimeshaanza kuonekana, hatukuridhia *protocol* hii lakini bado kuna faida ambazo zimeanza kuonekana. Wanapata *capacity building* yaani wanawezeshwa zaidi katika maeneo haya ya *training* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ubaya wake ni kwamba kwa sababu hatujaridhia kisheria Tanzania haiwezi ikatoa maamuzi na yakasikilizwa na kutekelezwa. Wao wenyewe wanashirikiana, kuna *corporation* nyingi wanashirikiana, tunafaidi sote lakini hatuwezi sasa mawazo yetu yakasikilizwa pale kwa sababu hatujaridhia *protocol* hii. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ndiyo tumeleta hapa ili turidhie ili sasa mahusiano ya taasisi zetu yaweze kukua na baadaye sisi kama Tanzania tuwe tunatoa mawazo yetu vile ambavyo tunasikia kwamba hivi ni sawasawa na yawe yanasikilizwa. Sasa hivi tunashiriki lakini katika maeneo ambayo siyo rasmi ingawa tunafanya vizuri lakini bado hakuna nguvu zile za kisheria ambapo mawazo yetu yanaweza yakasikilizwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja ambayo ilikuwa inaelezea kwamba hakuna kifungu pindi nchi mwanachama itakaposhindwa kutekeleza yale yaliyokubaliwa kama ni adhabu au hatua au vikwazo gani vinatakiwa kuchukuliwa dhidi ya nchi hiyo. Itifaki yetu hii inajielekeza zaidi katika utaratibu wa maridhiano na nchi wanachama kuwajibika katika kutekeleza matwaka ya itifaki hii kwa kuzingatia manufaa yatakayopatikana.

Mheshimiwa Spika, kuna Ibara hii ya 25 ya Itifaki inasema kila mwanachama wa Jumuiya hii anao wajibu kwa ridhaa yake kuhakikisha anatekeleza makubaliano ya itifaki kwa manufaa ya nchi wanachama. Kwa hiyo, maridhiano ndiyo kwanza yanachukua nafasi zaidi kuliko kuweka adhabu au kuweka hatua kwa nchi wanachama. Hata hivyo, hizi taasisi vilevile zinazoshiriki na wao wamewekeana utaratibu wa kufanya kama taasisi ya nchi fulani haikuwajibika. Kwa hiyo, vipangele viko hapa, kuna *Article* nzima ambayo inaelezea ni jinsi gani hatua zinaweza zikachukuliwa lakini inaelezea kwanza hatua muhimu ni kwa nchi kuweka maridhiano mbele kwa maslahi ya nchi yake pamoja na wananchi ambao wapo katika *region* yenyewe.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihusu Ibara ya 3, Nyongeza ya Kwanza ya Itifaki inayoelekeza nchi wanachama kuratibu taratibu zao za uwekezaji na kushirikiana katika kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji katika Kanda, ilionekana kama inapingana na nyongeza ya kwanza ya Itifaki inayohamasisha nchi wanachama kuhamasisha uwekezaji katika eneo lake na kuruhusu vitega uchumi husika kufuatana na sheria na kanuni za nchi yake. Tunaingia katika eneo moja, tunaingia katika *region* moja lakini kuna nchi tofauti na hii haikatazi kwa nchi moja kuwa na mazingira mazuri ya uwekezaji. Lazima uweke mazingira mazuri ya uwekezaji katika nchi yako na wala haimaanishi ukiweka mazingira mazuri kwamba ndiyo unashindana na mwenzio, hapana. Kwa sababu kama *block* mtakuwa mnafanya biashara ninyi kwa ninyi lakini vilevile kama nchi itakuwa na fursa ya kufanya biashara na wengine ambao hawako kwenye

*block*. Kwa hiyo, hiyo inakupa changamoto ya wewe kuweka mazingira mazuri sana ya biashara katika nchi yako.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo linaruhusiwa na sisi tujikite zaidi katika kuweka mazingira bora zaidi katika nchi yetu ili kuvutia wawekezaji kwenye *SADC* vilevile kuvutia wawekezaji ambao wanatoka nje ya *SADC* na vifungu viko *clear* wala havikinzani kabisa. Hili limewekwa mahsusi kwa kujua kwamba, hata kama tutaridhia *protocol*, hata kama tutakuwa kama *block* moja bado maendeleo ya nchi yanawahitaji wengine ambao hawapo kwenye *block,* waje kuwekeza na sisi ndivyo ambavyo sasa hivi tunafanya. Tuna wawekezaji wengine wengi ambao si tu wanatoka kwenye *SADC* lakini wanatoka katika maeneo mengine. Kubwa ni kwamba tuweke mazingira bora ya uwekezaji Tanzania ili kuweza kuvutia zaidi wawekezaji ambao wanawekeza kwetu.

Mheshimiwa Spika, nadhani mengi yameshasemwa, utoroshaji wa mitaji nadhani limeelezwa lazima kama nchi tuwe tunajikita zaidi katika kupanua fursa za uwekezaji kwa kuweka mazingira zaidi ya uwekezaji *otherwise* mtaji utaweza kuondoka. Kama tuna fursa nzuri ya kuwekeza hapa nyumbani, nadhani kutakuwa hakuna haja ya mtaji kuondoka.

Mheshimiwa Spika, kuna eneo lingine kuhusiana na mikataba ambayo Tanzania imeingia. Je, itakinzana vipi na sisi tukiingia kuridhia hii *protocol*? Hapa hakuna matatizo, bado *protocol* inaruhusu kuingia mikataba ya nchi na nchi, *bilateral agreements* bado zinaruhusiwa. Kwa hiyo, mbali ya kuwa tutakuwa katika *protocol* hii lakini tutakuwa vilevile tuna fursa ya kuwa na ushirikiano baina ya nchi moja ambazo zimo kwenye *SADC* na hilo halina shida yoyote. Hata hivyo, napenda niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba mikataba kama hii mara nyingi ilikuwa iko katika himaya za kiutendaji zaidi, kwa hiyo, si ile mikataba ambayo inafunga nchi kwa maana hiyo kulikuwa na toleo la Mwanasheria Mkuu kwamba mikataba kama hii ya kibiashara bado iko katika mamlaka ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, vilevile kulikuwa na hoja kwamba kwa nini Serikali imesaini mikataba hii kabla ya kuridhia Itifaki. Ndiyo kama nilivyosema kwamba, hata hiyo itifaki yenyewe haizuii nchi kuweza kusaini mikataba na nchi nyingine, mradi tu sheria na taratibu zote zimefuatwa. Tunayo mikataba ya biashara kati ya Malawi na Tanzania, tunayo mikataba ya biashara na Zimbabwe na vilevile tunayo mikataba ya kiabisahara kati yetu na Afrika ya Kusini, hii tumeweza kusaini na tunaitekeleza kabla hata ya itifaki yenyewe haijasainiwa.

Mheshimiwa Spika, mengi yameelezewa labda la mwisho Mheshimiwa Terezya Huvisa alitaka tu kujua faida gani ambayo tutapata sasa. Tumeshasema soko la bidhaa litakuwa kubwa zaidi, watu wetu wa ndani sasa watakwenda kupata fursa za soko kwenye nchi nyingine za *SADC*. Pia, tutapata fursa za kuweka vivutio kwa uwekezaji maana tutakuwa tunapata changamoto sana ya kujikita zaidi katika kuweka vivutio vya uwekezaji. Vilevile ushindani ule wa kimataifa nao utatusaidia katika kujiweka sawa kiuchumi, tutakuwa tuna-*compete* lakini ndipo ambapo tutajiweka sawa katika kuweka mambo yetu vizuri zaidi. Tukiruhusu itifaki hii wananchi wetu ama sisi wenyewe wakati tunatafuta bidhaa kupata bidhaa ambazo zitakuwa ni bora na za unafuu zaidi maana soko litakuwa pana zaidi lakini kwa sababu ya ushindani ina maana kila soko sasa, ama kila wawekezaji watakuwa na changamoto ya kuweza kufanya bidhaa zao ziwe bora zaidi. Kwa sababu itifaki hii vilevile inatoa fursa ya kufanyiwa *review* kutokana na hizo *microeconomic convergence* yaani vile viashiria vya kiuchumi. Maana ukiwa umeingia katika *protocol* hii maana yake ni kwamba sasa wewe utakuwa katika nchi ambazo zinafanyiwa *review*. Maana hiyo, kama tumejiwekea *inflation* yetu iwe chini ya asilimia tano, maana yake tutajitajitahidi sasa tuwe chini ya asilimia tano, umekwenda mbele kidogo

wenzako watakuambia hapana uko juu zaidi na vitu vingine kama hivyo. Kwa hiyo, *performance* yetu tunatarajia itakuwa nzuri kwa sababu sasa tutakuwa tunakuwa *reviewed*.

Mheshimiwa Spika, utandawazi, *globalization* nayo ndiyo inachukua nafasi yake. Sisi kama Tanzania siyo kisiwa lazima sisi tufanye biashara, tuwe pamoja na wenzetu. Lingine ni fursa za kazi na ajira, mfano umetolewa, Watanzania wengi wako katika nchi nyingine lakini wakati huohuo nao tunaingia kwenye *protocol* na wengine watakuja kwetu. Kitu cha muhimu ni kwamba tuwekeze sana kwenye *vocational training* ili na sisi tuwe tunapata fursa zaidi. Kama kwetu hakuna fursa basi wengine watakuwa na fursa na hilo litapelekea ajira lakini vilevile litapelekea sasa Tanzania kupata mapato zaidi *in the form of remittances* kwetu sisi. Faida ziko nyingi lakini kama Tanzania tunatakiwa kuchukua fursa hii. Wenzetu wanazitaka hizi fursa, wameshaona faida zamani sana, kwa hiyo na sisi Waheshimiwa Wabunge tujitahidi, sisi kama Serikali tuwe tayari kutoa elimu mara kwa mara ili sasa na sisi twende kwa wananchi wa ngazi ya chini kuwaambia faida itakayopatikana na nini hasa kifanyike na wao wana *role* gani katika kuchukua fursa hizi ambazo zinajitokeza kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, nadhani tumemaliza majibu yote labda kama kutakuwa kuna hoja nyingine tutazileta kama tutakavyoambiwa. Baada ya maelezo hayo sasa, naomba Bunge lako Tukufu liridhie Itifaki ya *SADC* ya Fedha na Uwekezaji *(The SADC Protocol on Finance and Investment)* ili Tanzania iweze kunufaika na hivyo kujenga uchumi imara na endelevu na kupunguza umasikini nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

**SPIKA:** Hoja hii imeungwa mkono na kufuatana na Kanuni ya 57 na 58, hakuna mtu aliyeleta mapendekezo ya kufanyia mabadiliko maazimio haya, sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Kuridhia Itifaki ya SADC ya Fedha na Uwekezaji (The SADC Protocol on Finance and Investment)*
*liliridhiwa na Bunge)*

**SPIKA:** Tuwashukuru Waziri wa Fedha na Naibu Mawaziri wake pamoja na wataalam wao kwa kazi nzuri. Kikubwa siyo kupitisha Azimio, kubwa ni kuchukua fursa ambazo ziko kati yetu. Fursa zichukuliwe si tu na Serikali lakini na Watanzania waanze kujifungua na waanze kuona fursa zilivyo nyingi katika nafasi yetu. Kwa hiyo, nawatakiwa kazi njema.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nitambue wageni ambao wameingia jioni hii, hawa ni Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Ruaha (*RUCO*) kilichopo Iringa Mjini, Wanyalukolo hawa, naomba wote wasimame mahali walipo.(*Makofi*)

Hawa Wanyalukolo kati yao pia yupo mtoto wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Aggrey Mwanri. Kwa hiyo, tunashukuru. Sisi tunafurahi kuwaoneni, leo ni Ijumaa ndiyo siku yetu tunapumzika mpaka Jumatatu lakini kikubwa tunaomba, hizi fursa zote tunazosema zitategemea ninyi wenzetu mkisoma vizuri, ninyi ndiyo fursa zenu hizi. Humu ndani kuna wengine saa kumi na moja, wengine saa kumi na mbili lakini ninyi mko asubuhi. Kwa hiyo, asubuhi yenu ni tofauti sana kuliko asubuhi zetu za zamani. Kwa hiyo, nawatakia kheri sana,

msome kwa bidii bila vikwazo vyovyote vile kwa sababu hizi ndizo fursa tunazosema, karibuni sana. *(Makofi)*

Matangazo mengine, asubuhi nilisema kesho saa kumi tuna mchezo wa mpira kati yetu na Akiba *Commercial Bank*. Kesho kutwa tarehe 8, tutakuwa na mchezo wetu kati yetu na Madiwani wa Dodoma. Kwa hiyo, wote mliopo hapa mnakaribishwa kwenye uwanja huo mkaone mambo yenu, msilete hapa watu walioshindwa, maana mkishindwa sitangazi, kwa hiyo, nategemea kwamba mtafanya vizuri. *(Kicheko)*

Tangazo lingine la kiutawala tu, mmepokea makabrasha mengi sana humu ndani, sasa mnayaacha humuhumu kwenye *floor* kwa hiyo *weekend* kufagia inakuwa vigumu. Sasa nawaombeni kila mtu aondoke na makabrasha yake isipokuwa muache vile vitabu vya bajeti kwa sababu kazi bado lakini mengine yote nendeni nayo huko kwenu. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, msije mkaacha halafu wakachukua hawa wafagiaji, wakapoteza vitu vyenu ambavyo ni *valuables,* hamtaweza kuviona tena. Kwa hiyo, naomba sana mchukue, muende navyo. Hata kwenye *pigeon holes* kuna *documents* nzuri sana, wengine huwa wanaacha hukohuko halafu inakuwa tena mzigo kwa ofisi.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza niwashukuru sana, mmefanya kazi nzuri sana wiki hii, naomba tu kesho muweze kupumzika ili tuanze siku ya Jumatatu ambapo tutakuwa *protocol* nyingine ya Afrika Mashariki kuhusu mambo haya ya fedha na tutakuwa na uchaguzi mdogo kati yetu.

Kwa hiyo, nawashukuru sana, nawatakia *weekend* njema, naahirisha kikao cha Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 12.15 jioni Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatatu,*
*Tarehe 9 Juni, 2014, Saa Tatu Asubuhi)*